# Mkristo na Ndoa

Mwandishi
**Paul L. Canner**

Kimetafsiriwa Katika Kiswahili na

George Opara na Kikundi Chake
S.L.P. 2245, Kitale, Kenya

na

Kitula G. King'ei
Kenyatta University
S.L.P. 43844, Nairobi, Kenya

**MOMENTS WITH THE BOOK**
PO Box 322 • Bedford, PA 15522
(814) 623-8737 • www.mwtb.org

Madondoo kutoka katika Biblia yametolewa katika "King James" isipokuwa machache kutoka katiak tafsiri mpya ya J.N. Darby (yalioonyeshwa kwa herufi, "JND").

Kimechapishiwa Marikani

# *Yaliyomo*

Utangulizi . . . . . 4

**1.** Kuchaguwa Mchumba . . . . . 5

**2.** Kujitayarisha Kwa Ndoa . . . . . 10

**3.** Mambo Muhimu Kwa Furaha Katika Ndoa . . . . . 14

**4.** Kuoana na Mtu Asiyekuwa Mkristo . . . . . 25

**5.** Talaka na Kuoana Tena:Mafunzo Muhimu . . . . . 29

**6.** Talaka na Kuoana Tena: Miongozo Kuhusu Hali Halisi . . . 35

**7.** Talaka na Kuoana Tena: Nidhamu Katika Ushirika na Kurudia Ushirika . . . . . 45

**Nyongeza 1.** Kabla Hujafunga Ndoa . . . . . 52

**Nyongeza 2.** Watu Wafaao Kuoana . . . . . 58

**Nyongeza 3.** Kupotoka kwa Ndoa . . . . . 60

# *Utangulizi*

Nilipokuwa nikipitia gazeti hivi karibuni jicho langu lilitekwa na kifungu kilichosema kwamba watu "wanaoana na kuachana kwa wingi sana … familia ya Kimarikani imo hatarini kwa sababu ndoa za kimarikani zimejaa migogoro." Takwimu za mwaka wa 1980 zinatueleza kuwa kiwango cha talaka katika nchi ya Marikani kimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 50% ya ndoa zote zinazofanywa katika mwaka mmoja. Pia maandishi mengine yanaonyesha kwamba kiwango cha talaka Marikani ni kikubwa kuliko cha taifa lingine lolote ulimwenguni. Bila shaka hili ni tatizo linaloikumba dunia nzima hivi leo.

Maelezo ya namna hii yanasikika kila mara hivi kwamba hayatushitui wala kutushangaza tena. Hata hivyo, tabia na mienendo inayoonyeshwa na maelezo kama haya ni ya kusikitisha sana kwa Wakristo na wasiokuwa Wakristo pia. Mwandishi wa kifungu cha kwanza kilichotajwa hapo juu aliendelea na kutoa suluhisho kuhusu tatizo hili. Suluhisho lilikuwa zuri kiasi kwani lilisisitiza haja ya wenye kuoana kukuza uhusiano thabiti. Hata hivyo, kama mapendekezo yote yatolewayo katika vyombo vya habari siku hizi, suluhisho hili lilikuwa na upungufu kwani lilipuuza upande wa maisha ya kiroho katika uhusiano wa ndoa na ushauri ambao Mungu ameutoa katika hekima yake kupitia Neno lake takatifu.

Kwa bahati mbaya, kadiri ulimwengu unavyozidi kutumia njia, viwango na mienendo isiyohusiana na Neno la Mungu juu ya ndoa na talaka, ni lazima mabadiliko yatatokea—pengine tayari yametokea—katika jamii ya Wakristo pia. Mambo ambayo yalitushitua sana miaka ishirini iliyopita leo yanakubaliwa bila tatizo katika jamii nyingi za Kikristo. Kuna vikundi vingi vya kilimwengu na kishetani ambavo vimekazana kuharibu uhusiano wa ndoa na wa kifamilia. Kwa hivyo, ni kutokana na dharura hii kuhusu ndungu na dada katika Kristo, pamoja na dunia yote kwa jumla ndipo nikachukua mzigo wa kukiandika kitabu hiki juu ya Mkristo na ndoa.

# 1
# *Kuchaguwa Mchumba*

Bila shaka jambo muhimu zaidi linaloleta furaha ya kudumu katika ndoa ni uchaguzi ufaao wa mchumba. Nina hakika kuwa Mungu analichukulia jambo hili kuwa muhimu sana kwa kila aliye mtoto wake. Sio tu kwamba Mungu ametoa mwongozo kuhusu uchaguzi wa mchumba katika neno lake bali pia yuko tayari kutuongoza iwapo tutamruhusu—kutuelekeza kwa mchumba ambaye Mungu, katika hekima yake kuu, anamjua kuwa anafaa zaidi kuwa mwenzi wetu katika maisha. Uchaguzi wa mchumba wa Isaka (Mwanzo 24) ni mfano mzuri wa jambo hili.

Je, tunawezaje kuyaelewa mawazo ya Mungu kuhusu mchumba wa ndoa? Kwanza, Neno la Mungu linatupa mwongozo kuhusu mahali pa kuanzia na jinsi ya "kutafuta."

## Miongozo ya Kijumla

Ni jambo lililo wazi katika Biblia kuwa kwa vyovyote vile, Mkristo hafai kuoana na mtu asiyekuwa Mkristo. "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja isipokuwa wawe wamepatana?" (Amosi 3:3). "Msifungwe nira moja na watu makafiri; kwani pana uhusiano gani kati ya watakatifu na wenye dhambi? na pana ushirika gani kati ya nuru na giza? na pana umoja gani kati ya Kristo na Shetani? au fungu gani kati ya muumini na asiyeamini?" (2 Wakorintho 6:14,15). Taifa la Waisraeli lilionywa mara nyingi lisioane na wanawaume na wanawake wa mataifa mengine jirani, sababu, "watawapotosha wana wenu wasinifuate ili kuwatumikia miungu wengine" (Torati 7:1-4). Maonyo haya bado yanahitajika na wana wa Mungu hivi leo kama hapo kale.

Kifungu kingine chenye funzo sawa na hiki ni 1 Wakorintho 7 kisemacho kuwa ndoa iwe tu "katika Bwana." Bila shaka funzo hili linahusu fikira kwamba Mkristo aliyezaliwa upya anapaswa kuoana tu na Mkristo aliyezaliwa upya. Lakini kuna fikira nyingine katika kifungu "katika Bwana." Tunapaswa kumtafuta mchumba ambaye sio tu kwamba ameokoka bali amejitolea kuishi katika Kristo, akiwa naye kama Bwana wa maisha yake, akifanya mapenzi ya Mungu Baba na kujawa na Roho Mtakatifu.

Mwongozo huu unaweza kutuchukua hatua nyingine mbele zaidi hasa tukifikiria kwamba mke wa Isaka angechaguliwa kutokana

na ukoo wa baba yake (Mwanzo 24:3,4) na binti zake Selofehadi waliamrishwa kuolewa tu na wanaume kutoka katika ukoo wao wa Manase (Hesabu 27:1-11; 36:1-13). "Tumeona ya kwamba ni kosa Mkristo kuoana na mtu aliyekuwa Mkristo kwa sababu kufanya hivyo ni kukiuka kanuni inayokataza Wakristo kufungwa nira moja na makafiri. Lakini, tutasema nini kuhusu mtoto wa Mungu kuoana na mtoto mwengine wa Mungu ambapo wana mawazo tofauti kuhusu mafunzo ya Mungu? ambapo mmoja wao anahusika na kikundi ambacho kinapinga msimamo wa kikundi cha mwenzake? Ndoa kama hiyo haiwezi kuitwa nira isiyokuwa sawasawa kwa maana ya mtu Mkristo na asiyekuwa Mkristo kwani wote wawili wameokolewa kwa damu ya thamani ya Kristo.… Bali utakuwa ni muungano wenye hatari kwa waliooana na hata kizazi chao" (Paul Wilson, *The Institution of Marriage,* Bible Truth Publishers, Addison, IL 60101).

Ndoa ni jambo gumu sana, yaani, jambo linalohitaji kuungana kwa watu wawili tofauti, wenye fikira tofauti, jamii tofauti, viwango tofauti vya elimu na kujifunza kuishi pamoja kwa miaka kama hamsini hivi—hata bila ya kuzidishiwa ugumu kwa kuwa na mume au mke mwenye mawazo tofauti ya kidini. Kama tutakavyoona katika maelezo zaidi katika sura ijayo, msingi wa ndoa thabiti yenye furaha ni uhusiano imara wa kiroho; na uhusiano huu hudhoofika iwapo mke na mume hawana mawazo sawa kuhusu haja ya kushirikiana na Wakristo wengine.

Matatizo mengine hutokea iwapo mna watoto katika jamii inayohusika. Mara kwa mara, mume atapenda watoto kuandamana naye na pia hali kadhalika mkewe atataka watoto waandamane naye kwenda katika ushirika fulani. Hali hii huleta migogoro katika ndoa na na watoto huchanganyikiwa kimawazo. Kujaribu kusuluhisha tatizo hili kwa kufanya mapatano hakuleti suluhisho la furaha na la kudumu. Hatua kama hii huishia mume au mke kuacha kikundi chake na kuandamana na mwenzake kama hatua ya kupunguza kutoelewana na kuleta amani kuliko kuwa na imani moyoni kwamba kwa kubadili kikundi chake cha dini, mtu anatenda mapenzi ya Mungu. Tabia hii inaweza kuleta kujisikia mwenye dhambi mbele ya Mungu na kuharibika kwa maisha ya kiroho ya mtu anayehusika. Ni bora kuepuka hali kama hii kwanza kwa kutojiingiza katika uhusiano kama huo. Ni dhahiri kuwa matatizo kama haya huzidi sana iwapo Mkristo ataoana na asiyekuwa Mkristo.

## Kulielewa Chaguo Halisi la Mungu

Katika sehemu iliyotangulia, miongozo kadhaa ya kibiblia kuhusu uchaguaji wa mchumba wa ndoa ilitolewa. Mkristo anapaswa kumtafuta mchumba ambaye pia ni Mkristo aliyeokoka kikweli, ampendaye Mungu na kutaka kuishi ndani yake na ambaye ni mfuasi wa kikundi cha dini kilicho sawa na chake. Katika sehemu hii, tunajadili jinsi ya kuelewa mtu ambaye Mungu ametuchagulia kuoana naye.

Kama tulivyoona hapo juu, Ibrahimu alimwagiza mtumishi wake asimchagulie Isaka mke kutoka kwa Wakanaani bali kutokana na ukoo wa Ibrahimu (Mwanzo 24). Huu ni mwongozo wa kijumla. Lakini mtumishi alipofika katika mji wa Nahori, utafutaji wake wa mchumba halisi ulianza wazi wazi. Alipokuwa amesimama karibu na kisima cha umma, alimwomba Mungu ili kwamba yule msichana ambaye Mungu alikuwa amemchagulia Isaka kuwa mkewe apate kutokea pale kisimani jioni ile na kwa ishara fulani maalumu apate kumtambua atakapofika. Mungu aliyajibu maombi yake na akakutana na Rebeka ambaye alitokea kuwa mpwa mjukuu wa Ibrahimu. Kwa sababu hiyo, mtumishi alisujudu na kumwabudu Mungu akisema, "Libarikiwe jina la Mungu wa Bwana wangu Ibrahimu ambaye hakumpunguzia Bwana wangu neema na haki; nilipokuwa njiani, Mungu aliniongoza hadi kwa jamaa wa Bwana wangu" (kifungu 27).

Mfano mzuri sana kwetu leo! Kadiri vijana Wakristo wanavyozidi kufanya urafiki na kufikiria kuoana siku moja, wanapaswa kumwomba Mungu ili awaelekeze kwa mchumba aliyewachagulia kuoana naye. Wazazi wa vijana hawa wapaswa kuomba pia na kuwahimiza watoto wao kuomba vivyo hivyo.

Hatuwezi kueleza ni njia ipi ambayo Mungu ataitumia kumfunulia kila mtu mchumba ambaye amemchagulia kwa ndoa. Ni vizuri kutazamia lolote kutokea hadi hapo mapenzi ya Mungu yatakapodhihirika. Haifai kufanya uamzi wetu binafsi na kumwambia Mungu atuzuie iwapo uchaguzi wetu sio mapenzi yake. Mara nyingine anaweza kufanya hivyo lakini si jambo la kutegemewa. Mungu, mara nyingine katika hekima yake, hutuacha kutenda tunayoyataka iwapo tumekata shauri kuyafanya.

Iwapo tunatafuta kikweli mapenzi ya Mungu kuhusu ndoa, tunaweza kuona Mungu akitufungia na kutufungulia milango—mara nyingine kwa njia isiyotazamiwa—katika njia ya kutuelekeza kwa mchumba aliyetuchagulia kwa ndoa. Mara nyingine, anaweza kutumia

tabia zetu katika kutimiza jambo hili. Kwa mfano, mara nyingi urafiki kati ya vijana huvunjika kwa sababu mmoja wao huwa na pupa ya kutaka kufanya uhusiano wa karibu kwa haraka au pengine mmoja wao huwa hana mapenzi ya kufanya uchumba imara. Kama matokeo ya jambo hili, yule aliyekuwa na "hatia" huanza kujuta kimoyo kwa kosa alilolifanya la kuwa na haraka, kutokuwa na mapenzi au mambo mengine kama hayo. Lakini, tukumbuke kwamba ingawa tunapaswa kujifunza kutokana na makosa yetu, inawezekana kuwa Mungu anatumia tabia zetu ili kutuelekeza kwa mchumba aliyetuchagulia.

Kiasi Mungu anavyotufungia milango, pia ndivyo anavyotufungulia milango mingine. Kwa wale wasomaji ambao pengine hawajui wafanyeje kuhusu uchaguaji wa mchumba wa ndoa ingawa wamejaribu kufuata miongozo iliyoelezwa hapo awali, hawapaswi kukata tamaa kwa sababu Mungu hufungua milango na ana uwezo wa ku-kuelekeza kwa mcumba akufaaye. Hatahivyo usifikirie kuwa atakukabidhi mke au mume kwa urahisi huku ukiwa raha mstarehe katika chumba chako. (Kumbuka juhudi alizofanya mtumishi wa Ibrahimu kumtafutia Isaka mke.)

Mungu anakutazamia kutoka nje kufanya urafiki na marika zako pamoja na washirika wengine walio karibu nawe. Na iwapo hapana watu wengi katika ushirika ulio karibu nawe, unapaswa kwenda katika ushirika wa mikoani au wa kitaifa na kufanya urafiki na washiri ki waliomo. Na jambo hili halimaanishi kwamba utapata mke au mme; Mungu anaweza kuwa amekuandalia mipango mingine (kama itakapoelezwa hivi punde), ama Mungu anaweza kuwa na mambo kadhaa ambayo angependa wewe ujifunze kabla ya kukuu-nganisha na mchumba wako.

## Chaguo la Kutooa au Kutoolewa

Kufikia hapa tumekuwa tukijadili shauri la kujua mapenzi ya Mungu kuhusu chaguo la mchumba wa ndoa. Lakini bado hatujajadili swali kwamba, "Je, ni mapenzi yake Mungu kuwa lazima nifunge ndoa?" Mkristo kukaa bila kuoa au kuolewa ni chaguo ambalo limeelezwa katika Neno lake Mungu. Mtume Paulo anaeleza, "Ningetamani sana watu wote kuwa kama mimi [yaani kapela]…. Nawaambia watu ambao hawajafunga ndoa pamoja na wajane, kuwa ni bora wao kuishi kama mimi" (1 Wakorintho 7:7,8). Katika aina fulani za huduma kwa ajili ya Mungu kuna faida kadhaa za kukaa bila kufunga ndoa ambapo pia aina nyingine za utumishi wa kikristo huwa rahisi zaidi iwapo mtu ameoa au kuolewa. Mtume Paulo ni mfano mzuri wa mtumishi wa aina

ya kwanza; angetimizaje yote aliyoyafanya kama angekuwa na jukumu la kifamilia? Wale waliobarikiwa kutofunga ndoa (1 Wakorintho 7:7) wako huru, mtume anatueleza, kumhudumia Mungu bila pingamizi (1 Wakorintho 7:35). Kwa hivyo Wakristo waliofunga ndoa wasiwafanye wale walio kapela kujisikia kuwa wana kasoro fulani za kijamii kwa sababu ya kutofunga ndoa wala wasione kuwa ni lazima kuwatafutia wenzao wachumba wa kufunga ndoa nao.

Kuna wito katika 1 Wakorintho 7 sio tu kwa wale ambao hawajafunga ndoa, bali pia kwa wajane na waliotalikiwa. Tutajadili katika sura itakayofuata baadaye mafunzo ya Biblia kuhusu talaka na kuoana tena lakini inafaa kutaja hapa kuwa hata katika hali ambapo kuoana tena kunaruhusiwa na Neno la Mungu, chaguo la kutooa linafaa kufikiriwa kwa makini kulingana na mapenzi ya Mungu (1 Wakorintho 7: 8, 27, 32-34, 38-40). Mtu aliyefiwa na mume au mke anapaswa kuomba na kufikiri kwa uangalifu ili kujifunza jambo ambalo Mungu anataka kumfundisha kupitia kwenye msiba huo wa kufiwa na kufahamu kama Mungu anayo kazi ambayo angependa mfiwa kuifanya akiwa katika hali hiyo ya ujane. Wajane walioteuliwa kupatiwa msaada na waumini ni wale ambao walikuwa na mume mmoja tu lakini ambao walijitowa katika maombi na ibada, kutenda wema kama kulea watoto, kuwapa wageni malazi, kusafisha miguu ya mitume na kuwasaidia wenye dhiki (1 Timotheo 5:3-10). Maaskofu (au wasimamizi) na viongozi wa makanisa pia walihitajika kuwa "mume kuwa na mke mmoja" (1 Timotheo 3:2,12). Kisarufi, kifungu hiki kinalingana na kile kingine katika 1 Timotheo 5:9—"mke wa mume mmoja," hivi ni kusema kuwa ili kuchaguliwa katika vyeo hivi, mwanamume alihitajika kubaki mjane iwapo alikuwa amefiwa. Kauli hii ilimweka Mungu na mahitaji ya kanisa mbele na pengine ilichukulia hali ya ujane kuwa na uhuru zaidi wa kumtumikia Mungu na kuwasaidia waumini wengine (1 Wakorintho 7:32-33). Kwa upande mwingine Mtume anaeleza wazi wazi kuwa sio dhambi wala aibu kwa mjane kufanya ndoa tena (1 Wakorintho 7:9,28,36,39).

Kwa muhtasari, Mungu anajishughulisha sana na swala la kuhusu iwapo tunapaswa kuoa, na kama tutaoa, tutafunga ndoa na nani. Wote wanaofikiria kufanya ndoa na waombe bila kuchoka na kwa moyo wote ili wajue mapenzi ya Mungu kuhusu maswala haya.

# 2

# *Kujitayarisha Kwa Ndoa*

Kuna majadiliano mengi leo kuhusu tatizo la watu wanooana "kuwa na tabia zisizochukuana." Sehemu kubwa ya ndoa huishia katika talaka leo kwa sababu ya kukosekana kwa upatano katika uhusiano wa ndoa. Kwa hivyo, kadiri urafiki kati ya msichana na mvulana unavyopita kutoka kiwango cha urafiki wa kawaida na kuwa uchumba wa kudumu na kuweza kufikiria kufunga ndoa, swala la upatanifu wa kitabia huwa muhimu.

## Kujenga Upatanifu wa Kiroho

Katika nchi hii kuna wazo kwamba watu wana-otazamia kuoana wanapaswa kulala kitanda kimoja au kuishi katika nyumba moja kusudi waweze kufahamu iwapo wanapatana kimwili. Tatizo kubwa kuhusu tabia hii—na takwimu juu ya talaka zinathibitisha jambo hili—ni kwamba kuwapo kwa upatanifu wa kimwili kabla ya ndoa si hakikisho kuwa uhusiano huu wa kimwili uaendelea kuleta furaha baada ya fungate ya harusi. Ndoa nzuri, iliyo imara na ya kudumu ni ile iliyojengwa sio kwenye uhusiano wa kimwili bali ule wa kiroho. Kufurahia upatanifu wa kimwili kwa watu waliooana kutategemea sana nguvu za uhusiano wao wa kiroho.

Jambo hili linaeleza nini kwa wale wanaotazamia kufunga ndoa hasa kabla ya kuchumbiana kindoa na baada ya kuwaposana ili waoane? Bila shaka ni bora kueleza mambo ambayo watu kama hao wanaweza kufanya pamoja. Katika wakati wa urafiki wa kawaida wanaweza kutambua mambo ambayo yanampendeza kila mmoja, yanayomchukiza kila mmoja, mawazo kuhusu Mungu, Kristo, Kanisa na iwapo kila mmoja ni Mkristo aliyeokoka kikweli. Kama wote wawili wameokoka, wameanza kuelewa ni sehemu gani ambayo Mungu anaichukua katika maisha yao. Kiasi uhusiano unavyozidi kukua, haja ya kuhakikisha uzito wa mapenzi yao na kujitolea kwao kwa Kristo kama Bwana wa maisha yao inakuwa muhimu.

Kwa hivyo, kipindi hiki cha posa kinapaswa kutumika kwa wachumba kutumia wakati wao mwingi pamoja wakisoma Biblia na miongozo ya Biblia kwa mfano ule ulioandikwa mahsusi kwa wachumba kama vile J. Allan Petersen, *Before You Marry*, Tyndale House Publishers Inc., Wheaton, Illinois. Wanapaswa kutumia wakati

wao kuchunguza msimamo wa kila mmoja kwa mjibu wa mafunzo ya Neno la Mungu. Iwapo wanatofautiana sana kuhusu mafunzo kadhaa—kama vile mmoja kuamini ubatizo wa kanisani na mwengine kuzingatia ubatizo wa kinyumbani, au mmoja kuamini kanisa "litaolewa" kabla ya kuja kwa mateso makuu ya mwisho wa dunia na mwengine kuamini kanisa "litaolewa" tu baada yakipindi cha utawala wa Kristo hapa duniani wa miaka elfu moja—wanapaswa kutafuta jinsi wanavyojisikia kuhusu tofauti kama hizi ama jinsi watakavyozisuluhisha ama kuzivumilia katika maisha yao baada ya ndoa. Iwapo mmojawao anaona haja kubwa ya "kumgeuza" mwenzake, jambo hilo linaweza kuwa ishara ya shida itakayotokea hapo baadaye.

Pamoja na kutafuta msimamo wa kila mmoja kuhusu mafunzo ya Biblia, ni vizuri kujadiliana jinsi Mafunzo hayo yatakavyotawala maisha yao hasa uhusiano baina yao kama mume na mke na kati yao kama wazazi na watoto wao. Kwa mfano, panaweza kutokea tatizo katika kulea watoto iwapo mmoja wao anapendelea kuwachapa kama njia ya kuwapasha nidhamu na hali mwenzake haipendi njia hii.

Katika kipindi cha kabla ya posa ambapo uwezekano wa kufanya ndoa unafikiriwa, na pia wakati wote wa posa ambapo mipango ya sherehe ya ndoa na maisha katika ndoa inafanywa, panapaswa kuwa na mapenzi ya wachumba wote wawili kuomba pamoja sio tu kwa baraka za Mungu katika mipango yao yote bali pia ili Mungu aweze kuwafafanulia mapenzi yake kuhusu ndoa yao waliyoinuia. Inapaswa kukumbukwa kuwa ingawaje posa ya ndoa ni ahadi imara anayoitoa mume kwa mke kama nia yao ya kuoana na haipaswi kutolewa au kuvunjwa ovyo ovyo, ni heri kuivunja posa kama ndiyo mapenzi ya Mungu kuliko kujiingiza katika uhusiao wa maisha ambao haujaidhinishwa na Mungu. Pia ni bora kuwa na wakati mrefu wa kuposana kabla ya ndoa ili kuweza kugundua baadhi ya matatizo na pia kuelewa kikamilifu mapenzi ya Mungu kuhusu ndoa yenyewe.

## Uhusiano wa Kimwili Kabla ya Ndoa

Kabla ya kuimaliza sura hii juu ya kipindi cha kabla ya kuoana, hebu tulirudie swala la uhusiano wa kimwili. Watu wengine wanaweza kusema, "Ni vizuri kujenga uhusiano wa kiroho, lakini pana kosa gani pia kujaribu uhusiano wa kimwili?" Wengine wanaweza kuongezea, "Kuna tatizo gani hata hivyo na hali tunakusudia kuoana?"

Hebu tuangalie kwanza Biblia inatufunza nini juu ya kujuana kimwili kabla ya ndoa. Kama msomaji unavyofahamu, pana mafunzo mengi yanayokataza uasherati, yaani kujuana kimwili nje ya ndoa

(angalia, kwa mfano, Matendo 15:20; 1 Wakorintho 6:13-20; 1 Wakorintho 10:8; Waefeso 5:3; Wakolosai 3:5; 1 Wathesolonike 4:3). Zaidi ya hapo, katika Torati 22:13-21, tunaona wasichana walitegemewa kuolewa wakiwa bikira. Na katika ushahidi wa Agano Jipya, Mariamu hangechaguliwa kuwa mamake Mesia kama mawazo yake yangekuwa sawa na yale ya ulimwengu wa leo—na ambayo yanawaathiri Wakristo wengi sana pia—kwamba iwapo wachumba wawili wanapendana, kiwango chochote cha maingiliano ya kimwili kati yao kama kielelezo cha mapenzi yao kinakubalika. Mungu alitukuza uadilifu wa Mariamu na atawatukuza vijana wote ambao watabakia mabikira hadi kuoana kwa kuwasaidia wawe na furaha ya kweli katika ndoa.

Kwa ushahidi zaidi dhidi ya maingiliano ya kimwili kabla ya ndoa, fikiria maneno ya mtume Paulo kwa Kanisa la Wakorintho: "Nimewahimiza kuwa na mume mmoja ili niweze kuwaonyesha kama bikira wasafi kwa Kristo" (2 Wakorintho 11:2) . Ndoa ni aina ya muungano kati ya Kristo na Kanisa lake (Waefeso 5). "Kipindi cha Kanisa" ni kile cha kuposwa kwa Kanisa; sherehe ya ndoa haitafanyika hadi kurudi kwake Kristo na kulitwaa kanisa "kama bikira" wake (1 Wathesolonike 4:13-18; Ufunuo 19:7). Kama vile Kanisa litakavyotolewa kama bikira msafi kwa Kristo, mposi wetu, vivyo hivyo ni jambo zuri na la kumpendeza Mungu wakati wachumba Wakristo wanapooana wakiwa mabikira.

Kujuana kimwili mapema kunafupisha wakati wa kujenga uhusiano wa kweli wa kiroho. Jambo hili linaweza kutokea kwa njia kadhaa kama alivyoeleza mtu mwengine: "Kwanza, ile siri ya kujuana kimwili ina mvuto wa kihisia na inawafanya wachumba kusahau mambo ya kiroho. Pili, kwa vile uhusiano wao ni siri kati yao ambayo wanaojaribu kuificha, hali hii inaweza kuwafanya kuwa na utiifu na undani kati yao. wawili. Wanaweza kukosea kwa kufikiri kwamba mvuto wa kimapemzi kati yao ni muungano wa kiroho lakini mvuto huu utakwisha mara tu ndoa itakapowafanya wawe na 'heshima' na kuondoa ile haja ya kuwa na siri kati yao. Hawatakuwa na siri wala jambo lolote la maana ambalo watashirikiana. Tatu, kwa vile hawampendezi Mungu hawawezi kuwa karibu naye huku wakiwa hawajumuiki naye. Nne, mawazo ya kujisikia wamefanya makosa yatazuia kuimarika kwa undani kati yao baada ya ndoa. Mungu atawabariki wale wanaotumia wakati wa kuposana kujenga uhusiano wa kiroho na kihisia na kubakisha uhusiano wa kimwili kwa maisha ya ndoa. Hawatakuwa tu na uhusiano thabiti wa kiroho bali pia watafurahia uhusiano mwema wa kimwili" (Martha K. Canner, *Vijana*

*wa Biblia*, Moments with the Book, Bedford, PA 15522 USA).

Sababu nyingine ya kukataza uhusiano wa kimwili wa mapema kati ya wachumba ni hii: Iwapo uhusiano huu utasababisha kushika mimba kabla ya ndoa, wachumba watazidi kwenda nje kimawazo kutoka katika msingi wa kujenga uhusiano imara wa kiroho pamoja na kuhakikisha kwamba ni mapenzi ya Mungu wao kuoana. Mara nyingi, mipango ya haraka hufanywa kufunga ndoa ili kupunguza aibu na haya katika hali kama hiyo.

Mwisho, hebu tufikirie maoni yaliyotolewa na mwalimu mmoja mtaalamu wa mafunzo ya Kikristo: "Katika Neno lake, Mungu amefafanua kauli kwamba uhusiano wa kimwili unapaswa kuwepo tu kati ya watu waliooana…. Mungu ametuumba na maumbile amabayo yanatufanya tuhisi uhusiano wa kimwili nje ya ndoa si mzuri kama vile ule wa ndani ya ndoa.

"Madhara makuu hutokea pale ambapo sheria za Mungu zinakiukwa. Hebu nitoe mfano kudhihirisha jambo hili.

"Wakati wangu mwingi wa mashauriano hutumika kuwashauri wachumba wanaotarajia kuoana. Wakati wa vipindi vitatu vya mashauriano kabla ya ndoa, huchunguza kwa undani uhusiano kati yao. Tunajadili kuhusu maisha yao kwa mitazamo tofauti: kiroho, kihisia, kipesa, kijamii na kimwili. Si vigumu kuona baadhi ya wachumba nitakaowaoza wakiwa tayari wamejuana kimwili. Kama hili limetokea, ninaamuru jambo hili likome. Kabla ya kuendelea ninapata ahadi ya kila mmoja wao kwamba kutokea siku hiyo na hadi watakapooana, watajaribu kuwa na nidhamu na kujizuia katika uhusiano wao.

"Hii ndiyo sababu. Iwapo maingiliano ya kimwili hayatakoma kabisa kabla ya ndoa, baada ya ndoa uhusiano wa waliooana utabadilika kabisa mke mchanga ataolewa huku akijawa na chuki kwa madhambi aliyotendewa na mchumba wake. Punde hugeuka na kuwa mtundu na hutwaa jukumu la uongozi kutoka kwa mumewe kwa ajili ya chuki na gadhabu. Na mwanmume? Yeye hujisikia hana furaha na ametenda dhambi na mwishowe hugeuka mnyamavu. Mke hutwaa uongozi huku akiwa anaji chukia mwenyewe na hali mumewe hujitenga (na kuwa mwenye dhiki). Haya yote ni kwa sababu uhusiano wao wa kimwili ulianza kimakosa kabla ya ndoa.

"Miongoni mwa mamia ya wachumba niliowa-shauri amabao waliungama kuwa na uhusiano wa kimwili, siwezi kukumbuka mmoja kati yao ambaye maisha yake aliyeepuka utaratibu huu. Mwanasaikolojia wa Kikristo ambaye ni rafiki yangu aliniambia kuwa

tatizo la kwanza ambalo hulishughulikia katika kazi yake nyingi kama mshauri ni lile la mume aliye mnyamavu.

"Wanaume wengi hivi leo wanaona vigumu (au jambo lisilowezekana) kuchukua nafasi ya uongozi katika nyumba zao. Nastaajabu iwapo tabia hii imesababishwa na maovu na uhusiano wa dhambi wakati wa kipindi cha posa…na kama sasa wanaadhibika kama matokeo ya makosa yao" (kutoka katika kitabu kiitwacho, *Strike the Original Match* cha Charles R. Swindoll, 1980, kilichochapishwa na Multnomah Press, Portland, OR 97266 USA; matumizi yameidhinishwa).

Mambo mengine zaidi ambayo wanaotegemea kuoana wanapaswa kuyafikiria yametolewa katika Nyongeza 1, kwa mameno "Kabla Hujafunga Ndoa."

## 3

# *Mambo Muhimu Kwa Furaha Katika Ndoa*

Baadhi ya mambo muhimu yanayoleta furaha ya kudumu katika ndoa yamejadiliwa katika sehemu zilizotangulia. Mambo haya ni pamoja na uchaguaji ufaao wa mchumba na tabia nzuri wakati wa kabla ya ndoa. Iwapo mume na mke ni Wakristo waliojitolea na waliookoka, na iwapo wamejenga uhusiano imara wakati wa kabla na baada ya posa, ndoa yao itaanza kwa msingi imara. Hata hivyo kudumisha furaha katika ndoa kunahitaji kujirekebisha kwa kila mmoja wao na juhudi kubwa ya kujisahihisha katika maisha yao yote.

Matokeo ya utafiti mmoja yalichapishwa katika gazeti moja hivi karibuni. Ulikuwa utafiti uliohusu jamii 35 za watu waliotimiza miaka 50 ya ndoa. Mke na mume walihojiwa mbalimbali wakiaahidiwa kuwa majibu yao hayataelezwa wenzao. Ajabu kubwa kwa wachunguzi ni kuwa waligundua kwamba wengi wa waliooana—asilimia 60%—hawakuwa na furaha katika ndoa zao. Kuishi kwao pamoja kwa miaka 50 hakukumaanisha kuwa walikuwa na furaha bali hasa kulionyesha namna ya wakati walimoishi. Hawakuamini katika kupeana talaka; na talaka haikuwa suluhisho lao ama wenzao walioishi katika wakati ule.

Lengo mojawapo la kitabu hiki ni kusisitiza msimamo wa

Neno la Mungu—ambao pia ndio msimamo wa jamii ya kikale ya Wamarikani—kwamba talaka si suluhisho na inachukiwa na Mungu (Malaki 2:16). (Hoja hii kuhusu talaka itajadiliwa katika sehemu itakayofuata baadaye.) Lakini katika kusisitiza kauli kwamba ndoa ni kitu cha kudumu, na kuwa walioana wanapaswa kustahimili kwa vyovyote, pia si kusudi langu kuwafunga waliooana katika dhiki ya milele. Ndoa haipaswi tu kuwa uhusiano wa milele (yaani, "hadi kifo kitakapotutenganisha"); bali naamini kuwa ni mapenzi ya Mungu kwamba ndoa iwe ni chanzo cha furaha ya kudumu kwa watu waliooana. Na jambo hili huwezekana iwapo watu hao ni Wakristo. Jinsi watu hao wanavyozidi kuvutwa karibu na Kristo, Kristo akiwa mioyoni mwao katika imani, wakiwa na msingi imara wa mapenzi (Waefeso 3:17), watahisi furaha katika Bwana na pia mapenzi na furaha kwao binafsi.

Mambo mengi yanahitajika ili pawepo na furaha katika ndoa; ni machache tu kati ya haya yatakayotajwa katika kitabu hiki. Mapendekezo kadhaa kuhusu maandishi yanayoweza kurejelewa yametolewa katika mwisho wa sehemu hii.

## Kujinyenyekeza na Mapenzi

Mambo mawili muhimu katika furaha katika ndoa—kujinyenyekeza na mapenzi—yameelezwa katika Waefeso 5: "Wake jinyenyekezeni kwa waume zenu kama kwa Mungu. Kwani mume ndiye kichwa cha mke; kama Kristo alivyo kichwa cha Kanisa; na pia ndiye mkombozi wa mwili. Kwa hivyo kama vile kanisa lilivyo chini ya Kristo, na wake wawe hivyo kwa waume zao katika kila jambo. Waume wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda Kanisa na kujitolea nafsi yake kwa ajili ya Kanisa…. Kwa hivyo ianawapasa waume kuwapenda wake zao kama wanavyoipenda nafsi zao wenyewe. Yule anayempenda mke wake anajipenda mwenyewe. Kwani hapana mtu auchukiaye mwili wake bali bali huulisha na kuutunza kama vile Kristo alifanyavyo Kanisa" (Waefeso 5:22-29).

Kwanza, mke anahitajiwa kujinyenyekeza kwa mumewe kama Kanisa lilivyo chini ya Kristo. Hii inamaanisha nini? Hebu tukumbuke kwanza kwamba yule ambaye Kanisa liko chini yake ni mwenye ujuzi wote, hekima yote, utakatifu, wema, na mapenzi. Sheria zake, matendo na maamuzi yake sio yenye kuadhibu bali yanaleta baraka kwa Kanisa. Kwa hivyo, ni kwa manufaa ya Kanisa kwamba kanisa liweze kusikia yote anayoagiza Kristo na kuyatekeleza kila moja bila kuyakanusha. Mke pia anahitajika kuwa mnyenyekevu kwa mmewe.

Lakini tatizo hapa ni kuwa mme si mwenye ujuzi wala hekima yote; kinyume na kuwa mwema na mwenye mapenzi anaweza kuwa na tabia ya kujipenda. Je, mke anatarajiwa kuachilia mbali mawazo, ujuzi na hekima yake na kujinyenyekeza kimyakimya huku akimwachia mmewe maamuzi yote makubwa na madogo? Katika Mwanzo 2:18 tunasoma kwamba, "Mungu alisema, si vyema kwa mwanamme kuwa peke yake; nitamfanyia msaidizi amfaaye." Kwa hivyo, kwa vile mume si mwenye ujuzi wote, hekima yote na pia kwa vile anajipenda kibinafsi, anapaswa kudhamini msaada wa mke wake katika kufanya maamuzi. Iwapo mke atahisi kuwa uamuzi ambao mumewe amefanya au anakaribia kufanya ni kinyume cha mapenzi ya Mungu, au utailetea familia madhara fulani, au kuwadhuru watu wengine, au sio wa busara, anapaswa kuwa huru—kama msaidizi wa mumewe—kumweleza kwa mapenzi kutoridhika kwake na mapendekezo kwa uamuzi bora zaidi. Mawasiliano kama haya ni kwa manufaa ya wote na yanapaswa kuhimizwa na mume.

Katika mashauri ambayo ujuzi wa mke unazidi ule wa mume, mume anastahili kuwa tayari kumwachia mke jukumu la kufanya maamuzi. Lakini, sharti mume akumbuke kwamba Mungu amemkabidhi mamlaka ya juu zaidi na wajibu wa kuisimamia jamii yake; kwa sababu hii, lazima awe tayari kuchukua lawama ya maamuzi mabaya atakayofanya mkewe.

Kwa upande wa mume, hapapaswi kuwa na tabia ya "kumsimamia" mkewe eti kwa vile mke yu chini ya mume. Mke si mtumwa wa kumtumikia mume wala si chombo ambacho mume anaweza kukitumia jinsi apendavyo. Amri iliyotolewa kwa waume ni "wapendeni wake zenu." Mapenzi haya ni yenye undani na ni mapana kuliko mapenzi ya kimwili. Waume wanaamrishwa kuwapenda wake zao "kama Kristo alivyolipenda kanisa na kujitolea kwa ajili ya Kanisa." Haya ni mapenzi ya ki-Mungu ambayo yanajitolea daima kuhakikisha manufaa ya wengine hata kama kitendo hiki kitamgharimu anayejitolea gharama fulani. Kwa hivyo, maamuzi yote atakayofanya mume huku akijawa na mapenzi kwa mke wake na familia yake, yatakuwa yenye kumpendeza mkewe; kwa njia hii, mume atataka kutafuta maoni ya mkewe katika kufanya uamuzi.

Pamoja na haya yote, bado panaweza kutokea baadhi ya mashauri ambayo mume na mke wataendelea kutosikilizana, hata baada ya kujadiliana kwa uvumilivu maoni ya kila mmoja na hata kuomba pamoja juu ya mambo yenyewe. Katika hali kama hii, lazima ifahamike kwamba Mungu amekabidhi mamlaka ya mwisho kwa

mume na mke ni sharti kutii uamuzi wa mume. Iwapo ni uamuzi ambao mke anaonelea kuwa unaweza kuleta matokeo mabaya kwa jamii (kwa mfano kununua kitu cha anasa ambacho bei yake inazidi uwezo wa kifedha wa jamii), mke anaweza kuomba Mungu ili Mungu azuie au kusimisha ule uamuzi au kitendo; anapaswa pia kuomba kupewa uvumilivu na kutafuta msaada wa Mungu kufanya awezalo ili kupunguza matokeo mabaya ya uamuzi kwa familia.

Iwapo wasomaji wengine ambao ni wanawake watachukia jambo hili kuwa Mungu amemkabidhi mwanaume mamlaka ya mwisho ya kuisimamia jamii, tafadhali na wafahamu kuwa katika kiwango chochote cha jamii, lazima pawepo na utaratibu wa usimamizi, uwezo wa juu zaidi. Kama sivyo, pangetokea mvurugano mkubwa. Kwa hivyo, Mungu amewafanya wazazi kuwa juu ya watoto wao; waalimu kuwa juu ya wanafunzi; waajiri kuwa juu ya wafanya kazi wao; mameya, magavana na maraisi juu ya raia katika viwango tofauti chini ya mfumo wa kisiasa. Watawala wote ni watumishi wa Mungu ili kuleta wema (Warumi 13:1-4). Hii ndiyo sababu kubwa kuwa mume Mkristo afaa kuwa mtumishi wa Mungu kwa ajili ya baraka ya mke na watoto wake. Mume Mkristo ana wajibu mkubwa ambao kuutimiza vizuri kunahitaji maombi mengi na kumnyenyekea Mungu. Kwa hakika, amri hii imetolewa kwa ajili ya kuitumikia familia yake, kama alivyosema Kristo, "Aongozaye na awe kama mtumishi" (Luka 22:26 JND).

Kwa ufupi, wakati mume na mke wanapojifunza kufanya kazi pamoja, kuelezana hisia na matakwa yao kwa njia ya kirafiki na mapenzi, kufanya uamuzi kwa kufikiria manufaa yao wawili na familia, kufuata agizo la wake kuwanyenyekea waume zao iwapo hawawezi kufikia uamuzi, patakuwepo na msingi wa ndoa yenye furaha.

## Kuomba na Kusoma Pamoja

Ni muhimu kwa mume na mke kutenga wakati maalumu kila siku bali na "wakati wa kutafakari" wa kila mmoja au ibada ili kusoma Biblia na maelezo kuhusu masomo ya Biblia pamoja na kuomba pamoja. Iwapo wakati uliopo unatosha tu kwa kufanya jambo moja tu kati ya haya, mambo yenyewe yanaweza kufanywa katika nyakati mbalimbali—kusoma pamoja siku moja na kuomba pamoja siku ya pili. Iwapo hapana wasaa wa kufanya maombi na kusoma kwa mtu binafsi, shughuli hizi pia zinaweza kufanywa katika nyakati tofauti. Maombi ya pamoja hayamaanishi mume aombe na hali mke anasikiliza bali wote wawili washirikiane katika kuomba. Katika kuomba pamoja tunapata mwamko wa kuyafikiria mambo yanayowahusu wenzetu.

Kwa mfano, jambo muhimu la kuombea pamoja ni kuhusu uleaji wa watoto wetu ili kuwakuza kwa ajili ya Mungu (angalia Mathayo 18:19 kuhusu umuhumu wa kuomba pamoja). Pia mfano mwingine wa maombi ya pamoja iwapo mume na mke wanashirikiana kuombea rafiki zao waokoke au waendelee kukua kiroho, mume atakuwa tayari kumuunga mkewe mkono katika shughuli kama vile kuwaalika watu hao nyumbani kwa chakula cha jioni ili kupata nafasi ya kushirikiana nao katika kujadili mambo ya kiroho.

## Mawasiliano

Mtu mwengine ameandika yafuatayo kwa wale wanaotarajia kufunga ndoa: "Kwa vile ufanisi katika ndoa unategemea mawasiliano ya kila mara, walioposana wanapaswa kuzungumza, kuzungumza, kuzungumza" (angalia Nyongeza 1). Mawasiliano haya ni muhimu sana katika maisha yote ya ndoa. katika Neno la Mungu tunasoma, "Furahini na wenye kufurahi na kuomboleza na wenye kuomboleza" (Warumi 12:15). Lakini, ili kutekeleza jambo hili lazima pawepo na mawasiliano ya mtu na mtu kuhusu furaha zetu, fanaka, na pia dhiki zetu, hofu na kutofaulu kwetu.

Mara nyingi huwa ni vigumu kwa mume kushirikiana na mkewe fikira zake juu ya dhiki zake, hofu ama kutofaulu. Mume hupendelea kujihisi kuwa yu huru na mwenye uwezo wa kuyasuluhisha matatizo yake binafsi. Lakini mke anayejali anaweza kuwa ni msaada mkubwa sana kwa mumewe katika hali kama hii (hii ni njia mojawapo ya mke kuwa "msaidizi," Mwanzo 2:18 JND). Kwa pamoja wanaweza kuomba na kuutafuta msaada wake Mungu kuhusu tatizo lenyewe. Na ushirika wa aina hii utawavuta pamoja kihisia na kiroho wote wawili—mume na mke. Mawasiliano halisi katika ndoa ni kuelezana hisia za kindani kwa mtu na mwenziwe. Ili jambo hili lifaulu, sharti pawepo na mapenzi kwa wote wawili, kuaminiana, uvumilivu, msamaha na uelewano.

Jambo liwafaalo waume na kina baba vijana kulifikiria ni kuwa wanapokuwa kazini kutwa nzima wakishirikiana na watu wazima wenzao, wake zao wanaweza kuwa wanashinda tu na watoto wadogo. Kwa hivyo mume— ingawa huwa amechoka kweli—lazima ajaribu kutimiza haja ya mkewe ya kuzungumza na mtu mzima, badala ya kujifikiria tu nafsi yake na kutaka kujipumzisha katika kiti chake cha starehe huku ameshika gazeti au anaangalia televisheni afikapo nyumbani kutoka kazini.

Hali nyingine iletayo matatizo ni hali ya kuwa mume na mke hutambua mambo kadhaa katika tabia ya mwenzake ambayo

hayapendi. Kama ilivyoelezwa katika sehemu iliyotangulia, ndoa inalazimisha watu wawili walio tofauti sana katika mambo wayapendayo, wayachukiayo na aina za marafiki na jamaa zao, n.k. Tuchukuwe mfano wa ambao hutolewa mara kwa mara wa jinsi mtu anavyobonyeza kifuko cha dawa ya kusafishia meno, inaweza kuleta ugomvi katika ndoa. Ama inaweza kuwa matumizi ya maneno fulani, hadithi na mzaha na tabia nyinginezo kama hizi ambazo zinaweza kumkasirisha mwenzako katika ndoa. Iwapo mambo haya hayahusu kutozingatiwa kwa Neno la Mungu au kutenda dhambi, mke au mume anaweza kujirekebisha kwa msaada wa roho mtakatifu kuivumilia na kuikuballi tabia ya mwenzake ama kutoitilia maanani. Bali iwapo tabia inayohusika inazidi kuchukiza au ni ya dhambi, anayeudhiwa anapaswa kumweleza mwenzake kwa mapenzi, upole na uvumilivu (Wagalatia 6:1) juu ya jambo linalomkera. Hapa pana haja ya kusema ukweli kwa upendo (Waefeso 4:15) na kueneza mwangaza wa upendo wa Mungu mioyoni mwetu (Warumi 5:5). Yule aliye na tabia ya kuchukiza mwenziwe hana budi kukubali kukosolewa bila hasira, kuekereka, kujitetea au kutaka kujilipiza. Kwa kawaida, wote wawili wanapaswa kuomba pamoja juu ya tatizo lenyewe. Baadhi ya watu waliooana wameonelea ni vyema kuandika orodha ya mambo wasiyoyapendelea kuhusu tabia ya kila mmoja na kuyajadili. Jambo hili lazima lifanyike tu iwapo pana mapatano ya wote wawili na lazima wote watilie mkazo katika mambo mazuri ya kupendeza katika tabia ya kila mmoja.

## Kuungama Makosa na Kusameheana

Kichwa hiki cha maneno ni ufafanuzi wa yale ambayo yametajwa hapo juu. Katika nyakati za udhaifu, haraka, uchovu, na kuwa mbali na Baba wetu wa mbinguni, tunasema ama kutenda mambo ya kijinga, dhambi au ya kuchukiza kwa watu wengine. Mara nyingi, yule mtu tunayemchukiza ni mwenzetu wa ndoa. Na kwa kawaida, kwa vile ni mwenzetu hatutilii sana maanani jambo hilo ama tunakuwa wenye kujitetea sana dhidi ya makosa yetu. Badala ya kusikitika kwa maneno au matendo yaliyomdhuru mwenzetu, tunakasirika eti kwa nini mwenzetu hawezi kupuuza mambo ya kimchezo tunayosema au kutenda. Jambo hili linaweza kuleta mabishano ya hasira na kugombana. Au, matokeo mabaya zaidi ni pale ambapo mtu mmoja hulipiza kwa “kumpa mwenzake kisogo” au kumnyamazia.

Linalohitajika katika hali kama ile ni msamaha—hii ni kusema, mwenye kuhusika kuungama kuwa ana kosa. (Mara nyingi wote wawili

hutokea kuwa wenye makosa wakati suluhisho linapofikiwa.) Na ifahamike kuwa maneno kama vile, "Nasikitika iwapo nimekukosea," hayamaanishi kuungama makosa. Bali yanamwekea hatia yule ambaye aliyeudhika kwa kuwa na hisia ambazo zinakasirika kwa haraka. Zaidi ya maneno, "Nakupenda," pengine maneno yaliyo muhimu sana kwa wale waliooana ni, "Mpenzi, nilikosea; unaweza kunisamehe?" Kuomba msamaha kwa Mungu hakutoshi iwapo hakuandamani na kuwaomba msamaha wale ambao tumewakosea (Mathayo 5:23,24; Yakobo 5:16; Mithali 28:13).

Kwa moyo huo huo, panapaswa kuwepo na kusameheana kati ya waliooana na watu wengineo. Si lazima kusubiri kuungama dhambi ili kutimiza jambo hili. "Hiari ya binadamu humfanya kuhairisha ghadhabu; na ni heshima kwake kuepuka uovu" (Mithali 19:11). Hebu yafikirie maovu yote ambayo Mungu ametusamehe; Sehemu kubwa ya makosa yetu hata hatuitambui. Tukifahamu haya yote, tunawezaje kukataa kuwasamehe wengine? (Mathayo 6:12,14,15; 18:21-35; Luka 17:3,4; Waefeso 4:32; Wakolosai 3:13).

Kwa kumalizia, kuhusu kusameheana, kuna kanuni muhimu iliyotajwa katika 1 Wakorintho 13:5: "[Upendo] haufikirii maovu." Kwa jumla maneno haya yanamaanisha kwamba upendo haukumbuki na kuhifdahi orodha ya maovu yote uliotendewa. Kwa hivyo, funzo kwa waume na wake ni kuwa wasiwekeane hasira na visasi ama kufufua maovu ambayo tayari yamekwisha ungamwa na kusamehewa.

## Uhusiano wa Kimwili

Kwa wale walioposana au wanaojitayarisha kuooana, onyo lilitolewa katika sura iliyotangulia kuwa hawapaswi kuingia katika mapenzi ya kimwili ambayo yanakubalika tu katika ndoa. Pia ilitajwa kuwa uhusiano uliojengwa juu ya mapenzi ya kimwili, usiokuwa na msingi imara wa kihisia na kiroho, hauwezi kudumu kwa muda mrefu baada ya fungate. Hii sio kusema kuwa mapenzi ya kimwili yanapaswa kupuuzwa lakini ni kusisitiza mambo mengine kuhusu ndoa ambayo hayatiliwi maanani sana. Kwa hakika, isipokuwa uhusiano uwe umejengwa juu ya mapenzi ya Kikristo, utageuka kuwa ni kitendo tu kisichokuwa na hisia na jambo la kibinafsi na hivyo kuleta mafarakano na chuki. Uhusiano mathubuti wa kiroho kwa upande mwengine, utaimarisha kufurahiwa kwa uhusiano wa kimwili.

Hebu tufikirie ushauri uliotolewa kwa wachumba wawili kuhusu maingiliano ya kimwili. "Na mume amtoshelezee mkewe haja zake na hali kadhalika mke naye amtoshelezee mumewe. Mke hana mamlaka

juu ya mwili wake bali mumewe anayo; na pia mume hana mamlaka juu ya mwili wake bali mkewe anayo. Msinyimane isipokuwa kwa masikilizano yenu kwa muda mfupi, ambao mtakuwa mkiomba, na tena muwe pamoja, shetani asije akawajaribu kwa sabau ya kujinyima kwenu" (1 Wakorintho 7:3-5 JND). Sio tu katika jamii ya Korintho ya karne ya kwanza bali katika historia nzima ya Kanisa mpaka leo pana Wakristo wanaofikiria kuwa maingiliano ya kimwili katika ndoa ni jambo linaloiteremsha hadhi na heshima ya Mkristo anayeishi kiroho. Wengine wamefikia hata kutengana na wake au waume zao ili "waishi maisha mazuri zaidi kiroho." Wengine wamepuuza uhusiano wa kimwili katika ndoa zao kwa sababu kama hizo. Lakini mtume Paulo anaonya kuwa hapana mtu afaaye kumnyima mwenzake uhusiano wa kimwili. Isipokuwa wote wawili wakubaliane kuishi kwa kujinyima uhusiano huo kwa sababu ya maombi na ushirika na Mungu, "kwa muda mfupi," mpango kama huo haupaswi kutekelezwa. Na jambo hili lifanyike tu kwa muda mfupi ili pasitokee mmoja wao akajaribiwa na Shetani kutenda uasherati kwa kukosa kutimiziwa haja zake za kimwili.

Neno la Kigriki "kukataliana" lililotumika katika 1 Wakorintho 7:5 linaweza kutafsiriwa kama "kufukuza, kukataa, kukana." Uhusiano wa kimwili haupaswi kutumiwa kama kilab uhusiano wa kimwili mwenzake kama njia ya kumlazimisha kukubali jambo lolote. Nguzo za maombi, ushirika na mapenzi zilizojadiliwa hapo mbeleni, zinapaswa kutumika katika hali kama hizi.

Maneno mengine matakatifu kuhusu uhusiano wa kimwili kati ya watu waliooana ni "Jitoleeni nyinyi kwa nyinyi kwa kumcha Mungu" (Waefeso 5:21). Upendo wa Kikristo (ulio mtakatifu) utawaongoza watu hawa kufahamu hisia na mahitaji ya wenzao. Upendo utamwongoza mume au mke kuachilia mbali haja zake za kimwili iwapo itatatambulikana mwenzake hana hisia kama hizo. Kwa wakati ule ule, yule asiyekuwa na haja anaweza kuongozwa na upendo kujitolea kwa mwenzake ili kumtoshelezea haja zake. Kutokana na upendo wao, kila mmoja atapenda kuwa wa kwanza kujitolea kwa mwenzake.

Iwapo mmoja wao atakuwa hana haja ya maingialiano ya kimwili mara kwa mara, ni kwa sababu pengine amemkasirikia mwenzake ama anayo sababu nyingine. Pia hapa, kama ilivyoelezwa hapo awali, pana haja kubwa sana ya mawasiliano. Kuwekeana hasira moyoni sio maisha ya Kikristo. Aliyekosewa anapaswa, kwa mapenzi, uvumilivu na unyenyekevu kumweleza mwenzake namna ya kosa alilotendewa

(Mathayo 18:15) Na mwenzake anafaa kuomba msamaha kwa kosa lolote ili furaha ya ndoa ipate kurejelewa haraka.

Kama tulivyoona hapo juu, wake wanaambiwa wajitolee kwa waume zao (Waefeso 5:22). Lakini agizo hili lisitumiwe na waume kama njia ya kujiridhishia haja na mahitaji yao yoyote mengine. Kwa sababu hii, vifungu 23 na 24 vimetiliwa nguvu na vifungu 25-29 vinavyohimiza mapenzi ya mume kwa mkewe. Isitoshe, pia ikumbukwe kuwa wanawake wanaweza kujitolea kwa waume zao kwa njia nyingi ngingine katika maisha, huku pia waume hawa wakiwa na mamlaka ya kusimamia nyumba zao. Kristo alichukua nafasi ya mtumishi ingawaje alikuwa mwenye cheo cha kunyenyekewa na wote. Itakuwaje sisi ambao hatuna cheo kikuu kama hicho kuchukua nafasi ya juu kuliko ile aliyoichukua Kristo kwa upendo wake? (Yohana 13:16)

## Usimamiaji wa Pesa

Kuna mafunzo kadhaa ya kibiblia kuhusu usimamizi wa pesa katika jamii. Kwanza, kufuatia 1 Wakorintho 11: 3, Waefeso 5:23,24, na 1 Timotheo 2:12,13, mume ndiye kichwa cha mke. Kwa hivyo, mume anapaswa kuwa na jukumu la juu zaidi katika kusimamia mapato ya kifedha katika jamii. Inaweza kutokea kuwa mume hajui hesabu hata kidogo na hali mkewe amesomea uhasibu; katika hali kama hiyo, wote wawili wanapaswa kushirikiana katika ulipaji wa madeni, kusawazisha akiba zao n.k. Bali uwezo wa mwisho wa usimamizi na matumizi ni wa mume.

Mara nyingine, mume anaweza kufikiri kwamba kwa vile pesa zake alizipata kwa kuzitolea jasho yeye binafsi, ana haki ya kuzitumia kama atakavyo. Mke anayefanya kazi pia anaweza kupata mawazo kama hayo hasa iwapo mumewe ameonyesha kufikiri hivyo. Hata hivyo, si jambo la busara kutofautisha “pesa za mume” na “pesa za mke.” Funzo la Biblia kwamba, “Wote wawili watakuwa mmoja,” halimaanishi muungano wa kimwili baina ya mume na mke. Linahusu pia kuunganisha mapato yao na kutumia kila kitu pamoja wala si kuwa na akiba tofauti katika benki. Kwa hivyo, tunapaswa kukumbuka kuwa vyovyote tulivyo navyo viwe vitu au mapato, vipawa, uwezo na akili, ni vyake Mungu na ametukabidhi kama mikopo au talanta (1 Samweli 2:5-7; Ayubu 1:21; Luka 16:12). Tunalo jukumu kwa Mungu la kutumia vyote alivyotupa kwa utukufu wake na kuwasaidia watu wake, wala sio kujitafutia heshima na vyeo katika ulimwengu ama kutosheleza mahitaji yetu ya kimwili.

Ni jambo la hekima kwa mume na mke kupanga matumizi yao

mara kwa mara pamoja kutegemea mali zao, mapato wanayoyategemea wakigawa kiasi fulani kwa chakula, nguo, matumizi ya nyumbani, gari, huduma za kinyumbani kama maji na umeme, nk. na pia wakitenga kiasi cha akiba kwa kununulia vitu vya gharama kubwa pamoja na matumizi ya wakati wa dharura. Pia waombe pamoja Mungu awape hekima juu ya matumizi, uwekaji akiba na namna ya kununua vitu mbalimbali. Maombi pia yanapaswa kufanywa katika kutoa fungu fulani (kabla ya kulipa kodi) la mapato kwa miradi ya jamii inayohitaji misaada. Ingawa agizo la Agano la Kale juu ya utoaji huu linasema tutoe sehemu ya kumi kwa mia, kama ishara ya shukrani zetu kwa Mungu kwa wingi wa neema zake na vipawa vyake kwetu, tunaweza kutoa hata zaidi ya kumi kwa mia ya mali zetu kwa kusaidia kazi ya Mungu.

Mtego ambao watu wengi waliooana huangukia na ambao mara nyingi huishia kuiharibu ndoa yao, ni kutamani kiwango cha juu cha maisha kutokea mwanzo. Kuna tabia ya vijana wengi kutaka kuishi maisha ya kiwango cha wazazi wao tangu mwanzo bila ya kukumbuka kuwa wazazi wao walianzia maisha ya kiwango chini na walijaribu kuishi kulingana na mapato yao. Katika kujaribu kudumisha kiwango hiki cha juu cha maisha, vijana hawa hujikuta mara wametumbukia katika madeni na sehemu kubwa ya mshahara wao wa kila wiki hutumika kuwalipa wadai wao. Ili kugharimia matumizi yao, mume huanza kujitolea kufanya kazi kwa masaa mengi zaidi ama hutafuta kazi ya pili na mke pia hupata kazi au hata kazi mbili. Kama matokeo, mume na mke huwa hawaonani na iwapo watapata watoto, wao hupelekwa kwa mayaya; na uhusiano wao wa ndoa huanza kudhoofika na hata kufikia kumalizika.

Sikiliza Neno la Mungu linasema nini kuhusu jambo hili: "Wema pamoja na kutosheka ni pato kuu. Kwani hatukuja ulimwenguni humu na chochote na ni hakika hatutatoka humu na chochote. Na tukiwa na chakula na mavasi, tuwe wenye kuridhika" (1 Timotheo 6:6-8). "Kuweni wenye kuridhika na mlivyo navyo" (Waebrania 13:5). "Msiwe na deni la mtu yeyote, bali mpendane nyinyi kwa nyinyi" (Warumi 13:8). "Mdeni ni mtumwa wa mdai" (Mithali 22:7).

Paul Wilson katika kitabu chake, *The Institution of Marriage* (Bible Truth Publishers, Addison, IL) anatoa mashauri yafuatayo kuhusu jambo hili: "Sio mtindo wa jengo la nyumba, wala muundo wa gari ambavyo ni vipimo vya kuonyesha maendeleo ya Mkristo, bali ni swala, je katika ile jamii pana tabia ya kumcha Mungu na mioyo yenye kutosheka? Baadhi ya Wakristo wenye furaha zaidi ni wale ambao

wana mali chache sana za kidunia bali ambao wanafurahia Kristo na Mambo yanayohusu Mungu na ambao pia wametosheka kwa hivyo vitu vichache vya kilimwengu walivyo navyo. Kutamani sana vilivyo nje ya uwezo wa mtu huleta kudhoofika kwa nafsi katika upande mmoja na kinyume cha furaha katika upande mwingine.

"Hata kwa mtazamo wa kidunia, ni jambo la furaha kwa vijana wawili waliooana karibuni kuonea fahari kufanya kazi pamoja kumaliza ujenzi wa nyumba yao ama kutengeneza viti, meza, vitanda, makabati, mashubaka ama vitu vinginevyo muhimu katika nyumba. Tumesikia watu wasiookoka wakisema kwamba njia nzuri zaidi ya kuwafanya vijana waliooana hivi karibuni kukosa kuridhika ni kuwapa kila wanachokihitaji, na kuwafanya wasiwe na kitu cha kuwashughulisha."

Kwa kumalizia, kama vile mtu anavyoweza kukataa uhusiano wa kimwili kwa sababu ya hasira ama chuki, mume au mke aliyekasirika anaweza kujaribu kumaliza hasira yake kwa kwenda kununua vitu au kutumia mali ovyo. Jambo hili, kama ulevi, linaweza kumleta nafuu ya muda kutokana na hasira bali, kwa hakika, hufanya tu mambo kuharibika zaidi. Suluhisho lifaalo, kama ilivyoelezwa hapo awali, ni kuzungumza na mume au mke kuhusu dhiki aliyo nayo mtu kwa upendo na upole katika kulitafuta suluhisho la tatizo lenyewe.

Tumalizapo sura hii juu ya mambo muhimu kwa furaha katika ndoa, tusikilize maneno ya mtume Paulo juu ya haja ya kuomba kila mara ... kwa bidii na kujitolea kwa mitume wote (Waefeso 6:18). Tusisahau mitume wengi waliokuwa wameoa waliomba wawe na furaha katika ndoa zao. Tusingojee hadi ndoa imeanza kuharibika kabla ya kuwaombea wahusikao. Na Mungu anapotufahamisha kasoro fulani katika ndoa ya watu fulani, tumwombe Mungu atupe njia ya kuwasaidia watu hao. Pengine, pangekuwa na "dawa nyingi" za kuzuia, pangekuwa na ndoa chache sana zenye "ugonjwa" ama zinazokufa na nyingi zaidi zingekuwa zenye furaha hivi leo.

Mawazo zaidi juu ya jinsi ya kuwa na furaha katika uhusiano wa ndoa yametolewa katika Nyongeza 2 kwa kichwa cha maneno, "Watu Wafaao Kuoana." Mapendekezo kadhaa kuhusu machapisho ya kusoma juu ya somo hili yametolewa hapa chini:

1. Lahaye, Tim: *How To Be Happy Though Married*. Wheaton, IL: Tyndale House Publishers, 1968.
2. Swindoll, Charles R.: *Strike the Original Match*. Portland, OR: Multnomah Press, 1980.

3. Wilson, Paul: *The Institution of Marriage*. Addison, IL: Bible Truth Publishers, 1969.
4. Wright, H. Norman: *Communication: Key to Your Marriage*. Glendale, CA: G/L Publications, 1974.

# 4

# *Kuoana na Mtu Asiyekuwa Mkristo*

Ni jambo la kusikitisha kuwajua watu au kukutana na watu waliooana ambao ni mmoja wao tu aliyeokoka. Ni lazima iwe vigumu kwa watu kama hao kufurahia uhusiano wa furaha ambao hupatikana tu na watu wawili wakiwa wanaishi ndani ya Bwana. Huruma zetu zinawafikia watu kama hao na tunamhakikishia yule aliyeokoka kwamba tutazidi kuwaombea. Lakini tunaweza kufanya zaidi? Kunayo mashauri ambayo tunaweza kuwapa ndugu na dada zetu walio katika hali kama hizo? Hebu tutafute mafunzo katika Neno takatifu la Mungu.

Katika 1 Petro 3:1-4 tunaona mawaidha yafuatayo yakitolewa kwa mke wa mume asiyeokoka: "Vivyo hivyo nanyi wake muwe wanyenyekevu kwa waume zenu; ili kwamba hata ikiwa hawajalikubali Neno la Mungu, waweze kugeuzwa nia zao bila ya neno lakini kwa mazungumzo mema na wake zao. Wanaposikia mazungumzo yenu mazuri pamoja na kuwaheshimu. Kujirembesha kwenu kusiwe kwa wasifu wa nje wa kusuka nywele, kujipamba kwa dhahabu au kuvaa nguo; bali kuwe kwa siri ya moyoni, katika kile kisichoharibika, hasa mapambo ya moyo mnyenyekevu, na roho tulivu, ambavyo ni vya thamani kuu mbele za Mungu."

Jambo la mwanzo alilolitaja mtume ni kuwa wake wanapaswa kuwa chini ya mamlaka ya waume zao. Tumeeleza katika sura iliyotangulia umuhimu wa kuhakikisha furaha pale watu wawili waliookoka wanapooana. Ni jambo muhimu pia iwapo mume hajaokoka, kuwa ili kuleta furaha na udhabiti katika ndoa, mke awe na ushuhuda wa wokovu kwa mume ambaye hajaokoka. Tabia ya upole (kifungu 1), utakatifu (kifungu 2), na moyo mpole na mnyamavu (kifungu 4) ni mambo muhimu katika tabia ya mke ambaye atamani kuokolewa kwa mumewe. Neno "mazungumzo" halifai hasa katika toleo la Biblia la

"King James." "Tabia" ni neno bora zaidi. Funzo kuu katika kifungu hiki cha Biblia ni kwamba mume haokolewi na kuhubiriwa kwingi na kubembelezwa na mkewe lakini ni kwa utakatifu, unyenyekevu, upole na unyamavu wa tabia ya mkewe. Mara nyingi, mke anaweza kujaribu kwa bidii kumsukumia mumewe mafunzo ya Kikristo. Kutapakaza mafunzo ya Biblia katika nyumba nzima, kutundika kutani makaratasi yenye mahubiri, kufungulia redio kituo cha Biblia wakati mume afikapo nyumbani, na kuwaalika wageni Wakristo nyumbani kumzungumzia mumewe, kunaweza kumfanya mume ajitenge mbali na Mungu. Kwa upande mwingine, mume anamchunguza mkewe kuona ni athari gani ambayo Kristo na maisha ya Ukristo yatakuwa nao juu ya maisha ya mkewe. Iwapo mkewe anaishi maisha ya Kikristo (angalia 1 Petro 2: 21-23 kwa maelezo zaidi kuhusu maana ya maisha ya Kikristo), kwa bidii akiyatumikia mahitaji ya mumewe ya kimwili, kihisia, na mahitaji mengine ya kimaisha aki-mwonyesha upendo na upole, haya yote bila shaka mumewe atayatambua.

Hoja nyingine iliyoelezwa na mtume ni juu ya mavazi. Mke anapaswa kuvaa mavasi ya kadiri kila wakati bila ya kuvutia hadhari ya watu kwake kwa sababu ya nguo au mapambo anayoyavaa. Mumewe anaweza kuanza kumdhaania mkewe kwamba anao watu wanaomtamani kati ya marafiki Wakristo, na kwa hivyo anahitaji kuwa na hakika juu ya kujitolea kwa mkewe kwake.

Kuhusu kifungu kisemacho, "Wake jinyenekezeni kwa waume zenu," swali la kutatiza linalozuka hapa ni, je, "Huku kujitolea kunapaswa kuwa kwa kiasi gani?" Mke anapaswa kunyenyekea mumewe na kubaki nyumbani au anapaswa kumkaidi mumewe na kudai "tunapswa kumtii Mungu badala ya binadamu" (Matendo 5:29) na "bila kuasi ushirika wetu wa pamoja" (Waebrania 10:25)? Hapana majibu rahisi kwa maswali haya, bali ningeshauri kumnyenyekea mume katika jambo hili na mengineyo yasiyomlazimisha mke kutenda dhambi. Ni jambo la kutusaidia kukumbuka kuwa, ijapokuwa binadamu huangalia wasifu wa nje wa mtu, Mungu huangalia ndani ya moyo. Iwapo moyo wa dada yetu anayehusika uko pamoja na washiriki wengine—iwapo anatamani kuwa nao bali anazuiliwa na mumewe—Mungu analifahamu jambo hili. Watu wengine wanaweza kudai kuwa agizo la Mungu kwamba tusiache kuhudhuria "ushirika wa pamoja" linapaswa kufuatwa badala ya amri ya mume kuwa mkewe abakie nyumbani. Hata hivyo, mtu hapaswi kuhesabiwa kama aliyeacha ushirika iwapo amepatikana na majaribu kama vile ugonjwa mbaya na wa kudumu; lakini si ni jambo tofauti iwapo mtu amezuliwa

kuhudhuria ushirika kwa sababu ya mume aliyetaka asiyeokoka na kutii amri kama hiyo?

Kumtii mume kama huyo ni sawa na kuwa na utiifu bila ya kutafakari. Ni vyema kwa mke kutafuta kuelewa sababu za mumewe kumzuia. Pengine inaweza kuwa ni kwa sababu hataki mkewe kuondoka nyumbani. Anaweza kuwa anahofu kuwa mkewe hatosheki na usuhuba na upendo anaompa na kwa hivyo mkewe anautafuta uhusiano kama huo kwa marafiki zake ambao ni washiriki Wakristo wenzake. Anaweza kufikiri kuwa mkewe atapuuza kazi zake za kinyumbani ama hatakuwepo nyumbani yeye anapomhitaji. Ama iwapo mkewe alikuwa mtundu kabla ya kuokoka, mume anaweza kuwa anamjaribu ili kuona kama wokovu wake umembadilisha kitabia. Kwa hivyo, mke hana budi kufanya bidii kuu kumhakikishia mumewe kuwa anamjali sana na hufurahia kuwa pamoja naye. Ni lazima mke awe wa kwanza kupendekeza mambo ya kufanya na mahali pa kwenda akiwa na mumewe na hasa akizingatia mambo anayoyapenda mumewe. Iwapo mumewe anamruhusu kutoka nje, lazima mke awe anarudi nyumbani bila kuchelewa mara tu ibada inapokwisha. Na iwapo mke atahisi kuwa ni mapenzi ya Mungu kutomtii mumewe ili aweze kuhudhuria ibada ya ushirika, lazima ajaribu kumnyenyekea mumewe kila njia nyingine iwezekanayo.

Iwapo ni mume aliyeokoka na mkewe hajaokoka, mambo yatakuwa ni vile vile. Ingawa mume hahitajiwi na Neno la Mungu kutii matakwa ya mkewe kuhusu shughuli zake za Ukristo, ni lazima mume kufikiria hofu, mahitaji na matakwa ya mkewe. Anaweza kufikiria kupunguza baadhi ya shughuli zake za kikanisa ili kuwa na wakati wa kukaa na mkewe. Sharti mara kwa mara amhakikishie mkewe upendo wake kwake. Na pia, Petro anawahimiza waume, "kuwaheshimu wake zao kama vyombo vidhaifu" (1 Petro 3:7). Kwa vile wanawake huwa wadhaifu kimwili wakilinganishwa na wanume na huchoka haraka zaidi kuliko wanaume, mume anapaswa kuepuka kutoroka nyumbani kila mara kwa kisingizio kuwa anakwenda kumtumikia Bwana au kukutana na Wakristo wenzake, huku akimwacha mkewe aliyechoka tayari kufanya kazi za jikoni, kuwatayarisha watoto kwenda kulala, kupiga nguo za mumewe pasi, na kumtayarishia kifurushi chake cha chakula cha mchana. Tabia kama hii haitafaulu kumvuta mkewe kwa Yesu Kristo.

Maagizo zaidi yametolewa katika 1 Wakorintho 7:12-16. Ijapokuwa Wakristo sharti wafanye kila hali kujiepusha na uhusiano usiopatana wa ndoa, mara wanapojikuta katika uhusiano kama huo, hawapaswi

kujaribu kuuvunjilia mbali. Aliyeokoka ana jukumu kubwa la kumvuta mwenzake asiyeokoka na hata watoto wao kwenye wokovu. Lakini, je itakuwaje iwapo yule asiyeokoka atatoa sharti kwa mwenzake aliyeokoka kwamba: "Ama uache tabia zako zote za Ukristo, au sivyo nitaondoka." Msitari wa 15 katika kifungu hiki unasema kuwa yule aliyeokoa anapaswa kumruhusu mwenzake kuondoka katika hali kama hiyo. Ingawa kila juhudi lazima kufanywa kuokoa ndoa (kwa kufuata kifungu Mwanzo 2:24 na Mathayo 19:6), hapana mtu anayeamrishwa kufanya hivyo hasa kama kitendo chenyewe kitaharibu imani yake ya Kikristo.

Katika kufikiria 1 Wakorintho 7, inafaa kukumbuka msitari wa 5 amabao ulijadiliwa katika sura iliyotangulia. Kauli inayosisitizwa hapa ni kuwa waliooana wasinyimane mapenzi ya kimwili "isipokuwa wawe wamesikilizana kufanya hivyo kwa muda mfupi." Mume au mke Mkristo asifikiri kuwa uhusiano wake na Kristo utaharibika iwapo atazidi kuwa na uhusiano wa kimwili na mwenzake ambaye hajaokoka.

Vifungu ambavyo tumekuwa tukivijadili katika 1 Petro na 1 Wakorintho viliandikiwa watu ambao tayari walikuwa wameooana tayari kabla ya kuokoka. Mafunzo haya pia yanahusu watu ambao kwa kutotii 2 Wakorintho 6:14, makusudi wataooana na watu wasiookoka. Hata hivyo, matatizo mengine mengi yanaweza kuwepo kwa mwokovu ambaye ataliasi Neno la Mungu kuhusu uchaguaji wa mchumba wa kufunga ndoa naye. Panaweza kutokea tatizo la kushitakiwa na moyo kwa kutoungama dhambi hiyo ama kwa kukosa kujua iwapo Mungu anaweza kusamehe dhambi mbaya kama hiyo. Jambo hili linatukumbusha ahadi ya ajabu katika 1Yohana 1:9, "Iwapo tutaungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na mwenye haki kutusamehe dhambi zetu na kututakasa kutokana na maovu yote." Panaweza kuwa na chuki dhidi ya wale ambao hawakutenda kosa kama hilo na ambao sasa wanafurahia maisha yao katika ndoa ya Kikristo. Mwelekeo huu unapaswa kuungamwa kama dhambi. Mtu pia anaweza kupatwa na kujisikitikia, ambako kunaweza kuleta kukosa furaha, kama matokeo ya kufanya uchaguzi huo wa kijinga. Ama kwa upande mwingine, panaweza kuwa na uotaji wa ndoto za kutamani jinsi maisha yangelivyokuwa mazuri kama mtu huyo angeoana na mtu fulani aliye Mkristo. Kufikiria wakati uliopita, kuhuzunukia wakati uliopo, kuhofia wakati ujao ama kutamamani kindoto jinsi mambo yangeli-vyokuwa…lakini sivyo yalivyo, kutazidisha tu matatizo kumfanya mtu kuona vigumu kumpenda mwenzake na kudhoofisha

ushuhuda wa Kikristo ambao mtu angemtolea mwenzake. Kwa wale wanaojikuta katika hali kama hiyo, tunawashauri kufanya yafuatayo: tubu dhambi zako kwa Mungu na upokee msamaha wake. Dumu katika maombi (Wakolosai 4:2 JND), kwa wokovu wa mwenzako na pia kwa ajili ya hekima ya kiroho, uvumilivu na nguvu zako. Endelea kuamini kuwa Mungu atayajibu maombi yako. Endelea kujilisha kwa Neno la Mungu na kama una watoto, endelea kuwalisha Neno la Mungu pia. Zidi kuishi maisha ya Kikristo kwa moyo mkunjufu, upole na moyo wa kunyenyekea. Na ingawa u mnyonge, endelea kufuata shabaha hizi (Waamuzi 8:4); endelea kumfuata Kristo.

Kuna matatizo mengine mengi yanayomkumba mume au mke aliyeooana na mtu asiyekuwa Mkristo ambayo hatujayajadili. Mengi ya matatizo haya ni magumu kiasi cha kutushinda kujua tutatoa ushauri wa aina gani. Wale baadhi yetu tunaojuana na watu waliooana wenye shida kama hizo, natuzidi kuwasaidia kwa njia zozote tunazoweza—kwa kuwaombea daima, kuwasikiliza na kuwaonyesha masikitiko yetu kuhusu matatizo yao, na kwa kutowalaani au kuwakasirikia wake ambao hukosa kuhudhuria mikutano ya ibada au wanaoanda-mana na waume zao kwenda katika shughuli za kilimwengu kwa kuwatii waume zao ama kutaka kudumisha amani katika nyumba zao.

## 5

# *Talaka na Kuoana Tena: Mafunzo Muhimu*

Ni jambo la busara kuhusu maradhi ya aina nyingi kuwa kuzuia ni jambo bora kuliko kutibu. Funzo hili linahusu pia ndoa ambazo zimevunjika. Ni kwa sababu hii ndipo ushauri ukatolewa katika sura zilizotangulia katika kitabu hiki ili kuimarisha uhusiano wa ndoa. Kama mafunzo ya Neno la Mungu yangefuatwa katika kumchagua mchumba wa ndoa, katika tabia wakati wa kuchumbiana na kuposana na katika uhusiano wa ndoa yenyewe, maswala ya kutalikiana yangepungua, kama yasingekwisha kabisa. Masistizo maalumu yametolewa katika kitabu hiki kuhusu "mambo makuu katika kuhakikisha furaha katika ndoa." Kama hadhari ingefanywa kuhusu tabia ya unyenyekevu, upendo, kuungama dhambi na kusameheana, kudumisha njia za mawasiliano yafaayo baina ya waliooana, kusoma Neno la Mungu na kuomba pamoja na kufuata mafunzo ya Neno la Mungu kuhusu

mapenzi ya kimwili, usimamizi mzuri wa pesa na mapato, pamoja na mambo mengine yote juu ya uhusiano wa ndoa, hakungekuwa tu na mazungumzo machache kuhusu talaka, bali hasa kungekuwa na mengi ya kusemwa kuhusu ndoa zenye furaha. Kwa hivyo iwapo kuna msomaji wa kitabu hiki ambaye ameanza kupekuapekua katika maandishi ya Kikristo kutafuta maoni ya waandishi kuhusu hoja ya talaka na ndoa, tunamshauri apitie tena sura zilizotangulia katika kitabu hiki.

Iwapo kuna watu waliooana ambao wana shida ambazo zimewalemea, watafute mashauri kutoka kwa ndugu na dada Wakristo. Iwapo hapana mtu katika kanisa lao waliye huru naye ambaye wanaweza kumwendea kwa shida zao, vipo vituo vya Kikristo vya kutoa ushauri amabapo wanaweza kupata msaada kulingana na Neno la Mungu—badala ya yale ya kidunia na kibinadamu. "Katika wingi wa washauri, kuna usalama" (Mithali 24:6). Mara nyingi, ndoa huishia katika talaka kwa sababu mtu mmojawapo au wote wawili wamesubiri kwa muda mrefu kabla ya kutafuta msaada kutoka kwa washauri. Hadi kufikia wakati msaada unapoanza kutafutwa, madhara ya kihisia yanakuwa makubwa hivi kwamba ni vigumu kwa wahusikao kuweza kupatanishwa. Sote na tuombe ili Mungu aweze kuwatayarisha makasisi na washauri wengi miongoni mwetu—ambao ndugu na dada wenye shida watakuwa na imani na kujiona huru kuwaendea na ambao watakuwa na ujuzi wa Neno la Mungu na hekima ya kiroho pamoja na busara ya kuweza kuwasaidia watakaowataka ushauri. Na heri sote tuwe macho na kuwa na wajibu wa Kimungu kati yetu, tukitafuta kwa maombi kutumikiana kwa uwazi na unyenyekevu pale Mungu anapotuonyesha haja ya kufanya hivyo, kama katika ndoa zenye matatizo.

## Mafunzo Mawili Makuu

Hebu tuanze majadiliano yetu kuhusu hoja hii ngumu na yenye kuzusha ubishi mkali inayohusu talaka na ndoa kwa kuangalia mafunzo mawili makuu katika Neno la Mungu:

1. Mungu huchukia talaka. "Nachukia kutenganisha (talikisha), asema Yehova Mungu wa Israeli" (Malaki 2:16 JND). "Basi, kile alichokiunganisha Mungu, pasiwe na mtu wa kukitenganisha" (Mathayo 19:6).

2. Mungu hupenda kusameheana na kupatana. "Kuweni wakarimu nyinyi kwa nyinyi, wenye mioyo mikunjufu, mkisameheana kati yenu, kama Mungu, kwa ajili ya Kristo alivyowasamehe" (Waefeso 4:32).

"Mke…na apatanishwe na mumewe" (1 Wakorintho 7:11).

Katika enzi hizi ambapo kuna kutojali kwingi kuhusu talaka na mambo mengi yanayohusu uadilifu, wakristo wengi wana mazoea ya kuliangalia jambo hili kwa mtazamo wa kimakosa. Hoja yao muhimu huwa ni kutafuta mafunzo ya Neno la Mungu yanayoruhusu talaka na kufunga ndoa tena, kujaribu kueleza kifungu "kinachotoa uhuru" n.k. Hata hivyo, ni wajibu mkubwa kwa washauri kuhusu ndoa pamoja na ndugu na dada Wakristo kuwaelekeza watu wanaotazamia kufanya talaka waone haja ya kusuluhisha matatizo yao na uwezekano wa kupatana tena. Tunahitaji kujikumbusha na kukumbushana mambo ambayo Mungu ametufanyia. "Ametupatanisha naye kwa sababu ya Kristo" (2 Wakorintho 5:18). Pia "Mungu kwa ajili ya Kristo ametusamehe" (Waefeso 4:32) . Na je, si ni mapenzi yake kuwa tusameheane sisi kwa sisi (na hasa wake au waume zetu!) na tupatane sisi kwa sisi? Mungu ametupa "mafunzo ya upatanisho" (2 Wakorintho 5:18). Tunahimizwa kuwa "wakarimu sisi kwa sisi, wenye upole, tukisameheana kama Kristo alivyowasamehe" (Waefeso 4:32). Na tunapotubu dhambi zetu kwa Mungu kila siku, tukumbuke kuwa, "mkiwasamehe wengine dhambi zao, Baba yenu aliye mbinguni, pia atawasamehe; lakini msipowasamehe wengine dhambi zao, Baba yenu hatawasamehe dhambi zenu" (Mathayo 6:14,15). Haja hii ya kuwa na moyo wa kuwasamehe wengine inaonyeshwa pia katika hekaya mojawapo za Kristo. Katika mwisho wa hekaya tunasoma hivi: "Na Bwana (Tajiri) wake…akamwambia, wewe mtumishi muovu, nilikusamehe deni lote hilo kubwa kwa sababu ulinililia; je, hungemwonea huruma mtumishi mwenzako, kama nilivyokuhurumua?" (Mathayo 18:21-35).

Makosa mengi hufanyika katika ndoa nyingi. Talaka hutokea hasa kwa sababu mtu mmojawapo hataki kumsamehe mwenzake makosa haya. Tunasahau kwa urahisi ajabu mzigo mkuu wa dhambi ambazo Mungu ametusamehe kwa huruma na neema na kuanza kujihisi watakatifu huku tukikataa kuwasamehe wenzetu wa ndoa makosa ambayo ni madogo sana yakilinganishwa na makosa tuliyomkosea Mungu!

Sasa tutajadili mafunzo ya Neno la Mungu juu ya sababu zinazokubalika za talaka na kufanya ndoa tena. Bali tunapojadili msitari wa "hali inayoruhusu" katika Mathayo 5:32 na 19:9 na "sio katika utumwa" katika 1 Wakorintho 7:15, tunahitaji kuwa waangalifu tusiwe kama Wafarisayo ambao walitafuta njia za kufasiri Neno la Mungu ili kutimiza tamaa zao za kibinafsi. Ijapokuwa kunaweza

kuwa na hali zinazoruhusu talaka na kufanya ndoa tena kulingana na Neno la Mungu katika hali maalumu, tunahitaji kukumbuka daima mafunzo yaliyotolewa hapo juu kwamba *Mungu huchukia talaka na hupenda kusameheana na mapatano.*

## Misimamo Minne Kuhusu Talaka na Kufanya Ndoa Tena

Kuna maoni tofauti miongoni mwa wafuasi wa madhehebu ya Kikristo na hata miongoni mwa Wakristo waliozaliwa mara ya pili kuhusu talaka na kufanya ndoa tena. Maoni haya yanaweza kuwekwa katika mafungu yafuatayo:

1. Talaka haikubaliki katika hali yoyote ile.

2. Talaka inakubalika katika hali fulani maalumu, lakini kufanya ndoa tena hakukubaliki.

3. Talaka na kufanya ndoa tena yanakubalika katika hali fulani maalumu.

4. Talaka na kufanya ndoa tena yanakubalika katika hali zote.

Katika kujadili misimamo hii minne, kwanza tunaona wazi kwamba Mungu alidhamiria ndoa kuwa mkataba wa kudumu kati ya mwanmume na mwanamke. “Kwa sababu hii, mwanamume atamwacha baba na mama yake na kushikana na mkewe; na wote wawili watakuwa mwili mmoja. Kwa hivyo, si wawili tena bali mmoja. Basi, kile alichokiunganisha Mungu pasiwe na mtu wa kukitenganisha” (Mathayo 19:5,6 na Mwanzo 2:24). “Kwa sababu mke aliye na mume amefungwa na sheria kwake hadi kiasi atakachokuwa yu hai; lakini mume wake anapokufa, mke yuko huru kutokana na sheria iliyomfunga” (Warumi 7:2). Hata hivyo, wayahudi wengi waliasi Neno la Mungu kuhusu umuhimu wa ndoa na walitalakiana kwa sababu za kila aina (Mathayo 19:3). Wakati huo, mgogoro kuhusu talaka ulitokea baina ya vikundi viwili vya kidini vilivyoitwa Hileli na Shamai. Mwalimu wa kikundi cha Shamai alifundisha kutoka kitabu cha Torati 24:1 kwamba sababu iliyokubalika ya talaka ilikuwa ni makosa mabaya yaliyofanyika katika uhusiano wa ndoa, kosa lisilokuwa la kawaida na lililo chafu mno. Mwalimu wa kikundi cha Hileli, kwa upande mwingine, alikuwa na maoni ambayo hayakuwa makali sana na alishikilia kuwa mke angeweza kuachwa kwa hata kwa sababu ya makosa madogo kama vile kutojua kupika ama kutokuwa na sura ya kupendeza. Katika Mathayo 19 tunasoma ya kwamba Wafarisayo waliimwuliza Yesu maaoni yake kuhusu mgogoro huu. Jibu lake Yesu lilikuwa ni kuwarudisha Wafarisao katika maandishi

yao matakatifu (Mwanzo 2) kuhusu hali ya kudumu ya mkataba wa ndoa. Kisha alieleza "Yeyote anayemwacha mkewe isipokuwa kwa sababu ya uzinifu, na kuoa mke mwingine, atakuwa ametenda dhambi ya uasherati" (kifungu 9). Kwa vile uasherati ni uvunjaji wa sheria za Mungu, talaka lazima pia iwe ni uvunjaji wa sheria—isipokuwa kwa sababu ya uasherati.

Kuna waalimu wa Biblia ambao leo huichukulia tabia ya uzinifu kumaanisha makaribiano ya kimwili kabla ya ndoa. Wanadai kuwa msitari wa "isipokuwa" wa Mathayo 5:32 na 19:9, hauruhusu kuvunjwa kwa mkataba (kama alivyosema Yusufu, Mathayo 1:19), kwa sababu ya wachumba kutojuana kimwili, bali tu kwa sababu ya ukosefu wa uaminifu. Hata hivyo, maana ya Kigriki ya neno, "uzinifu" na jinsi neno hili linavyotumiwa katika agano jipya, haitilii nguvu madai haya. Watu bado hutofautisha kati ya "uasherati" na "uzinifu" kwa njia ifuatayo ya kijuujuu; "Uasherati" ni kitendo kiovu baada ya kufunga ndoa na "uzinifu" ni kitendo kama hicho kabla ya ndoa. Lakini neno la Kigriki "porneia" amabalo limetafsiriwa katika Agano Jipya kama "uzinifu," linamaanisha hasa kuwa na uhusiano na kahaba, na kwa hivyo, lina maana ya uhusiano wowote nje ya ndoa kabla au baada ya ndoa. Ijapokuwa makahaba wenyewe wakati huo wa zamani walikuwa mabibi vijana wasiokuwa na mabwana, mara nyingi watwana waliotekwa nyara katika vita, wanaume waliowaendea makahaba hao, mara nyingi hawakuwa wameoa. Neno la Kigriki "moicheia" linalotafsiriwa "uasherati" katika Agano Jipya, lina maana maalumu, yaani kujuana kimwili kati ya mume na mke asiyekuwa mkewe au mke na mume asiyekuwa mumewe. "Uzinifu," kama lilivyotumika katika maandishi matakatifu, ni neno la kawaida na mara nyingi linafungamanisha maana ya uasherati na uhusiano kabla ya ndoa. Jambo hili halionyeshi kuwa pana haja ya kuifunga maana ya neno "uzinifu" kumaanisha uhusiano usioruhusiwa kabla ya ndoa pekee.

Isitoshe, iwapo msitari wa "isipokuwa" ungehusu tu watu walioposana kuoana, hebu tutazame jinsi kifungu cha Mathayo 19:9 kingesomeka: "Yeyote atakayevunja mkataba isipokuwa kwa ajili ya uzinifu na kuoa mwingine, atakuwa ametenda uasherati; na yeyote atakayemwoa huyo aliyekuwa amechumbiwa na mtu mwingine, atakuwa ametenda uasherati." Kwa hivyo, kama hapajawa na ukosefu wa uaminifu na mkataba wa ndoa umevunjika kwa sababu nyingineyo, na watu wote wawili wamebakia mabikira, neno lingekuwa likisema kuwa watu kama hao watakuwa wanatenda dhambi iwapo wataoana

na watu wengine hapo baadaye. Matumizi kama haya, yanafinya maana ya neno "uasherati." Pia matumizi haya yanapotosha lengo la kuwepo kwa kipindi cha posa, yaani kuwawezesha wachumba kujuana kwa kutazamia uwezekano wa kuishi pamoja, kutambua mapema mambo yanayoweza kuzusha matatizo hapo baada ya kuoana, na kuomba pamoja ili Mungu awafahamishe mapenzi yake kuhusu ndoa inayokusudiwa—yote haya yakionyesha uwezekano wa kuvunjika kwa uhusiano endapo itafahamika kuwa sio mapenzi ya Mungu kwa ndoa ile kutimia. Kwa hivyo, kukifanya kile kifungu cha "isipokuwa" kuwa na maana tu katika kuvunjika kwa uhusiano wa posa kuliko talaka, hakuna ushahidi katika Neno la Mungu.

Kutokana na hoja zilizojadiliwa hapo juu, hoja ya kwanza kati ya zile nne zilizoorodheshwa—"talaka hairuhusiwi kwa sababu yoyote ile"—haina msingi wowote. Vile vile, misitari iliyodondolewa katika Mathayo 5 na 19 inoonyesha upungufu wa hoja ya nne—"talaka na kuoa tena yanakubalika katika hali zote." Sasa, iwapo talaka inaruhusiwa katika hali fulani, je, Neno la Mungu linaruhusu kufunga ndoa tena katika hali hizo hizo? Inaonekana tena kuwa, kwa kufuata Mathayo 19:9 linaruhusu: "Yeyote atakayemwacha mkewe isipokuwa kwa sababu ya uzinifu, na kuoa mwengine, atakuwa ametenda uasherati." Wengine wanawezakusema kuwa kifungu cha "isipokuwa" kinasisitiza "kumwacha mke wake" na sio kuoa tena. Hebu tukisome kifungu hicho mara nyingine, tukiacha kifungu kinachohusu kuoa mke mwengine: "Yeyote atakayemwacha mkewe isipokuwa kwa sababu ya uzinifu, atakuwa ametenda uasherati." Kwa hakika, kifungu hiki hakina maana tena isipokuwa tu kwa kufikiri kuwa anayetoa talaka, ataoa mke mwengine. Kama kuoa tena hakungekuwa kumeruhusiwa kwa hali yoyote ile, kifungu 9 kingekuwa kimeandikwa hivi: "Yeyote atakayemwacha mkewe na kuoa tena mwengine, atakuwa ametenda uasherati." Kifungu cha "isipokuwa" hakingekuwa na maana yoyote hapa. Kwa hivyo, hoja ya pili—"talaka inakubaliwa katika hali fulani maalumu lakini kuoa tena hakukubaliki katika hali yoyote"—hakina ushahidi wowote kutoka Neno la Mungu.

Tunabaki na hoja ya tatu—"talaka na kuoa tena yana-kubaliwa katika hali maaumu." Vipengele tofauti vya maana ya hoja hii vitajadiliwa katika sura ifuatayo. Tutajadili kama kuruhusiwa kwa talaka kunampa Mkristo uhuru wa kuanzisha utaratibu wa talaka katika hali yoyote ile. Tutaangalia pia swala gumu na lenye kutatanisha la kujaribu kufafanua maana hasa ya kifungu "hali fulani maalumu" ambamo talaka na kuoa tena yanakubalika.

# 6

# *Talaka na Kuoana Tena: Miongozo Kuhusu Hali Halisi*

Katika sura iliyotangulia, hoja nne kuu juu ya talaka na kuoa tena ziliorodheshwa na kujadiliwa. Kwa kufuata vifungu tofauti katika Neno la Mungu, hasa Mathayo 5:32 na 19:9, hoja tatu kati ya hizi zilionyeshwa kuwa hazina ukweli kulingana na Neno la Mungu, na hivyo hoja iliyobakia ni kwamba, "talaka na kuoa tena yanakubalika katika hali maalumu." Hata hivyo, kama ilivyotajwa mwishoni mwa sura iliyopita, tunahitaji kufafanua maana ya "hali maalumu" ambamo talaka na kuoa tena yanakubaliwa tena kulingana Neno la Mungu. Hili ndilo swala linalojadiliwa katika sura hii.

Hali nne zinazojadiliwa katika sehemu hii ni hizi zifuatazo:

1. Mkristo amepata talaka na mwenzake aliyemtaliki amefunga ndoa tena.

2. Mtu aliyeoana na Mkristo ametenda uzinifu lakini hajamtaliki Mkristo.

3. Mtu aliyeoana na Mkristo anapata talaka bali hafungi ndoa tena wala kutenda uzinifu.

4. Mkristo anakimbiwa na mwenzake wa ndoa.

## Talaka na Kuoa Tena Kwa Mtu Aliyeoana na Mkristo

Iwapo Mkristo amefanya talaka na mwenzake amefunga ndoa tena, jambo hili linaweza kuhesabiwa kama "uzinifu wa hali ya juu" kwa upande wa huyo aliyeoana na Mkristo. Kwa hivyo, inaweza kueleweka kutokana na Mathayo 5:32 kuwa Mkristo, katika hali hii yuko huru kufunga ndoa tena wala hatakuwa ametenda uasherati. Lakini, lazima pia kuongezea kuwa yule aliyetalikiwa (au kufiwa), si lazima kujisikia sharti afunge ndoa tena, lakini anapaswa kufikiria kwa kumuomba Mungu kama ingekuwa bora kuoa tena au kubaki bila kuoa. Mtume Paulo anatoa ushauri, "Nawaambia makapela na wajane, ni vizuri kuishi kama mimi. …Umeachana na mkeo? usitafute mke mwingine" (1 Wakorintho 7:8,27; angalia pia vifungu 32-34, 38-40). Yule aliyepoteza mume au mke kwa kufiwa ama talaka anapaswa kutafuta Mungu anataka kumfundisha nini kwa majaribu kama haya na kuhakikisha kama Mungu anayo kazi maalumu

amabayo angependa aifanye akiwa hajafunga ndoa. (Angalia sura ya kwanza kwa maoni zaidi kuhusu jambo hili.)

## Uzinifu Pasipo na Talaka Kwa Upande wa Mtu Aliyeoana na Mkristo

Iwapo mtu aliyeoana na Mkristo atazini na akose kutalikiwa na Mkristo, itamaanisha kuwa, kwa kuzingatia tena Mathayo 19:9, Mkristo amepewa ruhusa ya kutaliki mwenzake asiyekuwa Mkristo na kuoa tena bila ya kuhesabiwa kuwa ametenda uasherati. Kama alivyotajwa katika sura iliyopita, kwa sababu ya matumizi tofauti ya neno "uzinifu" katika Neno la Mungu, yaonekana hapana msingi wa kuruhusu talaka kwa sababu ya aina tu fulani za dhambi za kujuana kimwili na sio kwa sababu za dhambi uzinifu wa aina nyingine. Hata hivyo, kwa mkristo ambaye anatazamia kutafuta talaka kutoka kwa mwenzake asiye Mkristo, kuna mambo kadhaa ya kufikiria.

Kwanza kabisa, ni muhimu kufikiria juu ya mwelekeo wa "mtu anayedai hana kosa" kuhusu ndoa na kuhusu yule aliyezini. Kama ndoa inazidi kuharibika, inawezekana kwamba mmojawao ama wote wawili wahusikao—badala ya kuchukua hatua zifaazo za kuungama, msamaha, mapatano, n.k.—wanatafuta kisiri mafunzo ya Neno la Mungu kama sababu za kuivunja ile ndoa. Kosa moja tu la mwenzake la kuzini, liwe la zamani au wakati uliopo, liwe limetubiwa au la, linaweza kuchukuliwa kama sababu ifaayo tu kufanya talaka. Kwa kufuata kifungu cha "isipokuwa" cha Mathayo 5:32 na 19:9 pekee, hapana anayeweza kupinga sababu hii. Lakini ni lazima kulifikiria jambo hili kwa mjibu wa *mafunzo yote* ya Neno la Mungu. Lazima tuipime tabia ya kulichukulia kosa moja la kuzini kama kisingizio cha talaka kwa kulinganisha na mafunzo mengine makuu kama yale yaliyoelezwa katika sura iliyopita kwamba *Mungu anachukia talaka na hupenda kusameheana na mapatano.* Bila shaka, iwapo mtu aliyetenda dhambi ametubu dhambi yake, pana jukumu la kumsamehe, kama vile, Mungu "ni mwenye imani na haki kutusamehe dhambi zetu" tunapotubu kwake (1 Yohana 1:9); tunahimizwa "kusameheana sisi kwa sisi kama vile Mungu kwa ajili ya Kristo alivyowasemehe" (Waefeso 4:32). Lakini, jambo muhimu zaidi, Mungu ametusamehe zaidi ya makosa ambayo tumeyakiri na kuyatubu. Na daima Mungu yuwatafuta watoto wake waliopotea na kutangatanga ili kuwarudisha kwake. Je, tunapaswa kuwa tofauti na Baba yetu wa mbinguni katika jambo hili? Hatupaswi kuwa wavumilivu tukiombea na kutafuta njia za kuwarudisha na kupatana na wenzetu wa ndoa haidhuru hata

kama dhambi zao ni kubwa au zimetapakaa kiasi gani?

Kuhusu jambo hili, inafaa kusoma milango mitatu ya kwanza ya kitabu cha Hosea juu ya mtume huyu na mkewe. Kwa kufuata maagizo ya Mungu, Hosea alioa mwanamke kahaba, na akazaa watoto watatu naye. Kulingana na sheria za Musa, Hosea hangekuwa na kosa kama angeshauri mkewe kuuawa kwa kupigwa mawe kwa sababu ya uzinifu. Lakini, kinyume na hayo, Hosea alifuatana na mkewe kila mara akijaribu kujua mkewe alipokuwa na akijaribu kwa njia tofauti kumrudisha kwake (Hosea 2:6-8). Mwishowe, mkewe alipofikia hali ya kuhuzunisha ya kuwa mtumwa, na kuwekwa kwenye soko la mnada ili kunadiwa, Hosea alimnunua mkewe kwa kumlipia kiasi cha vipande 15 vya fedha na kiasi fulani cha shayiri (3:2). Kisha Hosea alimwambia mkewe, "Utaishi nami kwa siku nyingi; hutakuwa kahaba tena, wala hutaishi kwa ajili ya mwanamume mwingine; nami pia vivyo hivyo nitakuwa wako" (3:3). Hii, kwa kweli, haikuwa tu hadithi ya Hosea na mke wake; iliandikiwa taifa la Waisraeli ili kuonyesha wingi na undani wa upendo wa Mungu kwa taifa la Waisraeli ambao walikuwa wamemuasi Mungu na kuabudu miungu ya sanamu. Kwetu sisi Wakristo, hadidhi hii ni mfano wa urefu ambao upendo wetu unapaswa kuufikia katika kutafuta kupatana na wenzetu wazinifu. Tukumbuke pia kuwa, mara nyingi kosa au udhaifu wowote hautokani na mtu mmoja pekee. Tabia yote ya binadamu ina sababu na inawezekana kuwepo na sababu katika ndoa inayohusika ya mtu mmojawapo kwenda kutafuta kutimiza haja zake nje ya ndoa.

Kwa hivyo, hata kabla ya kufikiria kutafuta talaka kwa sababu ya uzinifu, yule "asiye kuwa na kosa," anapaswa kuwa anafanya kila juhudi awezayo (kwa uwezo wa Mungu, hasa kwa mwongozo wa Roho Mtakatifu), kuleta marudiano na mapatano na yule aliyezini. Lakini itakuwaje iwapo mwenye kuzini anaendelea na tabia yake ya kutokuwa mwaminifu huku akiwa hataki kuuvunja mkataba wa ndoa? Hali kama hii inaaibisha uhusiano wa ndoa na kumletea yule mwaminifu na jammii nzima dhiki na mateso makuu; kwa hivyo ingekuwa bora kwa wote wahusikao kumlazimisha yule asiyekuwa mwaminifu kuamua amtakaye kati ya mumewe wa ndoa na huyo wa nje—ama kutengana na hata kupeana talaka.

Kufikia hapa, swali muhimu linafaa kuulizwa: Je, Neno la Mungu linaturuhusu kumpa talaka mwenzetu, katika hali kama hii ya tabia ya kudumu ya kuzini ya mwenzetu au sababu nyingine yoyote? Vifungu vya Mathayo 5:32 na 19:9 vinaonekana kama vinatoa ruhusa kama hiyo. Hata hivyo kifungu kingine kinaeleza suluhisho hilo kwa njia tofauti:

"Na kwa waliooana, natoa amri, lakini si mimi bali ni Mungu, Mke asimwache mume [asijitenge mbali naye], lakini, iwapo atamwacha, na abakie bila kuolewa, au apatane na mumewe; na mume asimtupilie mbali mkewe" (1 Wakorintho 7:10,11). Vifungu vya mtume Mathayo vinachukulia kuwa mume yu huru kumwacha mkewe kwa sababu ya uzinifu na hali mtume Paulo anasema wazi wazi kuwa mume *hapaswi* kumwacha mkewe. Sina jawabu yakini kwa utatanishi huu. Inawezekana kuwa mtume Paulo katika 1 Wakorintho 7 anaeleza mambo kwa jumla bila ya kufikiria hali maalumu inayohusu uzinifu. Kwa kueleza kuwa, "Ninawapa amri, lakini si mimi bali ni Mungu" (kifungu 10), anaonekana anasisitiza funzo lililomo katika Mathayo 19:16 na Marko 10:9: "Kile alichokiu-nganisha Mungu pasiwe na mtu wa kukitenganisha." *

Matumizi ya funzo hili kuhusu hali halisi ya uzinifu yametolewa katika misitari mitatu baada katika Mathayo 19:9. Kwa upande mwingine, maelezo haya yanaweza kutolewa kwa maana nyingine, kulingana na marejeleo yetu, Hosea na mkewe, uhusiano kati ya mume na mke unapaswa kuwa kielelezo cha uhusiano kati ya Kristo na kanisa (Waefeso 5:23-32). Yesu hatalitaliki Kanisa lake haidhuru hata Kanisa likiwa limekosa imani kiasi gani katika Kiongozi (Kichwa) chake. Mungu wetu mwenye baraka daima yuko tayari kutupatanisha naye pale tunapoteleza na kuiacha njia yake. Kwa hivyo, kwa mfano huo huo, inaweza kusemwa kwamba Mkristo hapaswi kumtaliki mke wake kwa ajili ya uzinifu wala mke Mkristo kumtaliki mumewe mwenye kutenda dhambi.

Kwa kuunganisha hoja hizi zote pamoja, inaelekea kuwa ni jambo la busara kwa Mkristo *kutotafuta kufanya* talaka. Kama ilivyoelezwa hapo juu, tabia ya mmojawapo wa watu waliooana ya kuzini daima inaweza kuzorotesha uhusiano hadi kufikia kiasi cha kutengana—pengine hata kuachana kisheria. Mlango unapaswa kuwa wazi kwa nafasi ya kufanya mapatano, na kutengana kunatoa fursa hii vyema zaidi kuliko talaka. (Kumbuka: hali nyinginezo isipokuwa tabia ya kudumu ya uzinifu—kwa mfano, kupiga mke au watoto—inaweza pia kumlazimisha Mkristo kutengana na mwenzake kwa muda. Lakini hata hivyo uwezekano wa kupatana lazima liwe ndilo lengo daima.)

Tuseme talaka imetokea katika hali kama hizi. Kulingana na vifungu vilivyomo katika injili ya mtume Mathayo, yule "asiye na kosa" anaweza kuoa bila ya kuhesabiwa kuwa ametenda uasherati. Hata hivyo, ingawa talaka inaonekana kuwa ni jambo la mwisho kabisa, haja na matumaini ya kupatana haipaswi kukoma pale

talaka inapokamilika. hayatawezekana. Kwa hivyo mtu aliyetalakiwa ingekuwa bora kumsubiri Mungu kufanya kioja chake na kuleta mapatano ama suluhisho lipatikane wakati yule asiyekuwa Mkristo atakapofunga ndoa tena na mtu mwingine. Hali kama hiyo, kama ilivyoelezwa hapo kabla, ni uzinifu mbaya sana na hufanya ndoa kutoweza kujengwa upya.

## Talaka Bila Kuzini Kwa Upande wa Mtu Aliyeoana na Mkristo

Mpaka sasa tumejadili swala la talaka na kufunga ndoa tena kwa Mkristo wakati zinaa au kufunga ndoa tena kwa mtu asiyekuwa muaminifu kumetokea. Hebu tufikirie hali ambapo Mkristo amepewa talaka na mwenzake na ambapo huyo mwenzake hajafanya ndoa tena wala hapana ushahidi wa kutokuwa mwaminifu. Swali muhimu hapa ni iwapo pana uhuru kwa Mkristo aliyetalikiwa kufunga ndoa tena.

Mafunzo ya Mungu katika Mathayo 5:32 yanaonekana dhahiri tena kuhusu jambo hili: "Yeyote atakayetengana na mkewe isipokuwa kwa sababu ya zinaa, *anamfanya mkewe kutenda uasherati*; na yeyote atakayemuoa mke kama huyo aliyetalikiwa, *atakuwa ametenda uasherati*." Kwa hivyo mke aliyetalikiwa akifunga ndoa tena, yeye na yule atakayemuoa, wote watakuwa waasherati; hii ni kwa sababu talaka kama ile haihesabiwi kuwa ya haki mbele za Mungu.

Kifungu cha 1 Wakorintho 7 kinarejelewa mara nyingi kuhusu hoja hii na kinatumiwa kutoa fasiri iliyo kinyume cha fasiri ya Mathayo 5:32. Kuhusu Mkristo ambaye ametalikiwa au kukimbiwa na mwenzake asiyekuwa Mkristo, kifungu 15, unasema, "Ndugu ama dada Mkristo hakuwekwa mtumwa katika hali kama hiyo." Msitari huu huchukuliwa na watu wengine kuwa kama kifungu kingine cha isipokuwa bali na kile cha Mathayo 5:32. Hii ni kusema, Mkristo yuko huru kuoa tena siyo tu kwa sababu yule anayetoa talaka ametenda uasherati, bali pia kwa kuwa si Mkristo. Tatizo kuu kuhusu funzo hili ni kuwa kifungu hiki cha "isipokuwa" badala ya kutilia nguvu kifungu cha kwanza cha "isipokuwa" kinatoa hoja pingamizi. Inawezekanaje kwamba Mkristo aliyetalikiwa na asiyekuwa Mkristo awe huru kuoa tena na hali imeelezwa, "Yeyote anayemtenga mkewe isipokuwa kwa ajili ya zinaaa, anamfanya mke kutenda uasherati"? Kile kinachoitwa kifungu cha "isipokuwa" katika 1 Wakorintho 7:15, hakiwezi kuwa na maana hiyo bila ya kupinga funzo la Mungu katika Mathayo 5:32.

Kifungu cha 1 Wakorintho 7:15 kina maana gani? Mktadha wa matumizi yake pamoja na maandishi yake asilia katika lugha

ya Kigriki (Kiyunani), yatatusaidia katika kukielewa kifungu hiki cha 1 Wakorintho 7 kwa undani. Katika kifungu 10 na 11, kama ilivyoelezwa hapo awali, tunayo maneno ya kifungu asilia: "Mke asimwache [ama kutengana] na mumewe; lakini iwapo atajitenga, na abakie bila kuolewa tena; ama apatane na mumewe; na mume asimwache mkewe." Kifungu hiki ni maneno ya fundisho lake Mungu katika Mathayo 19:6, "Basi kile alichokiunganisha Mungu, pasiwe na mtu wa kukite-nganisha." Kisha katika kifungu 12-16 mtume Paulo anajadili hoja ambayo Yesu haitaji moja kwa moja katika hotuba yake kwa wanafunzi wake. "Lakini kwa wale wengine nawaambia kuwa (si maneno ya Mungu bali yangu mwenyewe), iwapo ndugu Mkristo yeyote ana mke ambaye si Mkristo na ambaye atakubali kuishi naye kama mke, mumewe asimwache. Na dada Mkristo akiwa na mume ambaye si Mkristo, na ambaye amekubali kuishi naye kama mume, basi, mke asimwache mume huyo. Kwa sababu mume asiyeamini Neno la Mungu ametakaswa na mkewe na mke asiyeamini pia ametakaswa na mumewe; lau sivyo, watoto wenu wangekuwa wenye dhambi. Lakini sasa mu watakatifu. Lakini iwapo asiyekuwa muumini atajitenga, na ajitenge. Ndugu Mkristo ama dada Mkristo hakufungika katika hali kama hiyo. Lakini Mungu ametuita tuishi kwa amani. Kwani unajuaje wewe Mke kama hutamwokoa mumeo? au unajuaje wewe mume kama hutamwokoa mkeo?"

Katika mji uliojaa najisi na upotovu wa Korintho, haikuwa ajabu kwa Mkristo mpya kuwa alitangulia kuwa mwenye kuabudu sanamu na pengine mwaasherati na pia kuwa na mwenzake ambaye bado alikuwa anaishi maisha hayo ya kidhambi ya sehemu hiyo. Kwa hivyo, mtume Paulo, bila shaka aliulizwa swali kama ilikuwa ni haki kwa Mkristo kuendelea kuishi na mwenzake asiyekuwa Mkristo—kuendelea katika uhusiano huo usiolingana huku Mkristo akiwa ameungana na Kristo. Katika Agano la Kale, tunasoma katika kitabu cha Ezra 10 kuhusu Waisraeli ambao waliwaacha wake zao ambao walikuwa wamewaoa kutoka katika mataifa jirani. Je, hivi ndivyo Wakristo walivyopaswa kufanya na wake wao wasiokuwa Wakristo? La. Mtume Paulo anatoa ushauri kulingana na wakati wa neema ambamo tunaishi sasa: Iwapo asiyekuwa muumini angependa kuendelea katika ndoa ile, hiyo ni sawasawa; usiiache ama kuivunja ndoa. "Kwa sababu mume asiyeamini anatakaswa na mke na mke asiyeamini anatakaswa na mume" (kifungu 14). Maombi ya kila siku na ushuhuda wa Kikristo kwa mtu asiyekuwa muumini ni wa thamani kuu katika nafsi ya huyo asiyeokoka na mara nyingi humfanya kuokoka. Zingatia tena kuwa

mafunzo makuu kuwa ndoa ni kitu cha kudumu na kwamba Mungu huchukia talaka ni dhahiri katika maagizo yaliyotolewa hapa.

Bali, je, itakuwaje iwapo yule asiyeamini hapendi kuendelea katika ile ndoa? Itakuwaje iwapo anaona haya ama anafedheheka kwa kuwa na mke ambaye hatajiunga naye tena katika mambo yake kidhambi au kidunia kwa sababu mkewe angependelea kutumia wakati wake akisoma Biblia ama kuabudu na waumini wengine, n.k.? Itakuwaje iwapo mumewe atamtisha kuwa asipoiacha dini yake mpya, mumewe atamwacha au kumtaliki? "Iwapo asiyekuwa muumuni atajitenga, basi na ajitenge" (kifungu 15). Ingawa mapenzi ya Mungu ni kwamba ndoa iwe ni kitu cha kudumu, Mungu hamtarajii muumini kuitupa dini yake ya Ukristo ili kuiokoa ndoa yake isije ikaharibika. Ijapokuwa tunapaswa kuwa wapole au wanyenyekevu kati yetu kwa kumcha Mungu, na ijapokuwa wake wanapaswa kuwanyenyekea waume zao (Waefeso 5:21,22), unyenyekevu huu hauwezi kutekelezwa kwa kutomtii Mungu. "Tunapaswa kumtii Mungu wala sio binadamu" (Matendo 5:29); "Wake kuweni wanyenyekevu kwa waume zenu *kama inavyofaa mbele za Mungu"* (Wakolosai 3:18).

Jambo hili linaonekana kuwa msingi wa kifungu chetu kinachofuata, "Ndugu au dada Mkristo hakufungika katika hali kama hiyo" (1 Wakorintho 7:15). "Kufungika" kuna maana ya neno la Kigriki *douloo* linalomaanisha "kuwa katika hali ya utumwa au kugandamizwa." Kifungu hakisemi kuwa ndugu au dada Mkristo hayuko katika hali ya kufungika (neno la Kigriki lenye maana hii ni *doulevo*) bali kwamba *hakutiwa katika hali hii.* Kifungu hiki kinazungumzia hali mpya ya utumwa ambayo Mkristo atajitwisha iwapo atakubali kuiacha imani yake ya Kikristo ili kumzuia yule mwenzake asiyekuwa Mkristo asiivunje ndoa.

Baadhi ya watu wameeleza kwamba kifungu cha "hakufungika" kina maana kwamba mkataba wa ndoa (unaotajwa katika 1 Wakorintho 7:27,39 na Warumi 7:2) unavunjika pale ambapo yule asiye muumini anapojitenga au kutoa talaka, na hivyo kumruhusu muumini kuweza kufunga ndoa tena na mtu mwingine. Kwa kiasi fulani, dhana hii imetiliwa nguvu na kutoielewa maana ya maneno ya Kigriki katika vifungu vyote vinne. Katika 1 Wakorintho 7:15, "utumwa" ni *douloo,* hali katika Warumi 7:2 and 1 Wakorintho 7:27,39, "kufungika" ni *deo.* Wata-alamu kadhaa wa Biblia wamefasiri 1 Wakorintho 7:15, tuseme hasa sehemu katika kifungu hiki. Neno *Deo* linamaanisha "kufunga kama kwa kamba au minyororo," na linapatikana katika Marko 11:4 kuhusu "kitanda kilichokuwa *kimefungiwa* mlangoni,"

na katika Matendo 12:6 na 24:27 juu ya wafungwa waliokuwa wamefungwa kwa minyororo ama vifaa vingine. Neno *Douloo* pamoja na kitendo kinachoambatana nalo, *douleuo*, "kutumika au kuwa katika utumwa," yanatumika mara nyingine katika Agano Jipya kumaanisha kumtumikia bwana binadamu (kama katika Filemoni 16). Hata hivyo, maneno haya yanatumika mara nyingi kumaanisha utumishi wa kujitolea wa Wakristo kwa Mungu au kati yao wenyewe. Kwa mfano, "Mlifanywa watumishi wa utakatifu…na …watumishi wa Mungu" (Warumi 6:18,22); "Nilijifanya mtumishi wa wote" (1 Wakorintho 9:19); na "Kwa mapenzi tumikianeni nyinyi kwa nyinyi" (Wagalatia 5:13). *Deo* na *douloo* (na kitendo cha neno hilo) yana maana zinazotofautiana sana wala hayatumiwi kumaanisha kitu kimoja au kumaanisha viwango mbalimbali vya hali moja. Kwa sababu hii, pamoja na sababu iliyotolewa katika aya iliyopo hapo juu, hatuna sababu ya kudai kuwa kifungu "hawafungiki" katika 1 Wakorintho 7:15 kinamaanisha kuwa Wakristo wako huru kuuvunja mkataba wa ndoa.

Kuna jambo lingine lisiloeleweka vyema na watu wengi kuhusu "utumwa" unaotajwa katika 1 Wakorintho 7:15. Kulazimika kubakia bila kufunga ndoa tena kwa muda mrefu kwa matumaini ya kupatana kunaonekana na wengine kama utumwa. Mkristo hawezi kufurahia maisha ya ndoa pamoja na yule aliyeoana naye mwanzo, na wala hawezi kuwa huru kufunga ndoa tena iwapo mwenzake asiyekuwa Mkristo hajaivunja ndoa ya mwanzo kwa kuzini au kufunga ndoa tena. Kwa hivyo, inadaiwa kwamba "hawakufungika" katika 1 Wakorintho 7:15 kinamaanisha kuwa kuna uhuru kwa Mkristo kufunga ndoa tena katika hali kama hiyo. Hata hivyo, msitari huu hauambatani vyema na mktadha wa kifungu chote. Mtume Paulo hakuhesabu hali ya kubakia bila kufunga ndoa tena kuwa utumwa bali uhuru.

Inaweza kuelezwa basi ya kwamba ingawaje Mkristo hakutarajiwa kuacha imani yake ya Kikristo ili kumpendeza mwenzake asiyekuwa Mkristo na kuzuia ndoa yake kuvunjika, hapaonekani kuwa na idhini kamili ya kufunga ndoa tena. Kwa hakika, kulingana na Mathayo 5:32, kama ilivijoelezwa hapo juu, kufunga ndoa tena kwa Mkristo kutaleta lewa kuingia katika uhusiano wa kiuasherati iwapo mwenzake aliyekuwa Mkristo hakuzini ama kuivunja ndoa kwa kufunga ndoa na mtu mwengine. Kwa hivyo agizo lililotolewa kwa waliotengana au kutalikiana katika 1 Wakorintho 7:10,11—"bakieni bila kufunga ndoa tena ama mpatane"—linabakia kuwa thabiti katika hali kama hii.

Wale ambao hawakubaliani na maelezo haya na wanasisitiza kuwa

kifungu, "hawafungiki" kinamaanisha uhuru wa kufunga ndoa tena, ningependekeza kwamba mafunzo muhimu kuwa "Mungu huchukia talaka" na "Mungu hupenda kusameheana na mapatano," yafikiriwe kwa makini wakati hali kama hiyo ya kutolewa kwa talaka na mtu asiyekuwa Mkristo inapotokea. Kwa hivyo, fikira ya kufunga ndoa tena heri ikawishwe kwa muda murefu—pengine miaka kadhaa—ili kuwa na wakati wa kuona iwapo moyo wa asiyekuwa muumini utabadilika kutokana na nasaha ya uaminifu ya mwenzake Mkristo na haja ya kufanya mapatano. Kupatana na mtu aliyeoana naye mwanzo kuliko kuoana na mtu mwengine lazima liwe ndilo jambo muhimu zaidi katika fikira ya Mkristo.

## Kukimbiwa Kwa Mkristo na Mwenzake Asiyekuwa Mkristo

Tumekifikiria kifungu cha 1 Wakorintho kama chenye kuhusu kutolewa kwa talaka na mtu asiyekuwa Mkristo. Kinahusu pia kukimbiwa kwa Mkristo na mwenzake wa ndoa asiyekuwa muumini bila ya kutolewa kwa talaka rasmi. Maana ya "kukimbiwa" hapa ni kutoweka kwa mtu asionekane tena kwa muda mrefu. Hii kwa kweli ni hali ngumu sana kwa yule aliyeachwa hasa kwa kuwa ni hali isiyoeleweka. Haifahamiki iwapo amefariki ama la, iwapo amefunga ndoa na mtu mwengine ama iwapo pana uwezekano wa mapatano.

Katika hali kama hii, sawa na hali zilizojadiliwa, kila juhudi ya kufanya mapatano sharti ijaribiwe. Ningependekeza kuwa jambo *muhimu* kwa Mkristo aliyekimbiwa ni kujaribu kufuata utaratibu wa kisheria uliopo kuhusu hatua ya kuchukuliwa kama aliyefariki mtu aliyetoweka kwa miaka kadhaa. Mara mtu kama huyo anapochukuliwa kisheria kama aliyekufa, ndoa yake na yule aliyeachwa inaweza kubatilishwa iwapo mwenzake atatamani kufanya hivyo.

## Hatua Nyingine za Kufikiriwa

Watu wengine wangeonelea kuwa maagizo yaliyotolewa katika sura hii ni makali mno na yanawaachia mzigo mzito waliotalikiwa ama kuachwa. Inawezekana kuwa Mkristo aliyetalikiwa ama kuachwa hawezi kufunga ndoa tena kwa miaka kadhaa ama hata katika maisha yake. Hali hii ni yenye majaribu na ni ngumu mno kwa watu wengi, ingawaje haiwezi kumshinda Mungu kumpa anayehusika nguvu, uwezo na kumtia moyo wa kuvumilia. "Mungu ni mwenye uaminifu

na hatawaacha mjaribiwe kuliko kiasi cha uwezo wenu; lakini pamoja na hayo majaribu, Mungu atawapa njia ya kuyaepukia ili mkaweze kuyastahimili" (1 Wakorintho 10:13).

Panaweza kuwepo na majaribu makubwa kwa mtu kutamani kufunga ndoa tena licha ya mafunzo ya neno takatifu na kuwa na matumaini kwamba Mungu atamsamehe. Bila shaka, Mungu husamehe katika hali kama hizo, lakini tunapoteza baraka nyingi kutoka kwa Mungu tunapotenda mambo kulingana na mapenzi yetu yaliyo kinyume cha Neno la Mungu. Kwa wale wanaofikiria kuwa majaribu na mzigo wao ni mgumu na wa kipekee, wanapaswa kufikiria hali nyinginezo za misiba, baadhi mbaya sana kuliko talaka au kuachwa na ambayo husababisha kumalizika kwa uhusiano wa ndoa na pia kufanya uwezekano wa kufunga ndoa tena kuwa jambo gumu. Kuna watu waliooana ambao wenzao wa ndoa wamekuwa katika hali ya kukosa fahamu ama wasiojisikia kimwili kwa miaka mingi kutokana na kufa ganzi, mshituko wa moyo ama ajali; na wengine ambao wenzao wa ndoa ni mateka wa vita katika nchi za kigeni; na pia wale ambao wamekuwa wagonjwa wa akili na kulazimika kutumia sehemu kubwa ya maisha yao katika kituo cha matibabu.

Maelezo haya yanatuelekeza kwenye hoja nyingine muhimu. Ni nini jukumu la Wakristo kwa wenzao ambao ni wenye shida kama hizi? Lazima tutambue kuwa watu ambao wametalikiwa ama kuachwa—kama wale ambao wenzao wamefariki—watakuwa na mahitaji mengi, kama vitu, haja za kihisia na kiroho pia. Na ni lazima tuwe tayari kujitolea kama watu binafsi ama makanisa, kuwasaidia watu ambao ni sehemu ya mwili wa Kristo walio katika dhiki. Mke ambaye ni mama aliyetalikiwa au kuachwa na mumewe anaweza kuhitaji msaada wa kumlea mwanawe ili kupata wasaa wa kutoka nje na kufanya kazi kuikimu jamii yake. Na kwa siku kadhaa za mwanzo huenda akahitaji msaada wa kifedha kulipia madeni yake. Zaidi ya hayo, mume au mke aliye pekee atahisi upweke na atakaribisha sana mazungumzo kwa simu, kutembelewa na wageni ama kupelekewa barua na kujumuishwa katika shughuli za kijamii. Mtu kama huyo huenda akawa na makiwa na kujisikitikia na kwa hivyo akahitaji kutumikiwa kwa ushauri wa kiroho na Wakristo wenzake waliojawa na huruma na fahamu.

Kwa kumalizia, ni jambo la kutia moyo sana siku hizi kumwona mtu ambaye anaamini ukweli kuwa Mungu huchukia talaka na hupenda mapatano, na ambaye yuko radhi kuachilia mbali talaka, ama kukaa bila kuoa tena iwapo amekuwa katia talaka tayari, huku

akizidi kuomba na kutumainia kupatana na mkewe au mumewe. Mtu kama huyo atabarikiwa sana na Mungu na anastahili msaada wowote wa mali, kihisia ama kiroho ambao tunaweza kumpa.

# 7

# *Talaka na Kuoana Tena: Nidhamu Katika Ushirika na Kurudia Ushirika*

Miongozo ya kibiblia kuhusu talaka na kufunga ndoa tena imetolewa katika sura mbili zilizopita. Ilielezwa mwishoni kwamba kunayo idhini ya kibiblia ya kutoa talaka na kufunga ndoa tena, lakini idhini hii inakubalika tu katika hali ngumu na za kipekee. Hebu sasa tuseme Mkristo amekosa kuyafuata maagizo haya; hebu tuseme talaka na ndoa ya pili vimefanyika, ambayo sio kulingana na Neno la Mungu, na tuseme kiwango hiki cha kuzini ni kikubwa sana hata kiasi cha kumfanya Mkristo huyo kufukuzwa kutoka ushirika wa kanisa lake. Mtu kama huyo anapaswa kufanya nini pale ambapo dhambi imegundulikana na kutubiwa? Na ni nini jukumu la kanisa kwa mtu kama huyo?

Kabla ya kuingilia mambo halisi kuhusu hali kama hii, ingetufaidi kwanza kuangalia baadhi ya mafunzo muhimu juu ya kurudishwa katika ushirika kwa muumini aliyepotoshwa na dhambi. Mwandishi mwengine, akijadili kuhusu nidhamu dhidi ya mtu mwovu, ameandika yafuatayo: "Shukrani ziwe kwa Mungu, ana jambo la kupendeza, kwani baada ya kuzingatia huduma kwa uaminifu [kanisani] pana furaha ya kumwona mwenye dhambi akirudishwa katika ushirika. Tunaweza hata kuhisi furaha ya mtume Paulo alipokuwa akiandika kuhusu kurudishwa katika ushirika kwa Mkristo, 'Nimejawa na kutosheka, ninayo furaha ajabu katika shida zetu zote' (2 Wakorintho 7:4).

"Kuponywa ndilo jambo lililoombewa, lililotumainiwa na lililotegemewa. Ijapokuwa yule aliyefukuzwa kutoka kanisani ni heri aachwe peke yake, hii haina maana kwamba mtu kama huyo hafai kuombewa, au kumtumikia baada ya muda fulani kupita. Jambo hili ni heri lifanywe hasa ikiwa anayehusika ni Mkristo mwenye imani dhaifu ama ambaye hakufunzwa sana mambo ya dini, na iwapo

amekubali adhabu au hukumu ya Mungu kwa matendo yake. Lakini wale wanaojifanya wajasiri ama wanaoendelea katika maisha ya dhambi, wanaweza tu kuachwa mikononi mwake Mungu.

"Alama za kupona kwa kweli ni dhahiri. patakuwa na fikira za kumkosea Mungu (Zaburi 51), kuhukumu chanzo cha dhambi yenyewe, kukiri hukumu ya Mungu ingawa adhabu kali zaidi inaweza kupendelewa na Kanisa; hizi ni baadhi ya dalili za kupona kwa kweli. Iwapo kulikuwa na makosa dhidi ya mtu yeyote, makosa hayo yatasahihishwa kama iwezekanavyo—pato la wizi litarudishwa, mashitaka makali ya uwongo yataondolewa; na pia hatuna haja ya kuongezea, dhambi yenyewe itafutwa. Mpaka mkosaji amrudie Mungu kwa moyo wote, hawezi kurudishwa katika ushirika wa kanisa. Hatua zinazohusu kurudishwa katika jamii kwa mtu mwenye ukoma ambaye amesafishwa (Walawi 14) zinapendeza na zina mafunzo tele kuhusu swala hili. Ni kuhani tu ndiye aliye kuwa na uwezo wa kumchunguza mgonjwa huyo aliyekuwa ameponywa ukoma na miko iliyohusu kurudishwa kwake katika jamii ilisisitiza kupona kwa mgonjwa kama huyo kikamilifu.

"Itakumbukwa kwamba mwenye kuponywa ukoma, hata baada ya kurudishwa katika ushirika wa ibada ya Mungu, 'alibakia mbali na hema lake kwa siku saba'; inaonyesha kuwa hata baada ya kuponywa nafsi yake kabisa, bado panaweza kupita muda kadhaa kabla ya mtu kurudishwa kwenye ushirika wa kanisa. Kuna sababu nyingi za jambo hili: kama kosa lilikuwa dhahiri au baya mno, ni bora kwa watu wote kudhibitisha ukweli wa kutubu kwa mkosaji. Hali kama hii haitamdhuru mkosaji bali itamfanya kuhisi uzito wa dhambi aliyotenda. Zaidi ya hivyo, ni heri kukumbuka kuwa mioyo ya waumini wengine imechomwa sana na dhambi ya anayehusika na inahitaji muda wa kupona kutokana na madhara hayo. Dalili za kutaka kurudishwa mara moja baada ya kutubu ama kuchukia kukawishwa, zitaonyesha kuwa kazi ya kutubu katika moyo wa mkosaji haijakamilika.

"Kwa upande mwingine, kanisa lazima lijihadhari na moyo mgumu usiosamehe. Mioyo ya wote itakaporidhika, hapatakuwa na haja ya kukawia kumpa idhini ya kukubalika ndugu Mkristo aliyeponywa. 'Adhabu hii ambayo mkosaji ameipokea kutoka kwa watu walio wengi inamtosha. Kwa hivyo inafaa kumsamehe…ili mtu kama huyo asije akadidimia katika huzuni kuu. Kwa hivyo nawasihi kusisitiza upendo wenu kwa mtu kama huyo' (2 Wakorintho 2:6-8). Maagizo haya yamejaa wingi wa neema, upendo na utakatifu wa ajabu!

"Je hatuwezi kuongezea kwamba yule ndugu anaporudishwa

katika mahali pake pa ushirika dhambi aliyoitenda isikumbukwe kamwe? Kweli hataisahau *yeye* binafsi; lakini wale wengine watajizuia kuonyesha katika tabia zao na mitazamo yao kuwa wanaukumbuka ule uovu? Naam! tumefanana sana na walimwengu wengine ambao 'husamehe lakini hawasahau.' Wala hatuwezi kusema kuwa mtu kama huyo anyamaze kabisa na asijitolee tena ili Mungu aweze kumtumia. Kwa hakika, ni mtume Petro, kondoo aliyekuwa akitangatanga ambaye alifanywa mchungaji wa kondoo wengine (Yohana 21:15,17). Wakati mfalme Daudi aliposamehewa, alianza kuwafunza watu dhidi ya kutofuata njia zake Mungu (Zaburi 23:3)." (Kutoka katika *The Church and Its Order According to Scripture* by S. Ridout, Loizeaux Brothers, Neptune, NJ 07753.)

Dalili moja ya kupona kabisa kwa Mkristo mtenda dhambi aliyoitaja Bwana Ridout ni kuiacha ile dhambi. Hii ni sehemu yenye ugumu sana katika kutekeleza maagizo makuu ya dini juu ya talaka na kufunga ndoa tena. Baadhi ya watu huchukulia kwamba mtu ambaye ametalikiwa kulingana na mafunzo ya Neno la Mungu na akaoa tena, yuwaishi katika maisha ya kiuasherati muradi ndoa yake mpya bado ipo; muradi dhambi ya uasherati haijaachwa, mtu kama huyo—ijapokuwa anaweza kuwa ametubu na kumrudia Mungu moyoni mwake—hawezi kurudishwa katika ushirika wa Wakristo wengine.

Katika sehemu iliyobakia ya sura hii, tutajadili hoja hii kwa maoni mbalimbali kuhusu mtu ambaye ametaliki na kuoa tena bila kufuata mafunzo ya Neno la Mungu, ambaye ametubu dhambi zake na angependa kurudishwa katika ushirika wa Wakristo wengine. Masuluhisho matatu ya kwanza yanahusu matendo ama matukio ambayo yanaweza kufasiriwa kumaanisha kuwa mkosaji ameiacha dhambi ya uasherati; suluhisho la nne ni kitendo cha kiroho ambacho kinaweza kuchukuliwa kuwa ushahidi wa kuiacha dhambi hiyo:

1. Kuishi bila kufunga ndoa kwa kuzingatia ndoa aliyo nayo mtu kwa sasa.

2. Kuimaliza ndoa aliyona mtu kwa sasa.

3. Kuendelea kuishi katika ndoa ya sasa huku mtu akiwa ametengwa na kanisa hadi mwenzake wa ndoa atakapofariki.

4. Kuiungama dhambi na kumtolea Mungu ushahidi wa kututbu kikweli na kurudishwa katika ushirika.

*Suluhisho 1. Kuishi bila kufunga ndoa kwa kuzingatia ndoa ya sasa.* Hili ni suluhisho linalotolewa na dhehebu moja kubwa la Kikristo siku hizi, yaani kuwasihi mume na mke ambao wametalikiana na

kufunga ndoa tena kuweka nadhiri ya kuishi bila kufunga ndoa tena maishani mwao. Naamini kuwa Neno la Mungu linapinga jambo hili. (1 Wakorintho 7:5 inaeleza waziwazi kuwa: "Msinyimane wenyewe kwa wenyewe isipokuwa kwa makubaliano kwa muda mfupi, ambapo mmejitokea kufunga na kuomba; *na mrudiane tena,* Shetani asije akawajaribu kwa kujizuia kwenu." Suluhisho hili halifai pia kwa vile linawalazimisha waliooana kubeba mzigo mzito na kuifanya ndoa kuwa kitu kigumu.

*Suluhisho 2. Kuimaliza ndoa ya sasa.* Njia hii inaweza kuwaridhisha wale wanaosisitiza mkosaji aiache dhambi ya uasherati kabla ya kukubaliwa tena katika ushirika. Hata hivyo, tunahitaji kuchunguza iwapo kuna sababu yoyote katika Neno la Mungu ya kuimaliza ndoa iliyopo sasa katika hali kama hiyo.

Ninajua kifungu kimoja tu katika Biblia (Ezra 9 na 10) ambacho kinahimiza kuvunjwa kwa ndoa zilizo kinyume cha sheria ama zinazoasi amri ya Mungu. Wakati wana wa Israeli waliobakia waliporudi kwao kutoka Babeli ambako waliishi kama watumwa, walioa wake kutoka kaika makabila yaliyowazunguka (Wakanani, Wamoabu, Wamisri, n.k.). Lakini walipogundua kuwa jambo hili lilikuwa kosa na halikuambatana na sheria ya Mungu (Kutoka 34:10-17), walifanya mkataba na Mungu, chini ya uongozi wa Ezra, kuwaacha wake zao wageni na kizazi kilichotokana na ndoa hizo (Ezra 10:3-11)

Kwa Wakristo, kuna sheria kama hiyo kuhusu kufunga ndoa na wageni: "Ikiwa mume wake amekufa, mwanamke yu huru kufunga ndoa na yeyote ampendaye; lakini katika Mungu" (1 Wakorintho 7:39).* Lakini itakuwaje iwapo sheria hii itavunjwa? Ni jambo gani linalofaa kufanyika iwapo Mkristo ataoana na mtu asiyekuwa Mkristo au mtu ambaye tayari amefunga ndoa akiokoka na mwenzake akose kuokoka? Mfano wa Ezra unafaa kufuatwa? La, lakini hasa jawabu kwa watu wanaoishi katika enzi ya neema kulingana na Agano Jipya limeelezwa vyema katika 1 Wakorintho 7:12-14: "Ikiwa Mkristo yeyote ana mke ambaye si Mkristo, na ambaye angependa kuishi naye, basi asimwache mke huyo…. Kwa sababu mke ambaye haamini Neno la Mungu ametakaswa na mumewe."

Kwa kweli ni dhambi kwa Mkristo kufunga ndoa na mtu asiyekuwa Mkristo. Lakini iwapo ndoa kama hiyo imefanyika, hapana sababu yotote katika maandishi matakatifu ya kuivunja ndoa ili kuonyesha ushahidi kuwa mkosaji ameiacha dhambi hiyo. Kuhusu dhambi ya aina nyingine—yaani kuoana na kupeana talaka bila kuzingatia Neno la Mungu, hapana maagizo yoyote katika

Neno la Mungu kuhusu kuvunjwa au kutovunjwa kwa ndoa kama hiyo. Hata hivyo, mafunzo yaliyotolewa kuhusu hali kama hii—yaani, "Asimwache mke wake…mke asimwache mumewe"—yanaweza pia kuhusu hali ya kupeana talaka na kufanya ndoa tena.

Mafundisho ya mtume Paulo katika 1 Wakorintho 7:12-14 yamesisitizwa na kupanuliwa katika vifungu 18-24: "Kuna mtu ambaye ameokolewa akiwa ametahiriwa? asigeuke tena kuwa kama ambaye hajatahiriwa…. Kila mtu na abakie katika hali aliyokuwa pale alipookoka…na akiwa hivyo aishi katika Mungu." Ninaamini katika majadiliano yote katika sura hii, maneno haya yanamaana kuwa ikiwa mtu amehusika katika talaka na ndoa nyingi bila kufuata Neno la Mungu kabla ya kuokolewa, mtu kama huyo si lazima kubadilisha hali yake kwa kuivunja ndoa aliyo nayo kwa sasa ili kujaribu kusafisha maisha yake yaliyopita. Lakini, je, si mafunzo pia yanamhusu Mkristo ambaye amepotea njia na kumwacha Mungu, ambaye ameonyesha tabia ya kuishi kama mtu asiyekuwa Mkristo kwa muda fulani, na ambaye ametaliki na kuoa tena katika muda huo? Wakati mtu kama huyo anapoisikia sauti—wito wa Bwana—na anapoponywa tena katika nafsi na moyo wake, "anapaswa kuishi katika hali aliyokuwa nayo alipookolewa."

Kwa hivyo, inaonyesha hapana sababu katika Neno la Mungu ya kuivunja ndoa aliyo nayo mtu ili kuiepuka dhambi ya uasherati.

*Suluhisho 3. Kuendelea na ndoa ya sasa na kubakia nje ya kanisa mpaka mke au mume anapofariki.* Jawabu hili hufuatwa na baadhi ya makanisa ya Kikristo. Sababu ya kulifuata jawabu hili imo katika Warumi 7:3: "Iwapo mumewe bado anaishi, mke akiolewa na mwanamume mwengine, ataitwa mwaasherati; lakini ikiwa mumewe amefariki, mke yuko huru kutokana na sheria hii; kwa hivyo si mwaasherati kama akiolewa na mume mwingine." Inachukuliwa kuwa mtu ambaye ametaliki na kufunga ndoa tena bila kufuata Neno la Mungu mbele ya Mungu bado ameoana na mwenzake wa kwanza na anaendelea kuishi katika hali ya uasherati. Lakini iwapo mwenzake wa mwanzo amefariki, mkataba wa ndoa ya kwanza umevunjika na uhusiano huu wa pili hauwezi kuhesabiwa kuwa uasherati. Kwa hivyo mtu au watu kama hao wanaweza kurudishwa katika ushirika wa kanisa.

Kwa kiasi fulani, sababu za hoja hii zinaonekana kuwa ni za busara. Bali zinapochunguzwa kwa undani, haziambatani na mafunzo mengine ya Neno la Mungu. Kwa kawaida, kurudishwa katika ushirika baada ya kutengwa hutegemea kuungama, kutubu, na ushahidi ulio wazi kwa kumrudia Mungu na kumfuata tena. Lakini katika

hali inayojadiliwa hapa, kurudishwa katika ushirika kunategemea tukio maalumu—kifo cha mke au mume wa kwanza—jambo ambalo limo nje ya uwezo wa mtu au watu waliyetengwa kutoka kanisani. Je, inawezekana kwamba kifo cha mtu mwengine—na hicho pekee—kinaweza kuwa uhusiano moja kwa moja na kuponywa kwangu na kumrudia Bwana? Je kumrudia Mungu kwa Mfalme Daudi kuliathiriwa na kuuawa vitani kwa mume wa mke ambaye Daudi alikuwa amemwiba, ili kwamba Daudi hakuendelea kuishi katika uasherati? Hakuponywa kwa sababu ya kutubu moyoni mwake kikweli mbele za Mungu? Fikiria kutubu kwake katika Zaburi: "Nisafishe kabisa kutokana na uovu wangu na uniponye kabisa dhambi yangu. Kwani nakiri kabisa makosa yangu; na dhambi yangu daima i mbele yangu. Dhidi yako, wewe pekee nimetenda dhambi na kufanya uovu huu mbele zako…. Nirudishie furaha ya wokovu wako…. Sadaka ya Mungu ni roho yenye unyenyekevu na moyo mkunjufu, ewe Mungu hutapuuza" (Zaburi 51: 2,3,12,17). "Nimekiri dhambi yangu kwako na uovu wangu sikuuficha. Nillisema nitatubu makosa yangu kwa Bwana, Nawe unasamehe uovu wa dhambi yangu" (Zaburi 32:5).

Kuna jambo lingine linalotaabisha kuhusu suluhisho hili; linaweza kulifanya kanisa kukosa kutenda kwa njia sawa sawa kama ilivyoonyeshwa katika mfano unaofuata: Mtu anayemuua mwenzake wa ndoa na kuoa tena baada ya kuachiliwa kutoka jela ana nafasi kubwa ya kurudishwa katika ushirika kuliko mtu anayemtaliki tu mwenzake na kufanya ndoa na mtu mwengine. Basi wale wanaopendekeza suluhisho la kuendelea kumtenga mtu anayetaliki na kufanya ndoa tena hadi mwenzake wa ndoa ya kwanza afe, wanapaswa kuchunguza upya suluhisho hilo kwa mjibu wa maandishi yote matakatifu.

*Suluhisho 4. Kutubu dhambi na ku onyesha ushahidi wa kutubu kwa kikweli na kumrudia bwana.* Hoja hii, ninaamini, inaeleza maoni ya Neno la Mungu kuhusu masharti ambayo kanisa linapaswa kumwekea mtu ambaye ametaliki na kufunga ndoa tena kinyume cha Neno la Mungu. Ni kweli kuwa kulingana na suluhisho hili hapana haja ya ushahidi wa kuiacha dhambi kimwili na kufunga ndoa tena. Hata hivyo, kama vile Daudi alivyorudishwa kwa Bwana baada ya dhambi yake kuu ya uasherati na mauaji, hivyo, naamini, inawezekana kwa mtu yeyote ambaye ametenda dhambi mbaya hapo awali kwa kutaliki na kufunga ndoa tena, au kuua, ama dhambi ya aina yoyote ile, kutubu kikweli ile dhambi na kurudishwa katika Bwana.

Mkristo anapoana na mtu asiyekuwa Mkristo au kutaliki na kufunga ndoa tena kinyume cha neneo la Mungu, dhambi kubwa

hapa ni ile ya kufuata mapenzi ya moyo wake, kutenda ninavyopenda *Mimi* badala ya vile *Mungu* anavyopenda. Fikira za kuwa mwenye kosa zinamwandama anayehusika daima, muradi anazidi kuikana ile dhambi, kutoa vijisababu au maelezo. Lakini mkosaji anapoacha kukana huku ama vijisababu vya kutenda dhambi ile na kutubu kwa Mungu na watu wengine kwamba amtenda uovu na kufanya dhambi dhidi ya Mungu na binadamu, anasamehewa na anaelekea kumrudia Mungu. "Tukitubu dhambi zetu, Mungu ni mwaminifu na mwenye haki wa kuweza kutusamehe dhambi zetu, na kutusafisha kutokana na uovu wa aina yoyote" (1 Yohana 1:9). Kama vile moto au joto linavyo-komesha kukua kwa uyoga katika unga wa kukandia mkate, vivyo hivyo ndivyo kujihukumu binafsi na kutubu kwa kweli mbele za Mungu kunavyokomesha vitendo vya dhambi maishani mwetu (1 Wakorintho 5).

Wengine wanaweza kudai kuwa kutubu kwa mtu na kumrudia Mungu katika nafsi na moyoni hakumaanishi kwamba anaweza kurudishwa katika ushirika wa kanisa. Hata hivyo, uhusiano kama huo unamweka mtumishi juu ya Bwana wake (Yohana 13:16) na mwili (Kanisa) juu ya Kichwa (Kristo); na unalipa Kanisa kiwango cha juu cha usafi, utakatifu na wema kuliko Kristo.

Baada ya kusema haya, maelezo machache yanafaa kutolewa: La kwanza ni kwamba kwa vile kuiacha dhambi ya kimwili (kama vile talaka na kuimaliza ndoa) hakuruhusiwi na Neno la Mungu, aina nyingine ya ushahidi wa kuponywa kwa kweli na kumrudia Mungu inaweza kuhitajiwa na kanisa kabla ya kumkubali tena mwenye dhambi aliyetubu. Hivi ni kusema kuwa kanisa lina haki ya kuhitaji muda mrefu katika hali hii ili kuhakikisha kwamba pamekuwa na kuponywa kwa kweli na kwamba mtu aliyetenda dhambi sasa anamfuata Mungu na kutenda mapenzi yake. Pia, talaka inaweza kuwa imemdhuru mhusika kwa kumvunja moyoni na kumpa fikira zenye uchungu. Madhara haya yanahitaji muda kupona. Iwapo aliyepewa talaka na familia yake ni wanakanisa, wanaweza kutopendelea kurudishwa katika ushirika kwa yule aliyetoa talaka. Muda zaidi wa neema ya Mungu unahitajika kuponya mioyo ya wale waliodhurika na kuhakikisha kabisa kuwa mwenye kutoa talaka ametubu kikweli na kumrudia Bwana.

Sharti la pili ni kwamba ijapokuwa Mungu ni mwenye neema katika kumrudisha mwenye kutubu kwake, na ijapokuwa mkosaji aliyetubu anaweza kurudishwa katika kanisa, hapana hakika kuwa mkosaji atazuiliwa asiadhibike kutokana na matokeo ya dhambi yake. "Msidanganyike; Mungu hachezewi; kwani chochote mtu

anachopanda, ndicho atakachovuna" (Wagalatia 6:7). Daudi alisamehewa dhambi yake na Mungu, lakini pia, alivuna matokeo ya dhambi yake katika maisha yake yote—kwanza kwa kifo cha mwanawe mchanga, na baadaye kwa kupata matatizo mengi katika kuwalea watoto wake.

Kwa kumalizia, tunaweza kusema, kufanya talaka na kufunga ndoa tena bila kuzingatia mafunzo ya Neno la Mungu, kunaleta uhusiano wa kiuasherati amabao ni lazima kukabilianwa nao na kanisa ambalo mhusika anahusiana nalo. Hata hivyo, kwa neema ya Mungu, ambayo bila kuwa nayo hakuna kati yetu awezaye kupata msamaha wa dhambi, haki na amani pamoja na Mungu, mkosaji anaweza kurudishwa katika ushirika wa Mungu na, kama matokeo ya hayo, katika ushirika wa watu wa Mungu. Kurudishwa huku kunategemea kuungama kimoyoni kwa kweli na kutubu kwa Mungu, na kunadhihirishwa na kanisa na kumfuata Mungu kwa imani na kutii Neno lake.

Hoja hii inatufikisha mwisho wa mafunzo yetu kuhusu Mkristo na ndoa. Sura tatu za mwisho zimejadili tatizo la kuhuzunisha la talaka na kufunga ndoa tena; pamekuwa na haja ya kulijadili jambo hili kwa undani kutokana na tabia ya Wakristo wa sasa ya kuyaacha mafunzo ya Neno la Mungu na njia yake. Hata hivyo, tusisahau hoja zilizojadiliwa hapo mwanzo kuhusu uchaguaji wa mchumba wa ndoa, kujiandaa kwa ajili ya ndoa na mambo muhimu katika kuhakikisha ndoa ya furaha. Kwa maoni yangu, hizi ndizo sura muhimu zaidi katika kitabu hiki. Iwapo mafunzo ya Neno la Mungu kuhusu mambo haya yatafuatwa kikweli, hapatakuwa na haja kubwa ya kujadili maswala yanayohusu talaka na kufunga ndoa tena.

## Nyongeza 1

# *Kabla Hujafunga Ndoa*

Ndoa ni mkataba wa kudumu (Mwanzo 2:24; Mathayo 19:5,6). Haipaswi kuingiliwa kwa pupa au bila kufikiria kwa makini. Vifungu vifuatavyo kutoka katika maandishi mbalimbali vinatoa maoni tofauti kutoka katika Neno la Mungu na katika maisha ya watu ambayo yanaweza kuwasaidia wachumba katika kuelewa kama Mungu angependa waoane, na kama ni hivyo, ni ipi njia nzuri ya kujitayarisha kwa ndoa. Mambo kadhaa yanayoonyesha tofauti kati ya wachumba, ishara za kutahadharisha, mambo yanayoweza kuleta

matatizo, na maswali ya kuulizana yametolewa kwa ajili ya wachumba wanaofikiria kuoana.

* * *

Jambo moja muhimu zaidi la kufikiria wakati mtu anapotazamia kufunga ndoa ni kuelewa wajibu wa mume na mke. Ni nani katika uhusiano wa ndoa atakayekuwa na jukumu gani. Wote wawili ni lazima wayaelewe mafunzo kuhusu uhusiano wa ndoa yaliyotolewa katika Nyaraka za mitume (Waefeso 5:22-33; Wakolosai 3:18,19; 1 Petro 3:1-7) na sharti wakubali kuishi kwa kuzingatia mafunzo haya.

* * *

Jambo ambalo mara kwa mara halizingatiwi sana ni kuhusu uhusiano na wakwe. Vijana wengi wamedai kuwa, "Sitaoa familia yao; nitamuoa mwanamke tu." Lakini katika kumuoa mwanamke, mwanamume, kwa njia nyingine anaoa familia ya mkewe, kwani mke anaingia katika maisha ya ndoa na mambo chungu nzima yanayohusu msingi wa jamii yake. Na mume pia, hali kadhalika, ni vivyo hivyo. Ikiwa katika familia ya mke jamii nzima hukutanika kwenye nyumba ya nyanyake kila jumapili alasiri, basi si rahisi kamwe kwa mke kuibadilisha tabia hii. Ikiwa mwanamke huyu angependa kuolewa na mwanamume ambaye anatoka katika familia ambapo kila mtu hubakia nyumbani jumapili alasiri akisoma gazeti, kupumzika au kufanya jambo lolote, basi, sharti uamuzi ufanyike kati ya mume na mke. Lingekuwa jambo bora mno kama uamuzi huo ungefikiwa kabla ya ndoa ili kuepuka mgogoro amabo ungeadhiri hisia zao katika siku za mwanzo mwanzo za ndoa yao.

* * *

Swala lingine ambalo linapaswa kujadiliwa kabla ya kufunga ndoa linahusu kumtumikia Bwana. Kufikia wakati ambapo vijana wanafikia "umuri wa kufunga ndoa" wengi wao wamejitolea kwa Mungu kuhusu maisha yao ya baadae. Haya yanaweza kuwa ni kufanya kazi katika nchi za ng'ambo kama wamishonari wa aina mbalimbali, ama kufanya kazi ya Bwana karibu na nyumbani. Haitoshi tu kwa mtu binafsi kujitolea kumtumikia Kristo. Katika ndoa, watu wawili huwa mmoja na huyo "mmoja" aliyeumbika lazima awe huru kufuata maongozi ya Mungu. Ni bora kwa wachumba wote wawili kujua kuwa wanafuata njia moja katika kumtumikia Bwana kabla ya ndoa kuliko kuchukulia hivyo na baadaye kuja kugundua kwamba walikuwa na shabaha tofauti katika mawazo yao.

(Vifungu vilivyotangulia vimetolewa katika "Before the 'I Do'" na Jan Reeser; vimechapishwa kwa idhini kutoka *Good News Broadcaster*,

chapisho la mwaka wa 1976 kwa idhini ya The Good News Broadcasting Association, Inc., Lincoln, NE.)

* * *

Hebu zingatia mambo ambayo mtumishi wa Ibrahimu aliyafauata katika kumchagua msichana ambaye angeolewa na Isaka: "Na msichana akasema, Kunywa, Bwana wangu; na akasita, akatoa bilauri mkononi mwake na kumpa maji. Na alipomaliza kumpa maji ya kunywa, akasema, nitachotea ngamia wako maji pia, hadi watosheke na maji. Na akasita…na kuwachotea ngamia wake wote maji" (Mwanzo 24:18-20). Huyu ni msichana mdogo ambaye, naamini, alizaliwa katika familia tajiri, lakini alikuwa na moyo wa mtumishi. Ruthu pia, alikuwa na moyo wa mtumishi. Kifungu cha Ruthu 2 kinaeleza jinsi Ruthu alivyofanya kazi siku kutwa mashambani, na aliporudi nyumbani siku ile, alipata wasaa wa kusaga nafaka. Mwanamume au mwanamke Mkristo anayetaka kufunga ndoa anapaswa kumtafuta mtu mwenye msimamo mathubuti kama huyu na pia aliye mkarimu, ambaye yuko tayari kujitolea kuwatumikia wengine.

* * *

Ni muhimu pia kuona jinsi kila mmoja anavyowatendea wazazi wake. Wasichana, huyo mwanamume anamtendea mamake vipi? Nimeona mara nyingi kwamba mwanamume aliye mkatili kwa mama yake, atamtendea mkewe vivyo hivyo. Wanaume wenzangu, huyo mwanamke anachukuliaje maagizo ya wazazi wake? Nimewaeleza wavulana wengi jinsi wanawake wanaotegemea kuwaoa wanavyokaidi mamalaka ya baba na mama zao na kufanya watakavyo. Ninaweza kumwambia mvulana kama huyo kuwa mkewe atamtendea vile vile wakati wa fungate utakapokwisha.

(Vifungu hivi viwili vilivyotangulia vimetolewa katika, "Selecting Your Life Partiner" cha Curtis Lehman; kilichochapishwa tena kwa idhini na *Good News Broadcaster*, kwa ruhusa chapisho la mwaka wa 1979 kwa idhini ya The Good News Broadcaster Association, Inc., Lincoln, NE.)

* * *

Maisha ya ndoa yanahitaji uthabiti. Kwa hivyo, wachumba wanapaswa kutafakari kwa makini kabla ya kufanya mkataba. Uchunguzi ufaao unapaswa kufanywa kwa kila mhusika hasa kuhusu mambo kama vile shule, kazi, marafiki (wake kwa waume), kanisa, jamaa wa familia, mategemeo ya siku za baadaye na kujitolea kiroho kwa upande wa dini. Uliza maswali kama haya: Anafikiria kufanya kazi za aina fulani ama hubadilisha nia kila mara? Anadumu na

marafiki wa Kikristo kwa miaka kadhaa? Anapatana vizuri kila mara na wazazi wake? Majibu ya maswali haya yatakufahamisha kama ni mtu mwenye tabia thabiti au anayeyumbayumba.

* * *

Ndoa ni ushirika. Zaidi ya kupendana, wachumba wanaotazamia kuoana, ni lazima wawe wanavutiana—yaani kila mmoja anavutiwa na mwenzake. Lazima wahakikishe kuwa watakuwa wenye furaha katika kuishi pamoja maishani mwao. Ninawahakikishia kwamba kuna mvuto wa mapenzi ya kimwili. Lakini, katika ndoa, wakati mwingi hutumika katika "kushirikiana" —kwenda mahali tofauti pamoja, kufanya mambo pamoja, kusafisha vyombo pamoja, kuzungumza pamoja, kuwafundisha na kuwatunza watoto pamoja—yaani wakiwa washirika na marafiki.

(Vifungu viwili hivi vimetolewa kutoka *Young Only Once* cha Clyde M. Narramore, idhini ya mwaka 1963 ya Zondervan Publishing House, Grand Rapids, MI; vimetumiwa hapa kwa idhini.)

* * *

Utafiti kuhusu ndoa zenye furaha na zinazoridhisha umeonyesha kuwa mume au mke anayechaguliwa mara nyingi atakuwa:

1. Mtu ambaye unafurahia kuwa na urafiki naye.
2. Mtu ambaye amekomaa na asiyekuwa na fikira au mitazamo ya kitoto.
3. Mtu ambaye unaheshimu tabia na utu wake.
4. Mtu anayejiheshimu na kuwaheshimu watu wengine na hivyo, kukuheshimu wewe.
5. Mtu anayekuhimiza kutenda mema na kukusaidia kukua kimaisha.
6. Mtu aliye na mtazamo mwema wa kimaisha na aliye mchangamfu.
7. Mtu ambaye malezi yake ya kijamii na kitamaduni ni kama yako.
8. Mtu ambaye marafiki zake ni namna ya marafiki unaowathamini.
9. Mtu ambaye imani yake ya kidini ni karibu sana na yako na hivyo hapatakuwepo na kutopatana kuhusu ushirika wa kanisa.
10. Mtu ambaye kiwango chake cha maisha utakikubali bila shida.
11. Mtu kiwango chake cha elimu na mantiki kinakaribiana sana na chako ili kuhakikisha furaha ya ushirika katika mambo mnayoyafanya na kuyafikiria pamoja.
12. Mtu ambaye, ikiwezekana, ambaye amepata radhi ya baba na

mama yako. Wazazi mara nyingi wanayaelewa mambo kwa undani zaidi na hukutakia mema kila mara.

13. La muhimu zaidi, ni kuwa mtu akufaaye ni yule aliyejitolea kwa Kristo na kujitolea kiroho kama wewe. Yaani, Mkristo afaaye kwako ni yule "anayefuata njia yako" na Kristo—mtu anayekuhimiza kukua katika Bwana.

Ndoa ni uhusiano mgumu sana. Wakati watu wawili wanapojitolea kuishi pamoja, jinsi walivyo na mambo mengi yanayofanana ndivyo watakavyoweza kuishi bila kufarakana. Ni kweli kuwa tunajua ndoa nyingi ambazo zinaendelea vyema ingawa mume na mke wana misingi tofauti na wanapendelea mambo tofauti. Ndoa kama hizo, hata hivyo hazitokei kila mara.

(Vifungu hivi vimetolewa kutoka "Choosing the Right One to Love" cha Clyde na Ruth Narramore; vimechapishwa kwa idhini kutoka *Psychology for Living* idhini ya mwaka 1983 na Narramore Christian Foundation, Rosemead, CA.)

* * *

Maswali ambayo wachumba ambao hawajaposana wanapaswa kujiuliza:

1. Nyinyi wawili mnalingana katika mambo ya kiroho?
2. Misingi ya jamii zenu inalingana kiutamaduni? kimila? kiuchumi? kielimu na viwango vya kijamii?
3. Mnapatana kuhusu kazi mlizozichagua?
4. Mnapatana kuhusu uadilifu?
5. Mnayasikiza mafunzo ya wazazi wenu?
6. Mnayo mapendeleo yanayofanana kuhusu mambo ya kujistarehesha? kujifurahisha? marafiki?
7. Mnavutiwa na maumbile ya kila mmoja? uchangamfu? mwelekeo wa kimaisha? hali ya ufanisi? utu? hisia? tabia za kupendelea usafi?

Ikiwa majibu yako ya "hapana" ni mengi kuliko ya "ndio" kuhusu maswali hayo, unaweza kuvumilia tofauti hizo katika maisha ya kuishi pamoja?

* * *

Mambo kadhaa ya kufikiria kwa makini na kwa maombi wakati wa posa:

1. Nyote wawili mnao ujuzi ufaao wa Biblia?
2. Mnaweza kujadiliana bila shida imani zenu za kiroho?
3. Mnaomba kwa sauti mkiwa pamoja?
4. Mnajifunza Neno la Mungu pamoja?

5. Kunazo tofauti kubwa katika maoni yenu ya kidini?
6. Nyote wawili mnaona haja ya kuwahubiria waliopotea njia?
7. Mngependa kukuza vipawa vyenu kama ilivyoelezwa katika Warumi 12?
8. Mnafurahia ushirika na Wakristo wengine?
9. Uhusiano wako na ndugu na dada zako, baba na mama yako uko vipi? Migogoro ilisuluhishwa vipi kwenu nyumbani?
10. Unapendelea kufanya kazi mchana ama usiku?
11. Unaweza kupatana na wazazi wa mwenzako bila mafarakano?
12. Ungeweza kumsegenya mwenzako kwa wazazi wako kuwa ana udhaifu fulani?
13. Mnakubaliana kuhusu mahali panapofaa kwa nyumba yenu ya kudumu?
14. Shabaha zako za siku za usoni na siku za baadaye ni zipi?
15. Matumizi yako (na uwekaji akiba) yako vipi?
16. Mnafanana kwa kutochelewa? kwa usafi?
17. Mnasuluhishaje ugomvi wenu?
18. Mnawekeana visasi?
19. Unaweza kumsamehe mtu mtakayeoana naye kwa makosa yake ya siku zilizopita?
20. Unamlaumu mtu yeyote kwa makosa yako?

* * *

Haikosi kwamba tofauti kadhaa zitatokea kwa upande wa utu, mielekeo, shabaha, n.k. kati ya mwanamume na mwanamke wanaotegemea kuoana. Ndoa yao haiwezi kuharibiwa na tofauti kama hizo pekee. Hata hivyo, watu walioposa wapaswa kufahamu kuwa ndoa inaweza kufanya tofauti kama hizo kuwa kubwa zaidi. Kwa hivyo, tofauti zinafaa kujadiliwa na kufahamika na hatua kuchukuliwa wakati wa kuposana kukubali hali yao halisi bila kulaumiana wala kufanyiana matakwa ya tamaa za kibinafsi. Msingi wa ufanisi katika ndoa ni kukubaliana kutofautiana bila ugomvi.

Baada ya mwaka mmoja tangu afunge ndoa, mke mmoja alisema, “Wakati wa posa niliogopa kumpoteza hivi kwamba ingawa niliona kasoro kadhaa ambazo nilizichukia katika tabia yake, sikusema chochote. Nilifikiri mambo yangekuwa shwari baada ya ndoa. Sasa lililobaki ni kupigana tu.” Lakini kwa nini kungoja hadi baada ya ndoa kabla ya kugundua kasoro? Kipindi cha kabla ya posa ni muhimu sana kushinda watu wengi wanavyotambua; na posa ni muhimu zaidi, kwani huwatayarisha wachumba kwa maisha ya ndoa Kwa vile ndoa yenye kufana hutegemea mawasiliano ya kila mara, wachumba

walioposana wapaswa kuzungumza, kuzungumza na kuzungumza.

(Vifungu hivi vimetolewa katika sehemu ya "Before You Marry, Ask These Questions" mwandishi ni Craig Massey, kimechapishwa katika *Moody Monthly*; vimetumiwa hapa kwa idhini.)

## Nyongeza 2

# *Watu Wafaao Kuoana*

Wataalamu wa Kiebrania hutueleza kwamba neno lile lile linalomaanisha "moja" limetumiwa katika Mwanzo 2:24, "Nao watakuwa mwili mmoja" na katika Torati 6:4, "Sikia, ewe Israeli: Bwana Mungu wetu ni Mungu mmoja." Hoja hii hutumiwa mara kwa mara kuonyesha kuwa hata katika Agano la Kale hali ya utatu wa Mungu—umoja wa zaidi ya sehemu moja—ilitajwa. Ningependa kuingalia hoja hii kwa mtazamo tofauti na kuonyesha maumbile halisi ya umoja kati ya mume na mke.

Nafsi za Utatu zimekuwa, bado zinaendelea na zitaendelea kutimiza shabaha moja daima dawamu. Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanaweza kuwa na kazi tofauti katika kutimiza shabaha hizi, lakini hapana ufarakano wa shabaha ama nia katika maumbile ya Mungu wa Utatu. Vile vile, watu wenye kufaa kuoana watakuwa na shabaha moja ijapokuwa wanaweza kuwa na njia tofauti za kutimizia shabaha hizo. Hapatakuwa na ufarakano wa nia kwani kwa Wakristo waliooana, kamwe hawatajiuliza, "Tutafuata mapenzi ya mume au ya mke katika jambo hili?" lakini watajiuliza, "Mapenzi ya Mungu kwa jamii yetu ni yapi katika jambo hili?"

Katika Agano Jipya tunao watu wawili waliooana, Akila na Prisila, ambao walifuata hoja hii kwa dhati. Watu hao wametajwa mara ya kwanza katika Matendo ya Mitume 18. Paulo aliishi nao mjini Korintho kwa sababu walikuwa washona mahema kama yeye Paulo. Kifungu hiki kinaonyesha Akila na Prisila walishirikiana katika kazi hii ya kidunia. (Katika maandishi haya, kazi ya kidunia inamaanisha kazi ambayo inamwezesha mtu kutimiza mahitaji yake ya kimwili na mahitaji ya wengineo.) Ninaamini kuwa, kwa kawaida waume na wake wote hufanya hivyo. Kwa bahati mbaya, katika dunia ya kisasa, kuna watu wachache sana waliooana ambao wanaweza kufanya kazi ya aina moja pamoja. Hata hivyo, ingawa wametengana kimwili wakati wao wa kufanya kazi, huifanya kazi hiyo kwa lengo moja; wanao mwelekeo

mmoja. Kwa mfano, hebu tuseme kuwa mume katika jamii fulani changa yenye watoto anakwenda kufanya kazi au biashara huku mkewe akibaki nyumbani kuwatunza watoto na nyumba. Mume hapaswi kuichukulia kazi yake kama njia ya kuitukuza nafsi yake au kujitafutia heshima katika taaluma yake. Shabaha ya kazi yake ni kumtukuza Mungu, kutafuta njia ya kujiwekea akiba mbinguni, kutimizia mahitaji ya mwili na elimu ya jamii yake. Vivyo hivyo, anapotumia pesa alizozitafuta mumewe ili kuitunza nyumba, mke hapaswi kuwa na lengo la kujifanya yeye na watoto kuwa vielelezo vya mitindo ya nguo katika mtaa wao bali kumtukuza Mungu, na kuwa na njia ya kutimizia mahitaji ya kimwili na kihisia ya jamii yake.

Iwapo mke anafanya kazi mbali na nyumbani, shabaha zake zitakuwa ni zile zile; kazi yake haipaswi kuwa ni njia ya kujitafutia mambo yake binafsi. Lazima pawepo na upatanifu huu wa mwelekeo kuhusu kazi za kidunia hata ikiwa mke na mume hawawezi kufanya kazi moja ama mahali pamoja.

Mume na mke wanapaswa pia kuyatimiza mahitaji ya kihisia, kielimu na kiroho ya jamii yao. Wote wawili wanapaswa kuzingatia kuwafunza na kuwapa mwongozo watoto wao. Wote wawili sharti wajihusishe na shughuli ambazo watoto wao wanazipendelea. Wote wawili lazima wapate wasaa katika ratiba zao wa kuabudu, kufanya maombi kama jamii na kujifurahisha kama jamii.

Akila na Prisila hawakushirikiana tu katika kazi za kudunia bali pia katika kazi ya kiroho. Pamoja walisafiri na Paulo hadi Shamu (Matendo 18:18), pamoja walimhubiria Apolo (Matendo 18:26), na pamoja waliwakaribisha waumini katika nyumba yao (1 Wakorintho 16:19). Wote wawili wametajwa kama wasaidizi wa Paulo katika Yesu Kristo (Warumi 16:3). Watu wawili wafaao kuoana lazima watafute njia za kumtumikia Bwana pamoja na kusaidiana ili kila mmoja aweze kukuza na kutumia kipawa chake cha kiroho. Mume na mke wanaweza kutumika pamoja katika kuwafundisha watoto, kutembelea hospitali na makao ya watu wagonjwa, kutawanya vikaratasi vya mafunzo ya Biblia na kuwahubiria waliookoka na wasiookoka katika mtaaa wao. Ikiwa mume ametunukiwa kipawa cha kuwatumikia watu kwa Neno la Mungu, mke anaweza kuwa na sehenu yake pale wanapojifunza Biblia na kuomba pamoja. Maoni ya mke kuhusu mambo ya kiroho na Neno la Mungu yanapotolewa kwa mumewe faraghani yanaweza kumsaidia sana katika kazi yake ya kuhubiria umma. Hata ikiwa wanazo sehemu tofauti, wanapaswa kuwa na umoja na ushirikiano katika shabaha yao.

Kumtumikia Mungu pamoja kunasaidia kukuza umoja wa watu waliooana na pia utumishi katika kazi ya Kristo. Kwa hakika, umoja wa watu kama hao ni jambo mojawapo katika mambo ya Kikristo (Waefeso 5:28-31). Kufanya kazi pamoja ili kutimiza mahitaji ya kiroho, kihisia, na kimwili katika kila mmoja wao, watoto wao, na watu walio nje ya jamii yao kunasaidia kuimarisha umoja kati mume na mke, ambao hauwezi kupatikana kwa njia nyingine.

## Nyongeza 3

# *Kupotoka kwa Ndoa*

"Apataye mke hupata kitu chema, naye hujipatia kibali kwa Bwana" (Mithali 18:22, UBS). "Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi" (Waebrania 13:4).

Ndoa kati ya mwanamume na mwanamke si jambo la ajali. Mungu aliumba wanyama wote wakuu mume na mke. Noa alia-mrishwa na Mungu kuchukua wawili kati ya kila aina ya mnyama—mume na mke kuwatia ndani ya ngalawa (Mwanzo 6:19). Baada ya kumuumba mtu wa kwanza Adamu, Mungu alimuumbia mkewe kutoka kwenye ubavu wake (Mwanzo 2:22).

Lakini, kuanguka katika dhambi kumefanya ndoa ya mume mmoja na mke mmoja, kama vitu vingine vyote vizuri ambavyo Mungu aliviweka humu duniani, kuchafuliwa na kuharibiwa. Baadhi ya uharibifu huu ni dhahiri kuwa ni dhambi kubwa—kama vile ngono kati ya watu wa jamaa moja na kunajisiwa kwa watoto—kiasi kwamba hapana haja ya kuzieleza. Baba anayejaribiwa kumnajisi binti yake, au ndugu wa kiume dada yake, au msimamizi wa kambi fulani mmojawapo wa wasichana walio kambini mwake, hatashawishika vingine kutokana na maandishi haya au Biblia takatifu kuhusu uovu wa vietendo kama hivyo. Haya ni maswala ya moyoni yanayotokana na kuwa mbali na Mungu. Maneno ya pekee ya kuwashauri watu kama hao ni onyo la Mungu mwenyewe kuwa, "Bali atayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yafaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia na kutoswa katika kilindi cha bahari" (Mathayo 18:6).

Katika nyongeza hii, tutajadili kwa undani aina mbili za uharibifu wa nadoa ambazo zimeenea sana hivi kwamba hata wale wasiokuwa na hatia ya matendo yaho, huwatetea wale wanayo-yatenda matendo yenyewe. Mambo hayo ni pamoja na uzinifu, uzinzi na sinema au

maandishi maovu (au dhambi ya mseto) na madhihirisho tofauti ya dhambi ya ulawiti. Upotovu mwengine ambao utajadiliwa katika sura hii—ndoa za waume au wake zaidi ya mmoja—haujaenea sana katika nchi za kimagharibi hasa kwa sababu umekatazwa kisheria; lakini desturi hii imekubalika sana hata kwenye jamii za Kikristo. Pengine upotovu ulioenea sana wa ndoa—talaka na kuoa au kuolewa tena—umeneea na kukubaliwa sana hata katika Kanisa la Kikristo, licha ya kuwa jambo lenye utata mkubwa, ndipo tumetenga sura tatu tofauti 14-16 katika Mkristo na Ndoa ili kulijadili swala hilo.

## Uzinifu, Uzinzi, na Fasihi Chafu

Sheria ya Saba, "Usizini" (Kutoka 20:14), inaonekana dhahiri na rahisi kueleweka kwa nje, lakini, inapounganishwa na maandiko mengine, huwa ina maana nyingi. Sheria hii imekusudiwa wale wanaoishi au wenye uhusiano na watu wa jinsia tofauti kama watu waliooana. Iwapo tabia hii inahusu watu walioolewa au kuoana, basi huitwa, "uzinifu." Neno "uzinzi" hutumika katika Biblia kuhusu watu ambao hawajaoana. Hata hivyo, "uzinzi" hutumiwa mara nyingi katika Agano Jipya kama neno la kijumla kuwahusu wale walioana ama wale ambao hawajaoana wanaotenda dhambi ya ngono.

Maonyo dhidi ya uzinifu na uzinzi yametolewa mara nyingi katika Agano Jipya: "Msidanganyike, wazinzi na wazinifu hawatauridhi ufalme wa Mungu" (1 Wakorintho 6:9,10).

"Ukimbieni usinzi. Kila dhambi aitendayo mtu huitenda nje ya mwili wake; bali yule mwenye kuzinzi huutendea dhambi mwili wake mwenyewe" (1 Wakorintho 6.18).

"Ili kuepuka uzinzi, kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila manamke na awe na mume wake mwenyewe" (1 Wakorintho 7:2).

"Lakini uzinzi na uhafu wowote na tamaa yasitajwe kamwe miongoni mwenu, kama itastahilivyo watakatifu" (Waefeso 5:3).

"Basi viueni viungo vyenu vilivyo duniani: uzinzi, uchafu,..." (Wakolosai 3:5).

"Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu hata kutakaswa kwenu mwepukane na uzinzi" (1 Wathesalonike 4:3).

"Ndoa na iheshimiwe na watu wote na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu" (Waebrania 13:4).

Kwa mifano zaidi ya maonyo haya, angalia Matendo ya Mitume 15:20,29; 21:25; Warumi 13:9; 1 Wakorintho 5; 1 Wakorintho 10:8;

2 Wakorintho 12:21; Wagalatia 5:19; Yakobo 2:11.

Kuambatana na sheria ya Agano la Kale, adhabu kwa kosa la kuzini ilikuwa kifo: "Mwanamume atakayezini na mke wa mtu mwengine ... wote wawili, mwanamume na mwanamke watauawa. Mwanamume atakayezini na mke wa baba yake ... wote wawili watauawa" (Mambo ya Walawi 20:10-12).

Ingawa adhabu ya kifo haikutolewa kila mara kwa dhambi ya uzinifu, Mfalme Sulemani alifafanua aibu inayotokana na dhambi hii: "Watu hawamdharau mwizi akiiba kujishibisha iwapo ana njaa.... Bali mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa; anafanya jambo litakalomwangamiza nafsi yake. Atapata jeraha la kuvu-njiwa heshima; wala fedheha yake haitafutika" (Mitahli 2:30-33).

Katika Agano Jipya, kwa mwenye kuamini, adhabu ya kifo kwa dhambi ya kuzini imeondolewa na mahali pake kuchukuliwa na nidhamu ya anayopewa mwenye dhambi hii na baraza la kanisa. Katika 1 Wakorintho 5 tunasoma habari ya muumini mmoja katika kanisa la Korintho aliyekuwa anazini na mke wa baba yake. Baraa la kanisa lilishauriwa na Mtume Paulo "kumtoa mtu kama huyo kwa Shetani ili mwili wake uharibiwe lakini roho yake ipate kuokolewa wakati wa kurudi kwake Bwana Yesu, ama kwa maneno mengine, "mwondoeni kati yenu mtu huyo mwovu"(1 Wakorintho 5:5,13). Shabaha ya nidhamu ya namna hiyo ilikuwa ni kumfanya mwenye dhambi kutambua jinsi alivyokuwa amemkosea Mungu kwa kuishi kama mtu asiyeamini na, kwa hivyo, ilitumainiwa kuwa, matokeo yangekuwa ni kurudishwa kwa mwenye dhambi katika ushirika na Mungu na pia ushirika na kanisa. Katika hadithi hii ya mtu huyo wa Korintho, mtu huyo alirudishwa tena katika ushirika huo, Mungu asifiwe, kama tunavyoona katika sura za 2 na 7 za 2 Wakorintho.

Katika wakati huu, ambapo maadili mengi yanapuuzwa kuwa yaliyopitwa na wakati, ni kawaida kwa watu kujishughulisha na ngono. Umma umedanganyika na televisheni, sinema, majarida, magazeti na riwaya kuwa ngono kabla ya ndoa inafaa na pia ni kitu kizuri au sawa kutenda. Tabia hii imekuwa jambo la kawaida kiasi kwamba wata vijana wakristo hushangaa kuona kuwa Biblia inaikataza. Na ingawaje, baadhi ya watu huweza kujizuia kutokana na shinikizo na majaribu ya kuziniwanapokuwa katika uhusiano wa urafiki wa kawaida, hawako tayari kujizuia majaribu zaidi wanapokuwa katika "urafiki wa dhati" au pale wanapojitayarisha kuoana wakati wa uchumba. Baadhi ya watu wanaweza kuuliza, "Ina madhara gani? Tumepanga kuoana." Kwa kuongezea vifungu vingi tulivyodondoa vinavyokataza

uzinzi, tunasoma katika Kumbukumbu la Torati 22:13-21 kwamba ilitarajiwa vijana wa kike waingie katika uhusiano wa ndoa wakiwa bikira. (Na tunaweza kuwa na hakika kuwa maandishi hayo matakatifu yalimaanisha hata vijana wa kiume pia wawe bikira.)

Mariamu hangechaguliwa kuwa mama ya Masihi kama angekuwa ameathiriwa na mawazo ya ulimwengu wa leo—ambayo pia yamewaathiri Wakristo wengi—kwamba iwapo watu wawili ni wapenzi na wamechumbiana ili waoane, basi kiwango chochote cha maingiliano ya kimwili kati yao kinakubalika. Mungu alimtu-kuza Mariamu kwa utakatifu wake na atawatukuza vijana wote wa kiume na kike ambao wanapenda kumpendeza Mungu kwa kubakia bikira hadi wakati wa ndoa na atawawezesha kuwa na ndoa za furaha ya kweli.

Kama ushahidi wa ziada wa neno takatifu dhidi ya ngono kabla ya ndoa, fikiria maneno ya mtume Paulo kwa kanisa la Korintho: "Niliwaposea mume mmoja ili nimletee Kristo bikira safi" (2 Wakorintho 11:2). Ndoa ni mfano wa muungano kati ya Kristo na kanisa lake (Waefeso 5). Hii "Enzi ya Kanisa" ni wakati wa kuposwa kwa kanisa; sherehe ya ndoa haitafanyika hadi kurudi kwake Kristo na kulinyakua kanisa wakati wa "kunyakuliwa" (1 Wathesalonike 4:13-18; Ufunuo 19:7). Kama vile kanisa litakavyoletwa kwa Kristo, Mposaji wetu, vile vile inampendeza Mungu pale wenzi Wakristo wanapoingia katika ndoa wakiwa bikira.

Ingawa wengi wanaweza kumwona Mungu kama asiyependa watu "kujifurahisha," ukweli wa mambo ni kinyume cha maoni haya. "Amri zake sio nzito" (1 Yohana 5:3). Sheria za Mungu zinaonyesha hekima yake kuu na mapenzi yake yasiyo na mpaka kwa wanadamu. Ni yeye pekee ajuaye maana ya "furaha" ya kweli, "baraka" za kweli na "kujifurahisha" kwa kweli. Anafahamu kuwa ingawa furaha ya muda—"Kuji [furahia] kwa kutenda dhambi kwa muda mfupi" (Waebrania 11:25)—inaweza kupatikana kwa kuivunja amri ya saba, raha, furaha, baraka na, nadhubutu kuogezea, kujifurahisha kukubwa zaidi kutapatikana kwa kujiepusha na uzinzi kabla ya ndoa na uzinifu baada ya ndoa. Furaha ya kweli katika ndoa hutokana na kujitolea kwa mume na mkekila mmoja kwa mwenzake: "Kwa sababu hii mtu atamwacha baba na mama yake na ataambatana na mkewe na wote wawili watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24). Pia uhusiano huu una msingi wake katia kutilia mkazo uhusiano wa kiroho (hivi ni kusema, uhusiano wa kila mmoja kwa Mungu na kujitolea kusaidiana kukua kiroho kwa kusoma Neno la Mungu, kuomba, kuabudu na

kumtumikia Mungu pamoja) na vile vile uhusiano wa kihisia (hivyo ni kusema, kukuza mapenzi, huba, kumtunza na kumthamini mwenzake—Waefeso 5:29—wakiwa wasaidizi na kusaidiana nyakati za majaribu na matatizo). Ikiwa uhusiano wa kiroho na kihisia ni thabiti, uhusiano wa kimwili hutazidi kujengeka na kufanywa upya kila mara na utakuwa ndio chanzo cha furaha ambayo undani wake hauwezi kupatikana katika uhusiano wa kawaida nje ya ndoa. Kwa upande mwengine, ndoa imejengeka tu katika msingi wa uhusiano wa kimwili—mara nyingi ukiwa umeanza kabla ya ndoa—uzuri na furaha wa kimwili utayeyuka kwa sababu ya tofauti za kiroho na kihisia, ambazo huchochewa na hisia kama vile hatia ya moyoni, wivu na tuhuma kuhusu ngono nje ya ndoa.

Dhambi ya zinaa sio tu kitendo cha mwili pekee. Bwana Yesu Kristo alibainisha jambo hili katika Hotuba yake Juu ya Mlima: "Mmesikia yaliyosemwa na watu wa kale, Usizini. Lakini nawaambia, Yeyote anayemwangalia mwanamke na kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. Jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe na litupe mbali nawe; maana ni afahdali kupoteza kiungo chako kimoja kuliko mwili wako mzima kutupwa jehanamu" (Mathayo 5:27-29). Onyo hili limetiliwa mkazo katika Agano la Kale kwenye amri iliyorudiwa, "Usiufunue utupu wa..." (Mambo ya Walawi 18:6-18). Amri hii inapanua dhambi ya uzinifu kuhusisha sio tu ngono bali hata kuchezacheza na kupapasa (kufunua utupu wa mtu mwengine kwa mikono yetu) na pia sinema na maandishi machafu (kuufunua utupu wa mtu mwengine kwa macho yetu).

Watu wengi wanaweza kujipongeza kwa kutoanguka katika dhambi ya uzinifu. Lakini ni wangapi wetu tunaoweza kudai kwamba hatujafanya uzinifu katika mioyo yetu? Mfalme Daudi alikuwa na uhusiano wa uzinifu na Bathsheba, mke wa Uria Mhiti. Dhambi hii ilianza mapema pale Daudi, "Alipotembea juu ya dari na kutoka darini alimwona mwanamke akioga na yule mwanamke alikuwa mzuri sana na wa kupendeza machoni" (2 Samueli 11:2).

Katika maandishi ya Kiyahudi yaitwayo Talmud, mna hadithi kuhusu Mkufunzi wa dini (Rabbi) aliyeitwa Amramu na vita vyake dhidi ya tamaa za kimwili: Siku moja, alipokuwa anashindwa kujizuia kuwendea mwanamke mmoja mrembo, Rabbi aliamua kuficha tamaa yake kwa kuingia miongoni mwa umati na kuwaita wenzake kwa kupiga mayowe, "Nyumba yangu inaugua." Hadithi hii husimuliwa miongoni mwa Wayahudi ili kueleza utukufu na heshima ambayo mtu anaweza kujiletea kutokana na juhudi zake za kushinda majaribu na dhambi.

Jambo amablo halitajwi katika hadihi hii ni kwamba watu kama Rabbi huwa tayari wamefanya dhambi kwa kuruhusu tamaa kujaa mioyoni na akilini mwao. Kwa kweli, ingekuwa bora iwapo fikira za tamaa zinaweza kusimaishwa kabla ya kujionyesha hadharani katika kitendo cha uzinzi au zinaa; hata hivyo, fikira zenyewe zinahitaji kuungamwa mbele za Mungu kama kwa vile ziko katika kiwango sawa na dhambi kama vile zinaa mbele ya macho ya Mungu.

Tukimrudia Daudi, tunaweza kujiuliza ni vipi angeepuka dhambi baada ya kumtazama Bathsheba. Kwa hakika, alikuwa na haki ya kutembea juu ya nyumba yake. Angewezaje kujizuia iwapo macho yake yaliangukia mwanamke akiwa uchi kwenye nyumba jirani yake? Mara nyingi hatuwezi kujua ni kitu gani kitakachotokea machoni mwetu bila kutarajia. Lakini tuna hiyari ya lile tutakalotenda baada ya kuona. Tuna uwezo wa kuamua kuondoa macho yetu juu ya kile tunachokitazama au tunaweza kuamua kukaza macho na kuangazia kile kilichojitokeza mbele ya macho yetu. Ni Dhahiri kuwa daudi alitenda hivyo baada ya kumwona Bathsheba kwa mara ya kwanza.

Mara nyingine, majaribu hayajitokezi tu bila kutarajiwa. Tunaweza kuamini kuwa kutokana na yale yaliyokuwa yamemtokea hapo kabla, Daudi alifahamu ni mambo gani ya kupendeza ambayo yaliweza kuonekana mara kwa mara kutoka juu ya nyumba yake. Vile vile tunaweza kukaribisha majaribu kwa kutazama vipindi au senema za aina fulani kutafuta habari katika mtandao (Internet) au kwa kusoma vitabu vya aina au majarida au sehemu fulani za magazeti ambazo haziwezi kukosa habari zinazonuiwa kuibua hisia za tamaa za kimwili. Ninaweza kutambua kuwa nahitaji kuacha kusoma au kutazama mambo kama hayo lakini nikawa bado naendelea kuzama katika majaribu hayo. Nitafanya nini? Pengine naweza kufikiria kuiondolea mbali televisheni, kusimamisha ununuzi wa majarida au niache kutembelea mtandao wa Internet ama kuacha kwenda maktabani. Au, kama ningekuwa Daudi, pengine ningeitupilia mbali hata haki ya kutembea juu ya dari ya nyumba yangu, ama kama hayo hayatoshi, ningemwagiza seremala kufunika dari la nyumba yangu kwa kujenga ukuta mrefu. Hatua hizi zinaweza kuonekana kama kali mno lakini hili ndilo jambo ambalo Bwana Yesu alimaanisha aliposema kuwa, “Iwapo jicho lako la kulia linakukosesha, ling’oe na kulitupa mbali nawe.”

Hapana shaka sababu yetu kuwa wanyonge sana na kuingia majaribuni mara kwa mara ni kwamba tunapuuza kusoma na kutafakari Neno la Mungu na vile vile kuomba na kuzungumza na

Baba yetu aliye mbinguni na kwa sababu hatuenendi katika furaha ya wokovu wetu na kumwonea fahari Mwokozi wetu. Kuling'oa jicho letu, kunaweza kutusaidia, hata kama jambo hilo litahusu nini lakini hata kufanya hivyo hakutakuwa na thamani yoyote iwapo macho yetu ta kiroho hayataelekezwa kwa Kristo. "Yafikirini mambo ya mbinguni wala sio yale ya ulimwenguni" (Wakolosai 3:2).

## Dhambi ya Ulawiti

Kuna ushaidi mwingi kuhusiana na dhambi ya ulawiti. Sodomo na Ngomora ziliharibiwa kabisa na Mungu kwa sababu ya dhambi iliyoenea sana ya ulawiti iliyotendeka katika miji hiyo ya kale (Mwanzo 19:1-25; anagalia hasa kifungu cha 5). Kati ya sheria mbali mbali alizopewa Musa kwa ajili ya wana wa Israeli, tunasoma kwamba, "Usilale na wanaume ka vile ni wanawake; ni machukizo. Wala hutalala na mnyama yeyote ili kujinajisi. Wala mwanamke asilale na mnyama yeyote: ni kuvuruga maumbile. Usijinajisi kwa chochote kati ya vitu hivi; kwa maana katika mambo haya mataifa mengi yalijinajisi ambayo niliyatupilia mbali mbele ya macho yenu. Na nchi imetiwa najisi na kwa sababu hiyo nitailipiza dhambi hiyo juu ya nchi yenyewe na ardhi yenyewe itawatapika viumbe wake" (Mambo ya Walawi 18:22-25). "Kama mwanamume atalala na mwanamume kama anavyoweza kulala na mwanamke, wote wawili wametenda machukizo. Kwa hakika wakauawa; damu yao itakuwa juu yao wenyewe" (Mambo ya Walawi 20:13).

Tunaona maoni ya Mungu kuhusu ulawiti hayajabadilika katika maandishi ya Agano Jipya. Mtume Paulo anazungumza juu ya watu wa Mataifa ambao, "waliabudu na kutumikia kiumbe kuliko Muumba, aliyebarikiwa milele." Kwa ajili ya hayo, kwa hivyo, Mungu aliwaacha wafuate tama zao za aibu, hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo yaliyo haki yao" (Warumi 1: 25-27). Paulo pia anawaandikia wakristo walioko Korintho, "Hamjui nyinyi kuwa wasio watakatifu hawatauridhi ufalme wa Mungu? Msidanganyike: wazinzi, wala waabudu sanamu, wala washerati, wala wafiraji wala walawiti, wala wezi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji wala wanyang'anyi" (1 Wakorintho 6:9,10; na pia angalia 1 Timotheo 1:9,10).

Baadhi ya watu wamedai kwamba Neno la Mungu lililorejelwa hapo juu limekusudiwa kuwaonya dhidi ya tabia iliyoenea sana ya

walawiti kuwa na wenzi wengi ama wanaume wenye mazoea ya kufanya ngono na wavulana wadogo, na kwamba hakuna Neno la Mungu haliwahusu wale wanume au wanawake wenye kujitolea kuwa na uhusiano thabiti wa kimaisha. Ili kuyajibu madai haya, hebu tufikiria mafunzo makuu ya Kibiblia kusu ndoa na ngono.

1. **Ndoa ya Kibiblia.** "Kwa sababu hii, mwanamume ... na ataambatana na mkewe [Neno la Kiebrenia: *ishshah,* ni mke, mwanamke au mtu mwenye jinsia ya kike]" (Mwanzo 2:24). Hakuna mahali katika Biblia ambapo Mungu anawaamrisha wanaume au wanawake wawili kuwaacha wazazi wao na kuambatana pamoja. Biblia inatueleza vizuri kuhusu wake wa Adamu, Kaini, Lameki, Noa, Shemu, ... Akuila, Feliksi na Petero (jumla ya watu kama hao 72 ambao nimewahesabu). Orodha hii haiwajumlishi wake wanaotajwa katika vizazi vingi ndani ya Biblia. Hakuna mfano hata mmoja katia Biblia wa wanaume au wanawake wawili waliokuwa na uhusiano wa kujitolea na wa kudumu wa mfano wa ndoa.

2. **Tunaiga Mfano wa Nani?** "Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake. Kwa mfano wa Mungu alimuumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba" (Mwanzo 1:27). "Kama vile tulivyovaa maumbile ya kilimwenguni, pia tutayavaa maumbile ya mbinguni" (1 Wakorintho 15:48). Mungu, katika "kuwaumba mwanamume na mwanamke" na kuanzisha asasi ya ndoa ya, "mume na mkewe" (Mwanzo 2:25), alikuwa na usudi lingine kuu zaidi katika fikira zake. Uhusiano wa mume na mkewe katika ndoa unakusudiwa kuwa kilelezo cha uhusiano kati ya Kristo na Kanisa.

"Enyi wake, watiini waume zenu kama vile kumtii Bwana wetu. Kwa sababu mume ni kichwa cha mke, kama Kristo alivyo Kichwa cha Kanisa: na ni Mwokozi wa mwili. Kwa hivyo, kama Kanisa lilivyo na utiifu kwa Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Waume, wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda Kanisa hata akajitoa kwa ajili yake.... Kwa ajili hii mume atamwacha baba na mama yake na ataambatana na mkewe na wote wawili watakuwa mwili mmoja. Hii ni siri kubwa: lakini lakini nazungumza juu ya Kristo na Kanisa" (Waefeso 5:22-32; Wakolosai 1:18,19).

"Lakini, ningependa mjue kwamba Kichwa cha kila mwanamume ni Kristo; na kichwa cha mwanamke ni mwanamume; na Kichwa cha Kristo ni Mungu" (1 Wakorintho 11:3).

"Nawaonea wivu, wivu wa Mungu. Kwa maana naliwaposea mume mmoja ili nimletee Kristo bikira safi" (2 Wakorintho 11:2).

Yule aliye na bikira ni Bwanaharusi; lakini rafiki ya Bwanaharusi

anayesimama na kumsikia hufurahi sana kwa sababu ya sauti ya Bwanaharusi: Furaha yangu, kwa hivyo, imetimilika" (Yohana 3:29). "Tufurahi na kushangilia; na kumtukuza Yeye; kwa sabau harusi ya Mwanakondoo imefika na Mke wake amejitayarisha" (Ufunuo 19:7).

Kila Mkristo mwanamume na mwanamke ana wajibu wa kuvaa mfano wa Kristo, aliyeumbwa kwao na mfano ambao umefanywa upya katika uzao mpya (Warumi 8:29; 2 Wakorintho 3:18; 5:17). Isitoshe, kila mume Mkristo na mkewe wana wajibu katika ndoa yao wa kufuata mfano wa uhusiano wa Kristo na Kanisa. Kinyume cha kauli hii ni sawa pia: kuujua uhusiano wa Kristo na Kanisa huwasaidia Wakristo waliooana kuwekea mipaka uhusiano wao wenyewe.

Je, uhusiano wa kudumu wa ngono kati ya watu wawili wa jinsia moja unaashiria, kufuata au kuonyesha nini? Uhusiano wa mume na mume unaonyesha mfano wa Kristo akiwa pekee? Uhusiano wa mke na mke unaashiria mfano wa Kanisa likiwa peke yake? Biblia haielezi chochote kuhusu jambo hili na pia vile vile haitoi ushauri wowote kwa watu waliomo katika uhusiano wa jinsia moja. Hapana mafunzo yanayofanana na yale yaliyomo katika 1 Wakorintho 11 na Waefeso 5 kwa watu wa ndoa ya jinsia moja, kuhusu ni yupi atakuwa kichwa, yupi atakuwa mtiifu, yupi atampenda mwenziwe na ni yupi atajitolea kwa mwenzake. Pia hapana mafunzo kuhusu malezi ya watoto katika uhusiano wa jinsia moja ambao watakuwa na wazazi wawili wanaofanana huku wakimkosa mzazi wa jinsia ya pili. Naamini kuwa sababu ya kutokuwapo kwa mafunzo kama haya katika Biblia ni kwamba uhusiano wa jinsia moja ni kinyume cha Neno la Mungu. Uzito wote wa Neno la Mungu unapinga uhusiano kama huo.

3. **Uhusiano Uliokatazwa wa Ulawiti.** Katika Mambo ya Walawi 18 tunapata orodha ndefu ya mahusiano kati ya waume na wake. Hata hivyo, hapana mafunzo ya kukataza uhusiano wa mume na mume au mke na mke isipokuwa, kifungu cha kijumla kisemacho, "Usilale na mwnamume kama mfano wa kulala na mwanamke" (Kifungu cha 22).

4. **"Wanaume kwa Wanaume."** Katika Warumi 1:27 tunasoma, "Wanaume [*arsenes*] kwa wanaume [*arsenes*], wakifanya yale yasiyopasa" sio "wanaume na wavulana." Neno *arsenes* linamaanisha "mwanamme [kinyume cha *thelus,* mwanamke], dume lenye nguvu. Neno la Kiingereza "arsenic" linatokana na neno hili la asili. Huu sio mfano wa mwanamume mzima mwenye nguvu akiwanyanyasa wenzake wadhaifu au wavulana wadogo kwa kutafuta, "mapenzi." Lakini ni mfano wa wanaume wawili wenye nguvu—wenzi walio sawa. Wagriki

walitumia neno kuelezea uhusiano kati ya mwanaume na mvulana kwa neno *paiderastes* ambalo kutokana nalo tunapata neno la Kiingereza, "pederasty." Kama Mtume Paulo angefikiri kwamba Roho Mtakatifu alikuwa anamaanisha neno hili, bila shaka angelitumia neno hilo.

5. **Wenye Kujitia Najisi na Wanadamu.** Kifungu hiki cha kipekee kinachotokea katika 1 Wakorintho 6:9 ni tafsiri ya neno moja la Kigriki, *arsenokoitai* na pia linapatikana katika 1Timetheo 1:10. Neno hili linafanana sana na neno *(arsenes)* lililotumiwa mara mbili katika Warumi 1:27, na kwa jumla linamaanisha "ngono ya wanaume" au "ngono kati ya wanaume." Maelezo yangu katika sehemu ya namba 3 hapo juu, yanafaa hapa pia.

Ni jambo la kufedhehesha kuwa makanisa mengi yanayodai kuwa ya Kikristo yanawaruhusu walawiti kushiriki meza ya Bwana na hata kuwa Wazee, wachungaji na makasisi. Lakini si ajabu kuwa jambo hili linatokea kwa vile jambo hili lilitanguliwa na kuruhusu dhambi ya ngono kati ya wanawake na wanaume katika makanisa. Ikiwa wazinzi na waasherati wataruhusiwa kwa nini walawiti wasikubaliwe pia? Hili limekuwa ni swali wanaloulizwa wanajamii ya walawiti na ambalo linafaa kuulizwa. Ni unafiki kuhubiri dhidi ya walawiti huku kanisa likiwakaribisha wazinzi na waasherati kuwa washiriki. Kumekuwa na mahubiri ya dhati katika siku za hivi karibuni katika radio na televisheni dhidi ya dhambi ya ulawiti huku kukiwa na sauti hafifu dhidi ya dhambi ya ngono kati ya wanaume na wanawake ambayo imeena sana na pia kama ulawiti huweza kuharibu uhusiano wa watu.

Tunahitaji kudumisha utakatifu wa kibinafsi na pia utakatifu katika makanisa yetu sio tu dhidi ya dhambi ya ulawiti bali pia dhidi ya dhambi ya ngono kati ya wanaume na wanawake. Na pia tukumbuke kuambatana na mafunzo ya Bwana Yesu katika Hotuba Mlimani kwamba utakatifu unatokana na masiha yetu na fikira zetu, hutokana na kujisafafisha mioyoni mwetu dhidi ya uasherati.

## Ndoa ya Mume Mmoja na Wake Zaidi ya Mmoja

Ijapokuwa, ndoa ya mke mmoja na zaidi mume mmoja au, kama inavyotokea mara nyingi, mume mmoja na wake zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja, sio halali katika Marekani na katika mataifa mengi ya Kimagharibi, hutokea sana, kama ishara ya umaarufu na cheo katika jamii katika mataifa mengine. Ni vigumu kufafanua desturi hii kwa mujibu wa Biblia kwa sababu desturi yenyewe ilikuwa imeenea sana miongoni mwa wateule wa Mungu wakati wa Agano la Kale, wala Mungu hakuilaani.

Sababu zinazotolewa dhidi ya ndoa ya wengi huingiliana na zile zinazotolewa dhidi ya tabia ya ulawiti. Mungu alimwuumbia mtu wa kwanza, Adamu, mke mmoja wala sio wawili au wengi. "Kwa sababu hii mtu atamwacha baba na mama yake na ata-ambatana na mkewe na wote watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:24). Bwana Yesu anafafanua jambo hili kwa kunukuu kifungu hiki cha Agano la Kale kwa kusema, "Na wote *wawili* [sio *watatu* au *wanne*] watakuwa mwili mmoja. Kwa hivyo wale wawili sio wawili tena bali mwili mmoja. Wale ambao Mungu amewaunganisha, mtu yeyote asiwatenganishe (Mathayo 19:5,6). Mwanamume hawezi kuwa mwili mmoja na wake wengi.

Mafunzo kuhusu "Tunaiga Mfano wa Nani" juu ya dhambi ya uasherati hapo juu, pia yanafaa hapa. Ikiwa uhusiano kati ya mume na mke ni kielelezo cha uhusiano kati ya Kristo na Kanisa, mume mmoja na wake watatu wanaonyesha mfano wa nani? Kristo na makanisa matatu?

Wanaume walioteuliwa kuwa viongozi (au wasimamizi) na mashemazi katika makanisa walihitajika kuwa, "waume wa mke mmoja" (1 Timotheo 3:2,12; Tito 1:6). Mafunzo haya hayawahusu Wakristo ambao sio viongozi wa kanisa. Hata hivyo, kwa vile ni jambo la kawaida kwa viongozi Wakristo kuwa na wake wengi, kama ishara ya vyeo vyao katika jamii, vifungu hivi vinawazungu-mzia watu kama hao.

Wakati Yesu aliponukuu Mwanzo 2:24 akiongezea, "Kile Mungu alichokiunganisha asije mtu akakitenganisha," Mafarisayo waliitikia kwa kumwuliza, "Kwa nini basi Musa aliamuru mke kama huyo (Mwaasherati) apewe baua ya talaka na kuachwa?" Bwana aliwajibu, "Musa, kwa ajili ya ugumu wa mioyo yenu, aliwaruhusu kuwaacha wake zenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo" (Mathayo 19:6-8). Inaweza kuwa ni kwa sababu hiyo ndipo Mungu alipowavumilia wanaume walioa wake wengi kama vile Abrahamu, Yakobo na Daudi. Ingawa watu wote watatu hawa wanatajwa kama mashujaa wa imani (Waebrania 11), misingi ya imani yao haikuwa mikamilifu kama ile ya waumini wa Agano Jipya ambao imani yao ilijengeka kutokana na sadaka ya mateso, kifo na kufufuka kwa Bwana Yesu Kristo.

Ingawa Mungu hakulaani ndoa ya wake wengi miongoni mwa wateule wake wa Israeli, ni muhimu kuelewa athari za wake wengi juu ya uhusiano kati ya mume na mke na kati ya mke na mke mwenza.

**Sarai na Hajiri.** Wakati Hajiri alipoona kuwa amepata mimba, alianza kumchukia Memisabu wake Sarai ... na wakati Sarai

alipomnyanyasa, Hajiri alikimbia kutoka machoni pake ... na Hajiri akamzalia Abrahamu mwana wa kiume ... Ishmaili" (Mwanzo 16:1-15). Matokeo ya huusiano huo bado tunayaona kila siku leo, miaka 4,000 badaye katika mzozo baina ya vizazi vya Isaka, mwana wa Sarai na vile vya Ishamaeli, mwana wa Hajiri.

**Lea na Rakeli.** Yakobo "alimpenda Rakeli kushinda alivyompenda Lea.... Na Mungu alipoona Lea anachukiwa, alifungua kizazi chake; lakini Rakeli alikuwa tasa ... na Rakeli alipoona hamzalii Yakobo wana, alimwonea wivu dada yake, na akamwambia Yakobo, nipe watoto nisije nikafa. Na hasira ya Yakobo ilimwakia Rakeli" (Mwanzo 29:16-30:2).

**Anna na Penina.** Elikana ... alikuwa na wake wawili ... Penina alikuwa na watoto lakini Anna hakuwa na watoto.... Mke mwenza wake [Anna] aliamdharau sana ili kumkasirisha kwa sababu Mungu alikuwa amefunga kizazi chake.... [Anna] aliudhika sana moyoni" (1 Samueli 1:1-10).

**Mikali na Wake Wengine wa Mfalme Daudi.** "Kisha Daudi akarudi kuibariki jamii yake. Na Mikali binti yake Sauli akajitokeza na kukutana na Daudi akisema, Mfalme wa Israeli alikuwa mtukufu jinsi gani leo hata akajivua nguo na kuwa uchi mbele za vijakazi vya watumishi wake kama afanyavyo mtu mmoja wapo mjiga anavyojivua nguo na kuwa uchi mbele za watu bila kuona hya!" (2 Samueli 6:20). Mikali alikuwa mke wa kwanza wa Daudi—zawadi yake kwa kumwuua Goliathi. Tunasoma mara mbili kuwa Mikali, bintiye Sauli alimpenda Daudi" (1 Samueli 18:20,28). Lakini Mikali alipomsaidia Daudi kutoroka ghadhabu ya babake, Sauli alimpokonya yeye kutoka kwa Daudi na kumwoza mtu mwengine (1 Samueli 19:11-17; 25:44). Miak mingi baadaye, baada ya kifo cha Sauli na wakati Daudi alipokuwa mfalme, kwa upumbavu na uovu wake, daudi alimlazimisha Mikali kumwacha mumewe na kuwa mke wa Daudi tena (2 Samueli 3:14-16). Hata hivyo, wakati huu, Mikali alikuwa tu mmojwapo wa wake wengi na mahawara wengi wa Daudi (2 Samueli 3:2-5; 5:13-16), na ni dhahiri hakuwa anampenda Daudi tena.

**Wake wa Solomoni.** "Mfalme Solomoni aliwapenda wake wengi wageni pamoja na binti yake Farao, wake wa Kimoabi, Kiedomi, Kizidoniani na Wahatiti.... Na alikuwa na wake 700, malkia na mahawara 300; na ... wake wake waliupindua moyo wake akaifuata miungu mingine ... na moyo wake haukuwa imara na mbele za Bwana Mungu wake.... Na Solomoni alifanya dhambi machoni pa Bwana" (1 Wafalme 11:1-8).

Kwa hivyo, ingawa wanaume hawa wote hawakukakazwa kuoa wake wengi, ni dhahiri kutokana na hadithi zao za kusikitisha kwamba mpango wa Mungu kutoka mwanzo ulikuwa kila mwaaumume kumwoa mke mmoja.

Iwapo mume mwenye wake wengi atajifunza Neno la Mungu na kutambua kuwa kuoa wake wengi ni jambo baya, atafanya nini? Akimtaliki mke au wake zake wote atavunja Neno la Mungu (Mathayo 5:32; 19:9). Vifungu vifuatavyo vinafaa hapa: "Mtu akiokoka akiwa ametahiriwa, asijigeuze na kuwa kama asiyetahiriwa.... Kila mtu na adumu katika wito ambamo aliitwa.... Ndugu zangu kila mtu katika hali alimoitwa na adumu vivyo hivyo katika Mungu" (1 Wakorintho 7:18-24). Naamini katika muktadha wa sura hii nzima, hivi ni kusema kuwa iwapo mtu amekwishafanya msururu wa ndoa au talaka kinyume cha Neno la Mungu kabla ya kuokoka, mtu kama huyo hana lazima ya kuacha ndoa yake aliyo nayo ili kurekebisha maisha yake ya hapo awali. Je, kauli hii haimhusu pia Mkristo ambaye, kwa kukosa ufahamu wa Biblia au kwa kuwa mbali na Bwana, ameoa wake wengi kimakosa? Wakati mtu kama huyo anaposikia sauti ya Bwana, na kuunganishwa tena na Bwana kimwili na kiroho, na awe anataka kutenda lililo sawa kulingana na Neno la Mungu, "anapaswa kubakia katika wito alimoitwa." Mafunzo yaliyomo katika 1 Timotheo 3 na Tito 1 yanasisitiza kuwa viongozi Wakristo waliooa wake wengi wanapaswa kujiondoa katika uongozi.